Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Nane – Tarehe 8 Novemba, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunazo hati za kuwasilisha mezani.

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2011.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema leo ni siku ya Alhamisi, tunakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu. Hata kama mlioomba kuzungumza leo ni wengi zaidi kuliko kawaida, lakini tunaanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye yupo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumuuliza swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba Taifa letu sasa hivi linapita katika mchakato wa kutafuta maoni ya Watanzania kuhusu Katiba mpya iliyopendekezwa. Pamoja na Serikali kutoa ahadi yake kwamba, ingependa Katiba hii iwe tayari kabla ya Uchaguzi wa mwaka 2015, bado ni jambo la kupenda, lakini linaweza lisiwe la uhalisia.

Sasa swali langu, kwa kuwa mchakato wa Katiba hautoi mamlaka kwa Serikali kuvunja Katiba iliyopo na kwa sababu Katiba inatoa mamlaka kwa kila Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 kupiga kura. Pia kwa sababu tangu Uchaguzi Mkuu uliopita tumeendelea kufanya Chaguzi mbalimbali bila kuthamini kwamba tuna watu ambao tunawanyima uhuru wa kupiga kura kwa sababu daftari la kudumu la kupiga kura bado limepitwa na wakati.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 19 Aprili, nilikuuliza swali hapa kuhusiana na mpango wa Serikali hasa Ofisi yako katika kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura na ulitoa ahadi ya Serikali ya kulifanyia kazi jambo ambalo mpaka sasa hivi halijatekelezwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, una kauli gani ya kuwaambia Watanzania kuhusiana na hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ingawa swali lenyewe limezunguka zunguka.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Tanzania tumeweka utaratibu wa upigaji kura na namna gani tunaweza tukawapata wale wote wenye kustahili kupiga kura waweze kupata fursa ya kupiga kura na utaratibu wa lile daftari la wapiga kura ilikuwa ni juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba hakuna Mtanzania tunayemwacha nje ya utaratibu huo. Ndiyo maana katika daftari lile tulipoanza tukaweka na utaratibu vile vile wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na utaratibu wa kuendelea kuliboresha daftari lile mara kwa mara ili tusije tukamwacha mtu au tusije tukaenda na watu ambao tayari pengine bado hawako hai.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado naamini utaratibu ule ni mzuri na kama nilivyoahidi ni kitu ambacho kiko ndani ya utaratibu wa Tume na sisi kazi yetu ni kuiwezesha Tume kutekeleza hilo jukumu wakati wanapohitaji Serikali kusaidia. Kwa hiyo, tutaendelea kuifanya kazi hiyo kwa moyo mkunjufu na wala hatuna dhamira yoyote ya kutaka kumnyima fursa mtu yeyote kwa sababu hatuna sababu ya kutokufanya hivyo. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba bado tuko katika mstari sahihi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu yako mazuri, naomba kukuuliza swali moja la nyongeza. Ni dhahiri kwamba, nia njema ya Serikali haitoi mamlaka ya Serikali kuvunja Katiba. Bado nasisitiza kwamba utaratibu uliowekwa wa kuboresha daftari, kama utaratibu huo unakiuka misingi ya Katiba na mamlaka ya Katiba basi ni utaratibu ambao ni batili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, maadam hakuna *guarantee* ya kumaliza mchakato mzima *in time* na kwa sababu suala la Uchaguzi ni suala *sensitive* sana katika nchi. Ni kwa nini Serikali sasa isiweke mkakati wa makusudi wa kuanza kuboresha sheria mbalimbali hususan sheria inayosimamia Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na hii sheria sasa *PVR* ili mambo haya yaweze kufanyika bila ya kusubiri mchakato mzima wa kubadilisha Katiba?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika ni kwa nini Mheshimiwa Mbowe anatanguliza wasiwasi wa kutokufikia lengo ambalo tumelipanga kwa dhamira njema. Kwa sababu nadhani kubwa hapa kwanza tuamini kwamba, tunakwenda kwa mpangilio kama tuliokuwa tumeamua kwa imani kwamba, itakapofika mwaka 2014 ile Katiba itakuwa imefikia katika hatua zake za mwisho na kwa hiyo tutaingia kwenye Uchaguzi mwaka 2015 tukiwa na Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ndiyo imani niliyonayo na juzi nilikuwa nazungumza na Mwenyekiti wa Tume, Mzee Warioba akasema bado yeye ana imani kubwa kabisa kwamba tutaweza kulifikisha jambo hili kama tulivyokuwa tumepanga. Sasa ni kweli, inawezekana kwa sababu moja au nyingine kwa sababu ule ni mchakato, kukatokea mambo ambayo yanaweza yakafanya pengine tukatoka kwenye msitari ule, jambo ambalo tunaweza vile vile tukaangalia namna gani tufanye.

Nakuomba basi usiwe na hofu, tuwe na imani kwanza. Lakini ushauri wako kwamba pengine Serikali ianze kutazama sheria mbalimbali ambazo zingeweza kusaidia kuimarisha mfumo wetu endapo hakutakuwa na maafikiano katika hatua tulizokuwa tumekubaliana, ni ushauri mzuri na sisi tutauangalia, tutaona kama pengine kuna haja ya kufanya hivyo au pengine tuendelee na imani ambayo tunayo hadi sasa.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, ukimwondoa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, wachangiaji wako tisa, kwa hiyo kama mtakuwa mnauliza *direct,* naamini tunaweza tukawamaliza, lakini kama mtazunguka basi wengine watakosa nafasi. Sasa nimwite Mheshimiwa Khatib Said Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jeshi la Polisi ndicho chombo chenye dhamana ya kulinda na kusimamia usalama wa raia na mali zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Hupaswi kusoma.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 13 kifungu (6)(b). Naomba kunukuu inasema: “Ni marufuku kwa mtu yeyote aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.” Ibara hiyo hiyo kifungu cha 6(e) inasema, naomba kunukuu tena: “Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza na kumdhalilisha”.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa imetokea tabia ya Jeshi la Polisi kwa baadhi ya maeneo katika nchi hii wakati wanapoendesha harakati zao au operesheni zao kufanya mateso makubwa kwa raia ambao hawajathibitika kama wana hatia.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni nini kauli ya Serikali kuhusu utendaji huu wa Jeshi la Polisi ambao unapelekea maeneo mengine kuacha maumivu makubwa kwa raia ambao hawajathibitika kwamba wana makosa? (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba, kwa bahati mbaya swali unajua limewashtaki Mapolisi kwa ujumla mno. Kwa hiyo, linanipa taabu kidogo namna ya kujaribu kulijibu maana umetoa picha kana kwamba Jeshi la Polisi lote ndio matendo yao, sidhani kama ni kweli.

Mheshimiwa Spika, nafikiri cha msingi kama liko shauri mahsusi ambalo Jeshi la Polisi kwa namna ulivyolieleza limekiuka taratibu nadhani suluhu ya kweli, hebu tupe hiyo taarifa sisi tuifanyie kazi na wale wahusika wote kutegemea na mazingira yalivyo tunaamini watachukuliwa hatua stahiki kwa sababu sheria ni sheria na wala hakuna anayeweza kucheza na sheria hata kama ni Polisi mwenyewe. Kwa hiyo, tunachotarajia ni kwamba, katika kutekeleza majukumu watatekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria na taratibu tulizojiwekea.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni kulitokea matukio mawili ya mauaji ya kufanana katika nchi yetu. Kulitokea mauaji ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza na pia kulitokea mauaji ya askari wa kawaida pale Kisiwani Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, askari kwa upande wa Tanzania Bara wameweza kufanya upelelezi na utekelezaji wao wa kisayansi wa kazi zao uliopelekea kukamatwa kwa wahalifu wale ambao mpaka sasa hivi tuna taarifa kwamba wameshapelekwa Mahakamani, pasipo na kuathirika raia wengine kwa vipigo, mateso wala udhalilishaji.

Tofauti na yanayoendelea kutokea Zanzibar, hadi tunavyoongea tukio la kuuliwa askari yule limepelekea raia wengi kunyanyaswa, kupigwa na kuumizwa vibaya na hadi tunavyozungumza wengi wao wako Magerezani na wakati tukio linafanana. Je, kuna maelekezo maalum yanayotolewa kwa askari wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yao? Naomba jibu (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, lazima nikiri sina ufahamu wa kutosha juu ya tukio analolieleza. Kwa sababu kama askari yule ameuawa, kazi ya askari ilikuwa ni kutafuta nani amesababisha kifo cha huyo askari.

Sasa kwa maelezo yako Mheshimiwa Mbunge inaonekana ama katika kufanya hiyo kazi raia wengine hovyo hovyo tu wamekamatwa wanapigwa, wananyanyaswa na ndiyo maana nasema sina uelewa wa kina juu ya tatizo hili kutokana na kifo cha huyo askari. Lakini nikuahidi basi, nipe muda ili nipate maelezo, nione nini hasa kimetokea halafu tuone ni hatua gani stahiki tunazoweza kuchukua kusaidia kuondoa hilo tatizo. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa wananchi wa Kata ya Namonge, huko Bukombe katika maeneo ya Muhama, Nyamagangwalwa, Mtukula, Nyansato wanahangaika sana kwa sababu Maafisa Maliasili kutoka Wilaya jirani ya Biharamulo wamefika pale kupima eneo la hifadhi upya. Sasa wanahangaika hawana makazi na hivi leo nimeongea na Diwani wa kule anasema kwamba zaidi ya watu kama 7,000 hawana makazi, wamehama kwa sababu wanaogopa watavamiwa na Ma-*game*.

Swali, unawaambia nini wananchi hawa ambao wanahangaika na unawaambia nini hawa Maafisa ambao wamefanya zoezi hili bila ya kuzingatia misingi ya Utawala Bora ambayo inahusisha pia msingi wa ushirikishaji? Ahsante.

**SPIKA:** Swali lina namna ya eneo kabisa kabisa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitoe ushauri. Ningelikuwa mimi ningekuwa nimemletea Waziri Mkuu hilo jambo mapema sana akalifanyia kazi, akapata maelezo, bado tukakuruhusu ukaniuliza hilo swali kwamba nilikueleza hivi na hivi Waziri Mkuu lakini naona bado kuna kitu kinaendelea. Sasa mimi ndio nalipata hapa, ni tukio lipo kwenye ngazi ya Kata, kwa kweli mimi bila ya kuwa na ufahamu kabla, sitaweza kulieleza vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo maana nilikuwa na...

**WAZIRI MKUU:** Lakini nikuahidi tu kwamba, ili mradi umenipa hiyo taarifa acha na mimi nilifanyie kazi kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii tuone kilichotokea hasa ni nini, nione kama ni kweli katika jitihada hizi za Maliasili kupima upya, kuna dhuluma zozote zimefanyika au hapana.

**SPIKA:** Kwa hiyo, nakuagiza kwamba uliandike vizuri umpelekee Waziri Mkuu kusudi apate hizo habari kutoka hiyo Kata.

Mheshimiwa Mbunge tofauti ya hili sakata limetokea leo, tena kwenye Kata, ukimwuliza Waziri Mkuu hapa, kweli inakuwa shughuli kabisa.

Tunashukuru, sasa nimwite Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu.

**MHE. MWIGULU L.M. MADELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Watendaji wengi sana hapa nchini ngazi ya Vijiji, Kata, Tarafa na Halmashauri wanakaimu vyeo kwa kipindi kirefu. Hali hii inasababisha wasifanye maamuzi na wengine wanaokaimu hawana uwezo, hivyo inasababisha miradi kudorora. Jambo hili tulilileta, tukapewa taarifa kwamba lilikuwa linasubiri bajeti. Sasa tunakwenda nusu ya mwaka wa kifedha, ni nini kauli ya Serikali? (*Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nijaribu kutoa maelezo kwa ufupi sana juu ya suala hili ambalo Mheshimiwa Mchemba ameuliza.

Kwanza nataka kusema kwamba, kwa ushauri uliotokana na Wabunge hapa Serikali ilisharidhia kwamba nafasi fulani fulani katika ngazi ya Serikali za Mitaa zirejeshwe chini ya Mamlaka ya Halmashauri. Watendaji wa Vijiji hawa ni katika kundi lile ambalo tumekubali washughulikiwe na Halmashauri zenyewe. Kwa hiyo, napenda niamini kwamba mamlaka sasa ambazo zitashughulika na ajira hata kama ni kuthibitishwa, kama ni kupewa nafasi za kazi ni kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sasa pengine kwa hili ambalo Mheshimiwa Nchemba ameliuliza labda nimuahidi tu kwamba, tutaangalia tuone kitu gani kimetokea mpaka sasa bado Watendaji hawa hawajathibitishwa kuwa Watendaji kamili. Inawezekana kukawa na na tatizo la fedha ama inawezekana maamuzi yale ambayo Serikali imekwishafanya pengine hayajawafikia kwenye Halmashauri zenu.

**SPIKA:** Ahsante. Nadhani ameridhika, sasa nimwite Mheshimiwa David Zacharia Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Watanzania na nchi ya Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo ardhi imekuwa moja ya alama ya ujamaa kwamba, unapokosa nafasi ya biashara kokote kule Mtanzania maskini anaweza akaenda kushika eka mbili, tatu, akajikimu kwa kilimo kwa kuendesha maisha yake. Hii ni tofauti kabisa na duniani kwingine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka sasa kuna wimbi kubwa, kuna mjadala mkubwa kuhusu Mataifa ya kibeberu hususan Marekani kuteka eneo kubwa la ardhi ya Tanzania kwa kisingizio cha kilimo, naomba kukuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa utaratibu huu wa kuacha ardhi mikononi mwa mabeberu ndiyo ambao umesababisha machafuko, baadhi ya nchi za Afrika hususan Zimbabwe, lakini kwa Tanzania tayari umeanza kusababisha machafuko hususan Kigoma Kusini ambako tayari kuna wakulima wamehamishwa na mwekezaji anaitwa *FELISA*, kuna wakulima wamehamishwa na mwekezaji anaitwa *AGRISOL,* wamepigwa na mpaka sasa kesi ziko Mahakamani. Naomba kauli ya Serikali ni kwa nini isisitishe utaratibu wa kuwapa hawa wawekezaji ardhi, ibakishe ardhi mikononi mwa wazawa mpaka pale wazawa watakapothibitika kushindwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la ardhi linaonekana linagusa hisia za watu wengi na ni kweli vile vile kwamba, ni vizuri Serikali na sisi tukazingatia hizo hisia. Lakini nataka niseme kwa shauri ambalo Mheshimiwa Kafulila unalisema; kwa sababu unajua ardhi hapa nchini inapogawiwa na hasa kama inagusa maeneo ambayo yako ndani ya Halmashauri zetu, hakuna kitakachofanyika pale kama Halmashauri haijatoa kauli yake ama ardhi hiyo itumike kulingana na mazingira yake au hapana.

Hakuna anayetoka na uamuzi huku juu kwenda kwenye eneo lolote ambalo liko ndani ya Halmashauri ya Wilaya bila kwanza kupata ridhaa ya Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, nafikiri kimsingi hapa hili jambo lingezungumzwa kwanza kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu

muone mambo yaliyojitokeza, tuone ni namna gani tunaweza tukaondokana na hilo jambo. Kama mnaona kwamba hakuna sababu ya kuwa na hiyo ardhi, muishauri Serikali, tulitazame, tukubaliane nini tufanye kwa sababu huo ndiyo msingi mmoja mkubwa sana.

Lakini ndugu yangu Kafulila, mimi ni mmoja wenu kama Watanzania wengine wote. Lakini bado sijaamini kabisa kabisa kwamba ardhi inapoendelezwa na mtu alimradi tu ametoka nje kama mwekezaji ionekane kama ni dhambi, kweli? Kwa sababu naona ndiyo hisia ambazo zinajengwa muda wote.

Ninachosema ardhi ili iweze kuwa ni kitu cha kuleta maendeleo katika nchi, lazima tuigeuze, tuilime na tuhakikishe kwamba inakuwa *productive*. Vinginevyo tutapiga siasa kwenye eneo la ardhi, mtakuwa mnaruka mnaona mapori asubuhi mpaka jioni, badala ya kuyaendeleza sisi tunaona kama vile ni dhambi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nataka niamini jambo hili liko ndani ya uwezo wa Halmashauri yako na kama ninyi mnaona hakuna sababu ya mwekezaji kutumia ardhi hiyo, ninyi ni juu yenu kulisema, kutushauri na sisi tutaangalia, tutashirikiana na ninyi na mwisho tutaona nini tufanye kwa pamoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi binafsi naamini ardhi kuwapa wageni ni dhambi. Eneo hilo ambalo nalizungumza ni kwamba, mjadala ulifanyika ndani ya Halmashauri na maamuzi kufikia. Mimi kama Mbunge naomba nitoe taarifa hii Bungeni kwamba kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka pale Halmashauri, eneo lile walilitoa, lakini bado kuna hisia za manung'uniko na kwamba palikuwa na nguvu kutoka juu kufikia uamuzi ule.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuzungumza haya mambo, hii kitu ni *very sensitive*. Eneo lile ambalo mmelitoa kwa mwekezaji wa *AGRISOL* ndipo ambapo mmetenga kuwa Makao Makuu ya Wilaya. Kwa tafsiri nyingine ni kwamba, Makao Makuu ya Wilaya yatazungukwa na mashamba ya mwekezaji. *This is very dangerous.* Naomba kauli ya Serikali tena kwamba kama Waziri Mkuu ambaye Halmashauri zote ziko chini yako uagize au utoe kauli jambo hili lisitishwe.

**SPIKA:** Maliza, hatujadili sasa.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu nayazungumza haya naamini uamuzi wa kugawa ardhi ni kinyume hata cha sera ya chama chako. Chama cha kijamaa hakiwezi kugawa ardhi kwa mabepari.

**SPIKA:** Uliza swali usijadili.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, swali ambalo namuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba, eneo lile ambalo mmeligawa la hekta 10,000 sawa na ekari 25,000 ndipo ambapo yalipo Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza. Kwa hiyo, mpo tayari Makao Makuu ya Wilaya yazungukwe na shamba la Mzungu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Kafulila mwenyewe anakiri kwamba kumbe lilipita kwenye Halmashauri yake. Sasa kama limepita kwenye Halmashauri yako hizo hisia zako za mashinikizo na nini haziyana msingi. Maana ninyi ndiyo mnasisitiza utawala bora wa Sheria, ninyi ndiyo mnatuasa sana tuache vyombo hivi vya Halmashauri vifanye maamuzi. Sasa maamuzi yamefanywa na Halmashauri yako, unakuja unamkoromea Waziri Mkuu na kumtaka afanye hili. Nenda kazungumze na Halmshauri yako. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa kuna mgogoro kati ya Makatibu Tarafa nchi nzima na Serikali yao kutokana na waraka uliotolewa mwaka huu wa kurekebisha mishahara yao kutoka kima cha *TGS-F* mpaka *TGT-F4* kwa maana ya shilingi 856,600/- mpaka shilingi 470,000/- bila kujali umri wao kazini. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali haoni kwamba waraka huu hautawatendea haki Makatibu Tarafa hawa ukilinganisha Makatibu Tarafa waliostaafu mwaka huu mwezi Januari mpaka Mei wamepata malipo makubwa na atakayestaafu mwaka huu Novemba atapata malipo madogo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri jambo hilo na mimi nimeshaletewa na ni kweli inaonekana kuna mkanganyiko katika maamuzi yaliyofanyika kuhusu Maafisa Tarafa na tayari tumeshaiagiza Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wapitie tena yale maelekezo waliyoyatoa, waangalie wapi hasa tulipokosea. Kama tumekosea halafu wao wenyewe ndiyo watatoa maelekezo ya namna ya kurekebisha hiyo kasoro kama itakuwepo. Lakini ni kweli nimepata malalamiko hayo na mimi tayari nimeshawaagiza ili waweze kupata suluhu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi sasa nchi yetu au Taifa letu linakabiliwa na tatizo la njaa katika Mikoa mingi na Serikali imekuwa ikitoa matamko kwamba itapeleka chakula katika maeneo husika ambayo yana tatizo hilo. Napenda kufahamu ni lini sasa azma hiyo itatekelezwa na Serikali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Gekul kwamba yapo maeneo kadhaa hapa nchini ambayo yanakabiliwa na ukame, mengine kwa muda mrefu na kwa hiyo kumekuwa na tatizo la kutokupata chakula cha kutosha. Ni kweli vile vile kwamba, Serikali tumekuwa miaka yote tunajitahidi kuhakikisha maeneo haya yanapata chakula. Kwa hiyo hata hivi sasa tunavyozungumza Wilaya hizo ambazo zinakabiliwa na matatizo haya tunaendelea kupeleka chakula.

Sasa usitikise kichwa, mimi si ndiyo nasemea eneo hili bwana. Ndiyo maana nasema kama kuna eneo mahususi pengine kwenye Wilaya yako ambako hatujafika, basi naomba tu niarifu ili tuone kama ni kati ya vijiji tulivyonavyo au ni maeneo ambayo yameibuka baadaye hayajaingia kwenye tathmini yetu ili na yenyewe tuweze kuyazingatia.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na tatizo la njaa lakini hivi sasa wananchi wengi asilimia 80 ambao ni wakulima Watanzania wanaelekea katika msimu wa kilimo. Pia msimu wa kupeleka wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tano umekaribia kuwapeleka shule na kuwalipia ada. Lakini sasa mfano katika Wilaya ya Babati, kuna michango imeibuka ya kuchangia sekondari, zahanati na vituo vya afya katika msimu huu mgumu wa kupeleka wanafunzi shule na wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu ni kwa nini Serikali na mfumo wake wote au utendaje wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati hawazingatii msimu huu ambao wananchi wanatakiwa wajiandae katika matatizo au mambo yanayowakabili, wanaanzisha michango ambayo si kwa msimu huu.

**SPIKA:** Jamani swali la kwanza lilikuwa zuri, la pili baya. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama unapenda unaweza kujibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza lilikuwa ni zuri kama unavyosema, sasa unapohama unakuja kwenye michango taabu kweli. Lakini unajua mambo mengine haya Waheshimiwa Wabunge mko kwenye nafasi nzuri zaidi kwenye Halmashauri zenyewe kuweza kushauri. Kwa sababu sisi ni sehemu ya Baraza la Madiwani na mambo haya yapo kwenye Halmashauri kwa mazingira ambayo yanategemea ni eneo lipi.

Njia rahisi ni wewe Mheshimiwa Gekul kushirikiana na Halmashauri yako, kushauri kupitia Madiwani kwamba, pengine katika msimu huu wa sasa jambo hili lingeachwa kidogo tuje tulifanye baadaye kwa sababu ni vitu viko katika vieneo vidogo vidogo *multi scattered* kwa nchi nzima. Kwa hiyo, si rahisi sana wakati mwingine kwa Waziri Mkuu kuweza kuelekeza jambo kutokana na eneo moja. Kwa hiyo, naomba nikushauri hivyo pengine linaweza kupata ufumbuzi wa haraka zaidi.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa panapotokea uvunjifu wa haki za binadamu iwe Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar inayojulikana duniani ni Tanzania. Kwa kuwa Tanzania ilipata sifa kubwa sana Kimataifa kutokana na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar iliyoondosha uhasama wa muda mrefu na kwa kuwa inaonekana kwamba ziko dalili za kudhoofisha au kuvunja Serikali ya Umoja wa Kitaifa huko Zanzibar kutokana na malumbano na uvunjifu wa haki za binadamu. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itachukua hatua gani za makusudi kunusuru hali hiyo?

**SPIKA:** Jamani mbona maswali ya leo yamekaa vibaya vibaya. Sasa makubaliano yalikuwa ya watu wawili kule Zanzibar tena huyu anaingiaje? Leo maswali yenu yamekuwa hovyo. Jaribu Waziri Mkuu kujibu lakini msije mkamlaumu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Zanzibar wa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa ukiniuliza mimi nasema ulikuwa ni uamuzi wa busara na kwa kweli umesaidia sana kuimarisha hali ya mivutano na hali iliyokuwepo kabla ambayo wengi tulikuwa tunaogopa hatukujua tutaishia wapi. Kwa kweli naamini kilikuwa ni kitendo kizuri sana.

Sasa umeingiza jambo ambalo lazima nikiri sina maelezo sana. Unazungumzia juu ya uvunjifu wa amani kwa ujumla Zanzibar. Sasa sina hakika uvunjifu wa amani ni ule Uamusho, uvunjifu wa amani ni nini? Maana lazima nijaribu kutafuta namna ya Umoja wa Kitaifa kama nguzo mliyoikubali na matukio ya uvunjifu wa amani ambayo wewe yanakupa hofu kwamba nguzo hiyo sasa itatetereka. Sasa kwa sababu hunipi picha ni nini ndiyo maana nashindwa kusema, sasa sijui nisaidie. Kwa sababu kama ni mambo ya Uamusho ni uhalifu unatokea ndani ya kikundi, Serikali itashughulika na uhalifu ili kuhakikisha Watanzania wanalindwa na amani inakuwepo. (*Makofi*)

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu je, wewe binafsi uko tayari kumshauri haraka iwezekanavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nyote wawili kwa pamoja mkutane na Rais na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kutatua suala hilo?

**WAZIRI MKUU:** Bado na mimi nitauliza, suala hilo lipi? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** La malumbano linaloingia Zanzibar. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ni Mtanzania na wanaolumbana ni Watanzania una haki ya kuliingilia.

**WAZIRI MKUU:** Maana nitazidi kuuliza, malumbano kati ya nani na nani? Labda nifupishe niseme basi ni vizuri kaka yangu. Hebu basi na mimi ngoja nikapate maelezo zaidi pengine nitapata picha ya jambo lenyewe unalotaka tuliangalie. Kwa sababu Zanzibar kuna uongozi kamili tena uongozi uliochaguliwa, uongozi wenye busara sana. Sasa sijaona kama tumefika

mahali sasa ambapo lazima Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri na Waziri Mkuu sasa twende Zanzibar kuulizia wakubwa huku kwa lipi hasa ambalo limetusibu? (*Makofi*)

Kwa hiyo nadhani kwa sasa kama lipo hebu acha wazee wale wenyewe wakae wazungumze, waone ni suluhu gani wataipata. Lakini kwa upande mwingine umenipa somo acha na mimi nifuatilie nione ni lipi hasa tatizo ambalo unajaribu kulizungumza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Bahati mbaya wamebakia watu wachache, lakini wengine wame-*cover*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kama tunavyosema Kanuni zetu zimeandikwa waziwazi, tuulize maswali ya kisera na maeneo pia ni muhimu. Tusiulize habari ya kijiji cha mtu, Waziri Mkuu hawezi kujibu hapa maana havijui hivyo vijiji. Tunaendelea na hatua inayofuata, Katibu!

## MASWALI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Maswali ya Kawaida, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu na atakayeulizwa swali hilo la kwanza ni Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 96

### Bendera Kushushwa Nusu Mlingoti

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Bendera ya Taifa hushushwa nusu mlingoti mara vinapotokea baadhi ya vifo au matukio maalum:-

(a) Je, vifo vya watu wangapi hupelekea Bendera ya Taifa kushushwa nusu mlingoti?

(b) Je, ni vifo au matukio ya aina gani husababisha Bendera ya Taifa kushushwa nusu mlingoti?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna idadi kamili ya vifo vya watu iliyowekwa ambayo itapelekea Bendera ya Taifa kushushwa nusu mlingoti.

(b) Bendera hushushwa nusu mlingoti iwapo kumetokea matukio ya vifo vya viongozi wa Kitaifa waliopo madarakani au viongozi wa Kitaifa wastaafu. Pia Mheshimiwa Rais anaweza kutoa Tamko la Bendera kushushwa nusu mlingoti iwapo kutatokea maafa au janga kubwa litakaloitikisa nchi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna ubora wa kifo au hata roho isiyo na thamani kwa nini usiwekwe utaratibu maalum unaoeleweka ili matukio yanayohusisha kushusha nusu mlingoti hususani idadi ya watu wanaokufa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza, Mheshimiwa Rais hutangaza maombolezo na kuelekeza bendera ya Taifa kupepea

nusu mlingoti kwa idadi ya siku zitakazoonekana zinafaa kukidhi azma yenyewe. Lakini pili, iko Sheria kwa mujibu wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa namba moja ya mwaka 2006, matukio ya vifo vya viongozi wa Kitaifa ambavyo hupelekea bendera kushushwa na kupepea nusu mlingoti ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna aina ya watu ambao wamewekewa siku:-

(i) Rais aliyepo madarakani maombolezo ni siku 21;

(ii) Rais Mstaafu siku saba;

(iii) Makamu wa Rais aliyepo Madarakani siku 14;

(iv) Makamu wa Rais Mstaafu siku saba;

(v) Waziri Mkuu aliyepo madarakani siku saba; na

(vi) Waziri Mkuu Mstaafu siku tano.

Mheshimiwa Spika, kwa viwango vya siku kwa viongozi hawa, kuna Sheria nyingine ambayo imeshaweka viwango, hii nimeisoma lakini hii unayoisema Mheshimiwa Yahya kwa kweli ni changamoto ambayo sisi Wabunge lazima tutafakari na sisi kama Serikali tumeona hiyo changamoto ambayo kwa kweli nakubali wazo lako kuwa ni muhimu kuliangalia kwa kina.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere!

**Na. 97**

**Hospitali ya Wilaya ya Kwimba Kupatiwa Vifaa vya Macho**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Kwimba ina Daktari wa macho bila kuwa na vifaa vinavyotakiwa ili kutoa huduma hiyi:-

Je, Serikali itapeleka lini vifaa hivyo kama vile *oththalmic operating microscopes, slit lumps, cataract set na indirect ophthamoscopes* ili wananchi wapate huduma stahili?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri Mkuu, inaomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kwimba ina daktari mmoja tu ambaye anatibu macho. Halmashauri katika Wilaya ya Kwimba katika mwaka 2010, iliamua kumwendeleza mtaalam huyo kwenye fani ya magonjwa ya macho katika Chuo cha Udaktari *KCMC*. Uamuzi huo ulitokana na mahitaji makubwa ya mtaalam wa macho katika hospitali ya Wilaya ya Kwimba. Hivi sasa Daktari huyo yupo, anatoa huduma za magonjwa ya macho katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto ya ukosefu wa vifaa vya matibabu ya macho hospitalini hapo, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba katika mwaka wa fedha 2012/2013, imeweka kipaumbele na kutenga shilingi milioni 40 ambazo zitatumika kununulia vifaa vya matibabu ya macho pamoja na ununuzi wa dawa katika Hospitali hiyo. Jitihada hizi zitapunguza adha ya ukosefu wa vifaa na matibabu ya macho ambayo imedumu kwa muda mrefu hospitalini hapo.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kutenga fedha ni jambo moja na kwa kuwa kununua vifaa na kuvikabidhi ni jambo lingine, naomba Serikali leo itoe tamko ni lini itakabidhi vifaa hivyo katika Hospitali ya Ngudu ili na mimi niweze kushuhudia hilo tukio?

Swali la pili, kwa kuwa kupeleka Daktari katika hospitali ambayo haina vifaa ni sawa na kuvaa shati bila suruali *(Kicheko).*

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali yetu itaachana na mtindo huu ambao hauleti tija katika Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge anaonekana kuwa na wasiwasi nalo tamko ambalo tumetoa hapa ni kwamba, tumetenga shilingi milioni 40, najua wasiwasi alionao ni kwamba hii itatekelezwa? Sisi tutasimamia jambo hili kuona kuwa vinanunuliwa, tumeuliza wastani wa fedha zinazohitajika kwa ajili ya vifaa tukawaambia ni kati ya milioni 15 na milioni 30 na hapa tumeweka milioni 40 ambazo ziko katika bajeti ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nataka kumthibitishia Mbunge kuwa sisi tutafuatilia jambo hili kuhakikisha kuwa vifaa hivi ambavyo mmevitaja hapa ambavyo ni vigumu kutamka kwani vinaonekana ni vya kitaalam sana ulivyoandika hapa.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ambalo limetuchekesha sisi wote, lakini kama unavaa shati bila suruali itakuwa ni matatizo makubwa sana. Lakini anachotaka kusema hapa na ambacho kipo huwezi kubisha hapa kwani watasimama Wabunge wengi, hili la kwamba hatuna vifaa vya kutosha katika maabara zetu, katika Hospitali zetu na katika Zahanati zetu ni jambo ambalo mnasikia hata Waziri wa Afya analizungumza hapa na sisi wote tunakiri kuwa tuna upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, hapa katikati tumepitisha maamuzi kwamba, tuanzishe Zahanati katika kila Kijiji tukasema pia tuanzishe Kituo cha Afya katika kila Kata, moja ya changamoto ambazo tutakutana nazo ni hilo la vifaa ambalo Mheshimiwa Leticia anazungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine anachosema ni kwamba, kama wamepeleka Daktari kutoka *KCMC* akaenda pale hana vifaa ni *irrelevant,* ni kweli unachosema na ni kweli kama hakuna vifaa pale, sasa *wheather* ni suala la shati, suruali na nini mimi sijui, lakini ni kweli kuwa tumepeleka pale. Tunachotaka kuthibitisha ni kwamba, ziko jitihada za waziwazi za kuhakikisha tunakuwa na vifaa katika maeneo hayo ili kazi iweze kufanyika kama ilivyokusudiwa.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru umenipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Daktari na Watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Kwimba kwa kufanya kazi kwenye mazingira magumu, lakini pia wanatoa huduma nzuri sana kwa wananchi wa Kwimba.

La pili, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa vifaa ilivyokwishapeleka kwa Wilaya ya Kwimba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tambwe naomba urudi uliko toka, naomba urudi ulikotoka.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo ya macho kuna matatizo ya *transfomer* ya kupoza umeme ni ndogo sana na mara kwa mara inaharibika katika Hospitali ya Wilaya ya Kwimba. Tatizo hilo linafanya mochwari ya Hospitali ya Wilaya ya Kwimba haifanyi kazi, naomba kujua ni lini Serikali itatuletea *transfomer* kubwa ambayo itatekeleza matumizi ya Hospitali ya Kwimba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hiran, huoni kuwa ni swali jipya kabisa hilo, hili lilikuwa ni Ngudu tena umeshaingia Kwimba.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, ni Hospitali hiyo hiyo.

**SPIKA:** Ni Hospitali hiyo hiyo! Basi Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza tunamshukuru kwa pongezi Mheshimiwa Mansoor, lakini hapa napata shida kwa sababu anazungumzia *transfomer* na *transfomer* ni *issue* inayohusu *TANESCO*, zingekuwa jenereta, ningejua hilo lingekuwa la kwetu, nikuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nitawasiliana na *TANESCO* ili tuone hiyo *transfomer* kwa sababu sisi Halmashauri huwa hatusimamii *transformer,* lakini ni wadau muhimu kwa maana ya kuwa tunazitumia. Kwa hiyo, nitafuatilia jambo hilo kwa maana ya kushirikiana na wake wenzetu wa *TANESCO*.

Na. 98

**Ujenzi wa Majumba ya Starehe Kwenye Makazi**

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI** aliuliza:-

Hivi sasa kumezuka ujenzi wa majumba ya starehe, uuzaji wa vinywaji vikali na makasino katika maeneo ya makazi ya watu bila kuhusisha wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, mambo haya yanapata vibali vya Serikali?

(b) Je, wananchi wa maeneo jirani wanakingwa vipi na madhara yatokanayo na kelele za muziki na magari?

(c) Je, wananchi wa maeneo jirani wanayo haki ya kuzishtaki Manispaa na Halmashauri husika zinazoruhusu mambo hayo?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kanuni za ujenzi mijini za mwaka za mwaka 2008 Kifungu cha 124 (1) kinasema kuwa, hakuna mtu atakayeweza kujenga au atakayejenga mjini bila kibali kutoka kwenye Mamlaka husika inayohusika kwa madhumuni ya rejea rahisi hapa ninanukuu.

124 (1) "*No person shall erect or begin any building until he has:-*

*(a) Made an application to the Authirity up the form prescribed to be obtained from the Authority;*

*(b) Furnished the Authority with drawings and other documents specified in the following regulations and;*

*(c) Obtained from the Authority a written permit to be called a building permit to erect the building.*

(a) Mheshimiwa Spika, Aidha kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Mipango Miji cha mwaka 2007, kinazuia uendelezaji wowote katika eneo la mpango bila kupata kibali.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kukinga wananchi na madhara yatokanayo na kelele za muziki na magari waendelezaji wa majengo hayo wanatakiwa kuweka vidhibiti sauti *(sound proof).*

(c) Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaeleza Usawa wa Binadamu na Usawa mbele ya Sheria. Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1)(b) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na kifungu cha 14(1)(b) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288, Halmashauri ya Wilaya au Halmashauri ya Miji, Manispaa au Jiji zinaweza kushtaki au kushtakiwa. Hivyo, iwapo kutakuwa na ushahidi wa kutosha dhidi ya Mamlaka hizo, wananchi wanaweza kufungua kesi dhidi ya Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza kuwa ni muhimu kuzingatiwa kwa Sheria zote kote nchini. Katika kupambana na ujenzi holela mijini na nje ya miji ni vyema Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zikahakikisha kuwa kila aina ya ujenzi katika maeneo unazingatia Sheria kwa kuomba kibali cha ujenzi na kisha kufuatilia utekelezaji huo katika hatua zote.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza; kwa kuwa, suala langu lilikuwa *specific,* ni suala la ujenzi wa majumba ya starehe katika makazi ya watu, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuniambia kuwa hili lina baraka ya Serikali katika taratibu zao?

Pili, Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu la (b) ameniambia kuwa wajenzi wanatakiwa waweke vidhibiti sauti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuniambia kuwa ana uhakika masuala hayo wanaambiwa, wanafahamu na wanatekeleza? Wao wanajua vipi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kabisa kuwa, Mheshimiwa Daftari amekuwa *specific,* sasa najaribu kuangalia kuwa Mheshimiwa Maua Daftari akiuliza swali ningekuwa nikijua ni Kinondoni, Ilala au wapi, lakini kwa upande wa nchi yetu, najua kuwa anauliza kwa manufaa ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, unapotoa kibali, mtu amepewa kiwanja anapokwenda kujenga pale anapojenga kwa maana ya kuwa amepewa kiwanja, hataweza kujenga katika kiwanja kile pamoja na kuwa anazo *documents* zote mpaka apate kitu kinachoitwa *building permit,* ili kama anakwenda kujenga Msikiti Mamlaka ijue kuwa huyu anakwenda kujenga Msikiti ili kama anakwenda kujenga Kanisa Mamlaka ijue kuwa huyu anakwenda kujenga Kanisa, ili ijulikane kuwa huyu anakwenda kujenga hiki au kama ni ukumbi wa starehe ijulikane.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu anavyosema Mheshimiwa Maua Daftari ni kwamba, kama ni mahali ambapo unasema hapa ni *residential area,* huwezi kupeleka jumba la starehe kule na kuanza ngungungu, magoma yanapigwa pale, *no!* Kwa hiyo Mamlaka hiyo itakapojua kuwa huyu anakwenda kuleta kero kwa wananchi haitatoa hicho kibali.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea ni kwamba, mtu atafanya hivyo, atasema mimi najenga hivi, baadaye anabadilisha matumizi ya ule ujenzi uliofanyika pale na yale majengo yaliyofanyika pale na ndiyo maana tukasema kama wapo Wabunge wanaojua kuwa kuna mtu amejenga katika eneo ambalo halistahili tuambiane hapa. Mtuambie, mtupatie majina sisi twende sasa hivi, tushuke nao jumlajumla!

Mheshimiwa Spika, haiwezekani unakwenda kupiga muziki pale ngu ngu ngu ngu, watu wanaimba pale, inakuwa ni vurugu usiku kucha, *no way!* Kwa hiyo, tunachokisema hapa ni kuwa kama imetokea hivyo ni makosa, *building permit* itasema kwamba hapa ni kiosk, ni kiosk, hapa ni shule ya msingi, ni shule ya msingi.

Mheshimiwa Spika, la pili, vidhibiti sauti hivi tunavifahamu kuwa ni moja ya masharti, kwa mfano, imetokea sasa kwamba umejenga umepewa kibali na wanaofanya kazi hiyo wala siyo Halmashauri, ni Baraza la Sanaa la Taifa ndilo ambalo wanasimamia jambo hili na ndiyo wanaangalia mambo ya *quality control,* mambo ya *policy issues* na mambo mengine wako humu ndani wanaohusika. Wale ni lazima waseme sasa tunakubali kuwa unaweza ukafanya jambo hili. Hata Dodoma kuna mahali wanaweza kufanya sherehe za harusi, wala huwezi kujua kuwa kuna sherehe za harusi zinafanyika pale.

Mheshimiwa Spika, nikiri hapa kwamba, wakati mwingine unakuta tatizo ni yule aliyepewa ruhusa ya kujenga jumba la starehe, wananchi wamekwenda wakamfuata pale, wamekwenda pale kwa kufuata utaratibu au vyovyote vile itakavyokuwa tunaomba mtuambie Wabunge kama kuna watu wamejenga hovyo, au vibali vimepitapita tu hivi, tupatieni majina yao ndiyo kazi yetu sisi, twende tukashughulike nao kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nasema kama mtu amekwenda kuingiza jengo mahali ambapo sipo, sisi tutachukua hatua wala tusingoje kwenda, tupatieni majina.

**SPIKA:** Jamani swali lilikuwa refu na majibu yake ni hayo. Sasa tuendelee na Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Amina Mwidau atauliza swali hilo.

Na. 99

**Kuporomoka kwa Maadili ya Kitanzania, Uadilifu na Uzalendo**

**MHE. AMINA M. MWIDAU** aliuliza:-

Siku za hivi karibuni tumeshuhudia hali ya kuporomoka kwa maadili ya Kitanzania na upungufu wa Uadilifu na Uzalendo miongoni mwa Watanzania vilivyojionesha kwenye migomo mbalimbali ya elimu ya juu na katika taasisi za Serikali, vitendo vya rushwa, kutopenda kuwajibika katika taasisi za Umma na binafsi:-

(a) Je, Wizara imeshafanya utafiti kubaini kutokea kwa hali hizo?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kufuatia vitendo na hali hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y.WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zipo sababu kadhaa ambazo zinasababisha kuporomoka kwa maadili ya Kitanzania na upungufu wa Uadilifu na Uzalendo miongoni mwa Watanzania. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2009 kuhusu utawala wa rushwa *(Governance and security Survey),* baadhi ya sababu hizo ni pamoja na matumizi ya teknolojia ya utandawazi yanayoifanya jamii kuiga matendo wanayoyaona kupitia televisheni na mitandao ya kijamii na tamaa ya kimaisha ambapo baadhi ya vijana hutaka kuishi maisha ya kifahari bila kuzingatia uwezo walionao.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni kukosekana kwa mfumo unaojenga tabia ya uzalendo kwa jamii hususan kwa vijana kama ilivyokuwa awali ambapo kulikuwa na kambi za Umoja wa Vijana na Jeshi la Kujenga Taifa na kutopenda kufuata Sheria, taratibu na kanuni katika kuyapatia ufumbuzi matatizo au migogoro inapotokea.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la kuporomoka kwa maadili ya Kitanzania na upungufu wa uadilifu na uzalendo miongoni mwa Watanzania, Serikali inawataka Watanzania hususan vijana kuwa wazalendo, watiifu na waadilifu. Aidha, Serikali itaendelea kufundisha elimu ya Uraia katika shule za Sekondari na Msingi, kutoa mafunzo ya Mgambo na Jeshi la Kujenga Taifa ili kuwajengea misingi bora ya kiuzalendo, uadilifu na maadili mema.

Mheshimiwa Spika, pia Viongozi wa Taasisi mbalimbali zikiwemo za Kidini wanatakiwa kufanya vikao vya mara kwa mara kuhimiza na kujadili Watanzania hususan vijana kuwa wazalendo, watiifu na waadilifu kwa Taifa lao.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Waziri amesema Serikali itaendelea kufundisha elimu ya uraia katika shule za msingi na sekondari, kutoa mafunzo ya mgambo na JKT ili kuwajengea misingi bora ya kiuzalendo, uadilifu na maadili mema; na kwa kuwa, katika Bunge lililopita la bajeti ilipitishwa kurudi JKT kwa hiari na bajeti ikapangwa na inatarajiwa kuanza Februari, 2013. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kurudisha ile JKT ya zamani ambapo wanaomaliza kidato cha sita, wanaotoka vyuoni, vyuo vya ufundi, Diploma ni lazima kwenda JKT hata viongozi ili kuweza kuendeleza maadili yao?

Pili, katika utafiti nilioufanya ambao sio rasmi mbali ya utandawazi nimegundua kuwa asilimia ya Watanzania takribani sitini ni vijana na asilimia kubwa ya vijana hao hawana ajira kiasi cha kupelekea kukata tamaa na Serikali iliyopo Madarakani kwa kiasi kikubwa na kwa kuwa, Serikali katika mpango mkakati wake mmojawapo ilikuwa ni kujenga Vyuo vya Ufundi *VETA* katika kila Wilaya:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuharakisha mpango wa ujenzi wa Vyuo hivyo kwa mbio za marathoni ili vijana hao wengi wanaohangaika waweze kupata mafunzo?

**SPIKA:** Haya ni *VETA* na JKT tu, naomba ujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la JKT kuanzia mwaka 2001, Vijana wengi sana wamejiunga na JKT na mpaka sasa hivi, karibu vijana 42,400 wamehitimu mafunzo ya JKT. Kwa hiyo, hilo tunalitekeleza. Halafu kuna Kambi Nane za JKT zimeshaanzishwa na kama Waziri wa Ulinzi alivyowasilisha kwenye bajeti yake kwamba, mafunzo ya JKT yataanza katika mwaka wa fedha 2012/2013 na tumeshaanza maandalizi yamefikia mahali pazuri na bajeti imetengwa kwa ajili ya mafunzo ya JKT. Kwa hiyo, hilo tunalitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa Vijana, sisi kama Serikali mikakati iko mingi. Tunafahamu kabisa kwamba, ajira kwa vijana ni chache, lakini Serikali imechukua tahadhari mbalimbali na hatua mbalimbali kuhusu mambo ya kilimo kwanza, pia tumewajengea mazingira vijana ili waweze kujiajiri wenyewe na sasa hivi katika mitaala ya elimu pia tunatoa elimu ya ujasiriamali kwa baadhi ya mitaala ili vijana wanapotoka katika Vyuo mbalimbali waweze kujitegemea. Tusitegemee ajira tu za kuajiriwa ofisini bali hata ajira hizo za kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Ufundi, sasa hivi Wizara ya Elimu inajitahidi sana kujenga Vyuo vya Ufundi katika sehemu mbalimbali, kama ulikuwa umeisikiliza vizuri bajeti ya Wizara ya Elimu walitaja vyuo mbalimbali vya Ufundi ambavyo vitaanzishwa, na umeona kule Lindi kwa mfano, wameshafungua Chuo cha Ufundi kikubwa sana. Kwa hiyo, tutaendelea awamu kwa awamu kuhakikisha kwamba tunajenga Vyuo vya Ufundi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kuniona, mwuliza swali la msingi aliuliza kuhusiana na kuendelea kwa vitendo vya rushwa na majibu ya Waziri yanaeleza kwamba mkakati mmojawapo wa kuhusisha uzalendo dhidi ya ufisadi ni kurejesha JKT. Lakini kwa kuwa, katika orodha mbalimbali za watuhumiwa wa ufisadi katika nchi yetu wapo viongozi na watendaji ambao walipitia Jeshi la Kujenga Taifa hali ambayo inaashiria kwamba kuwepo kwa JKT siyo ufumbuzi peke yake wa ufisadi kwa kuwa sehemu kubwa ni kwa sababu ya kutokusimamia utawala wa sheria:-

Je, Serikali sasa iko tayari kutekeleza kwa dhati mikakati ya kuwachukulia hatua mafisadi wote kwa kadri ya utawala wa sheria ili kujenga funzo na nidhamu kwa vijana wasijiingize kwenye ufisadi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika angesoma lile swali *between the lines*, kwa sababu lile swali linauliza kuhusu kuporomoka kwa maadili, uadilifu, uzalendo, migomo, rushwa na kuwajibika, kwa hiyo lilikuwa ni pana sana na nimemjibu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama unataka hilo la rushwa ni swali *specific* na mimi nakujibu kama ifuatavyo:-

Masuala ya rushwa yako Mahakamani, tuziachie Mahakama zifanye kazi zake, masuala ya ufisadi tuziachie Mahakama zifanye kazi zake. Sisi Wabunge hatuwezi tukaamuru kuwafunga watu, hatuwezi tukawa Mahakimu, tukawa watunga sheria na sisi hao hao tukawa watekelezaji wa sheria. Kwa hiyo, tuheshimu hiyo mihimili ya dola. (*Makofi*)

Na. 100

**Uchakavu wa Nyumba za Askari**
**Magereza Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE)** aliuliza:-

Nyumba za Askari katika Gereza la Isanga zimechakaa na kubomoka, hali inayosababisha Askari na familia zao kuishi chumba kimoja kinyume na maadili ya maisha ya Kiafrika:-

Je, Serikali itakarabati lini au kujenga nyumba mpya za Askari hao wanaofanya kazi katika mazingira magumu ndani ya Gereza hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mciwa Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza kupitia Bajeti yake inayoidhinishwa na Bunge hili limeendelea kutumia bajeti hiyo kuboresha nyumba za Askari kwa kuzifanyia ukarabati, kujenga nyumba mpya na kukamilisha zile ambazo ujenzi wake haujakamilika. Pamoja na ufinyu wa bajeti, zoezi hili linatekelezwa kwa awamu. Nia ya Serikali ni kuendelea kuboresha makazi ya Askari kwenye Magereza yote nchini ikiwemo Gerezani Isanga kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mwaka huu wa fedha zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Gereza la Isanga, kukalimika kwa ukarabati wa majengo ya Gereza hilo kutatoa nafasi ya kuweka nguvu kwenye ujenzi wa nyumba za Askari pamoja na ukarabati wa nyumba za Askari zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linaendelea pamoja na hayo, kufuatilia utaratibu wa kupata mikopo toka Taasisi za Kifedha kama vile *NSSF, PSPF* na *PPF* kupata fedha za ujenzi ili zitumike kujenga nyumba mpya kwenye Magereza ambayo yana ukosefu mkubwa wa makazi likiwemo Gereza la Isanga.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, Askari Magereza ni watu wanaoshughulika na wahalifu na wahalifu ambao wamefungwa na kwa kuwa kukaa kwenye nyumba mbovu ni kuhatarisha maisha ya Askari hao pamoja na familia zao kwa sababu wanakaa pamoja na wafungwa waliopo Gereza la Isanga ambao wengi wao ni waliohukumiwa kunyongwa; Je, ni lini Serikali itawaonea huruma wale Askari na kuweka mkakati wa karibu sana kuhakikisha kwamba nyumba zile zinakarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina utaratibu mzuri sana wa kujenga nyumba kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa mfano, nyumba za Kilwa *Road* ambazo zimejengwa kwa ushirikiano na Shirika la *NSSF*, Je Serikali ina utaratibu gani hasa ukizingatia Mkoa wa Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali, kuhakikisha kwamba nyumba za Askari wa Mkoa wa Dodoma zinawekewa utaratibu maalum?

**SPIKA:** Waziri naomba ujibu kwa kifupi maana maswali yenyewe yanazunguka tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anauliza ni lini Serikali itawaonea huruma Askari Magereza wa Isanga. Kwenye hili nafikiri Serikali tayari inawaonea huruma sana na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba, kwenye Gereza lenyewe kulikuwa na ukarabati ambao ulikuwa wa lazima na *priority* kwa nchi hii kwa sababu hasa ulikuwa unahusiana na miundumbinu na kuondosha mtondoo. Mara tu baada ya hili kuna mpango madhubuti wa kujenga nyumba za Magereza nchi nzima kupitia mpango wa maboresho.

Mheshimiwa Spika, jibu la swali la pili ni kwamba, hivi sasa Jeshi la Magereza liko kwenye mazungumzo na Mifuko ya Jamii.

**SPIKA:** Tunaomba utulivu, wengine nafikiri wapo nje, nitawataja baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hivi sasa Jeshi la Magereza linaendelea na mazungumzo na Mifuko ya Jamii ili kuweza kupata *resources* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Magereza nchi nzima. Tusubiri hili likikamilika litajumuisha pia mpango mahsusi wa Dodoma na Isanga.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. Magereza mengi sana hapa nchini wafungwa wana miradi mbalimbali wanayoifanya ambayo inawaingizia fedha kama vile kilimo, ufugaji na kadhalika. Kwa nini fedha za miradi hii zisitumike kutatua sehemu ya tatizo hili ambalo ni kubwa sana, Askari wanaishi kwenye mabanzi wafungwa wenyewe wanaishi katika hali ya taabu, fedha hizi kwa nini zisitumike na zinakwenda wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hali ya nyumba za Magereza kote nchini ni mbaya na hivi tunavyoziona ni pamoja na kutumia baadhi ya fedha ambazo Magereza yenyewe inakusanya kwenye baadhi ya miradi yao.

Chini ya Magereza kuna mpango unaitwa *Self-help* ambapo kila Gereza limepewa agizo la kuhakikisha kwamba kwa kutumia *resources* ambazo zipo karibu zinajenga au zinakarabati nyumba zilizopo. Hivi sasa hili limesaidia sana. Tuna nyumba ambazo zimeshajengwa kwa mpango huu ambazo Wizara na Makao Makuu zinategemea kuzimaliza baada ya wenyewe. Kwa hiyo, pamoja na hali tuliyonayo ni pamoja na kutumia *resources* ambazo baadhi zinakusanywa ndani ya Magereza.

Na. 101

**Mahitaji ya Umeme ya Vijiji na Ukamilishaji**
**mradi wa Umeme- Vwawa-Hasamba**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza**:-**

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Nanyala, Senjele, Ivwanga na Mbimba ambavyo vimepitiwa na umeme wa msongo mkubwa wa umeme?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa umeme wa Vwawa-Kamsamba kilomita 13.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* iko katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kujenga miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo yote yaliyopitiwa na njia na upelekeaji wa umeme ili kufikia wananchi wengi zaidi. Mradi huo utahusisha vijiji vya Nanyala, Senjele, Ivwanga na Mbimba. Mradi huu utatekelezwa kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini mara taratibu za manunuzi zitakapokamilika.

(b) *TANESCO* iko katika hatua za awali za maandalizi ya utekelezaji wa mradi kabambe wa awamu ya pili ambapo mradi wa kupeleka Hasamba kutoka Vwawa umejumuishwa na unatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake lakini ni maswali mawili yafuatayo. Ahadi ya Serikali kupeleka umeme katika Vijiji vya Nanyala, Senjele, Ivwanga na Mbimba ni ya tangu mwaka 2008/2009 na nakumbuka Serikali ilishaweka hata bajeti kwa ajili ya transfoma kwa ajili ya vijiji hivyo. Leo mwaka 2012/2013 Serikali bado inakuja na majibu hayo hayo, naomba Serikali inipe majibu thabiti ambayo yatawafanya wananchi wa maeneo haya waone kwamba Serikali inawaambia kitu ambacho ni cha kweli.

Swali la pili, suala la kupeleka umeme katika Kijiji cha Hasamba kilomita 13 kutoka Vwawa Mjini lilianza mwaka 2003/2004 na nguzo zilishawekwa, mpaka leo hakuna kinachoendelea na leo ni nusu mwaka Waziri anasema Serikali itapeleka umeme mwaka 2012/2013, bado miezi sita mwaka kumalizika, Naomba majibu madhubuti ya Serikali ili wana Hasamba waelewe kwamba kweli Serikali inawapelekea umeme katika kipindi cha mwaka huu kwa maana ya miezi sita iliyobaki.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, katika vijiji ambavyo nimevitaja kwenye jibu langu la msingi vya Nanyala, Senjele na Mbimba, kama nilivyosema ni mchakato tu wa manunuzi unaendelea. Nikisema mchakato wa manunuzi unaeleweka, unaanzia wapi na unaishia wapi. Napenda nimhakikishie Mbunge kwamba tutaweza kutekeleza mradi huu katika kipindi cha mwaka wa fedha huu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni Kijiji cha Hasamba ambacho anadai Mbunge kwamba nguzo zilishawekwa. Nataka nikuhakikishie kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba na wenyewe huu kwa kuwa hata nguzo zilishawekwa, kazi iliyobakia siyo kubwa sana na pale kunahitajika transfoma tu, tutajitahidi kwa kadri tunavyoweza tuweze kufanya mapema kadri iwezekanavyo ili wananchi wa Hasamba waache kukata tamaa na kukulamikia Mbunge kama ambavyo tumekuwa tukizungumza juu ya Hasamba.

Na. 102

**Mpango wa Kupeleka Umeme Kwenye Kivuko Kinachounganisha Tanzania na Uganda**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza**:-**

Mradi wa ujenzi wa kivuko kinachounganisha Tanzania na Uganda katika Tarafa ya Bugaba, Kata ya Rubafu ni kama kilomita 20 kutoka Kibiengwe ambapo kuna umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kivukoni hapo?

(b) Je, wananchi waliopo njiani katika Kata za Buhenda-Ngabo-Kaagya-Kishanje na Rubafu watafaidika vipi na mpango huo wa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini *TANESCO* imefanya tathmini *(Bankable project studies Distribution reinforcement and expansion plan in TANESCO regions)* katika Mikoa 14 ukiwemo Mkoa wa Kagera, ikijumuisha eneo la kivuko husika. Shirika linaendelea kutafuta fedha za kutekeleza miradi hiyo ikiwemo eneo la kivuko.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo yaliyo njiani katika Kata za Buhenda, Ngabo, Kaagya, Kishanje na Rubafu watanufaika kwa kupata huduma ya umeme pindi mradi huu utakapokamilika.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa lakini nina swali la nyongeza. Swali hili linafanana na swali ambalo liliulizwa mwezi wa Saba katika Bunge la Bajeti, swali hilo lilihusu mahsusi hasa Kata Nne, Kata ya Buhenda, Ngabo, Kaagya, Kishanje na Rubafu na majibu yalikuwa kwamba, Serikali ilishatafuta pesa karibu bilioni nne na utafiti ulishafanyika na ulishakamilika.

Mheshimiwa Spika, na kwamba walishafanya tathmini ya kazi hii ya kujenga umeme katika Kata hizi kilomita 50 za njia kubwa na kilomita arobaini na kitu za njia ndogo na kwamba umeme ungepelekwa katika mwaka huu wa fedha. Sasa jibu la leo ambalo linahusu kivuko linaonesha kama tunarudi nyuma, haoni kama ni kuwaonea wananchi katika majibu aliyotoa leo?

Mheshimiwa Spika, naomba jibu la Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rweikiza la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kimsingi bado swali ni lile lile alililoliuliza siku za nyuma na kwamba jibu letu sisi hapa, sana sana limesogea mbele na kugusa kivuko ambapo hata awali ilikuwa ndio sehemu ya mradi wenyewe. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo haya aliyoyataja ya Vijiji hivi kwamba, bado madhumuni ya Serikali ni yale yale na kwamba ni lazima katika mradi ule tuhusishe na kivuko pamoja na maeneo haya yatakayopitiwa na mradi kwa maana ya Vijiji hivi vya Rubafu, Kaagya, Kishanje na maeneo yanayozunguka pale. Hata tunaweza tukaenda zaidi kwa sababu inategemea na upembuzi ambao tumeufanya na kuona kuna manufaa gani mradi huu unaweza kuleta kwa wananchi wa maeneo yale.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu liko karibu kabisa na suala la Kibengwe, ukiangalia kwa mfano, katika umeme unaotoka Mtukula, unatoka Uganda umepita Mtukula ukaenda Bukoba ukarudi mpaka Bunazi, Bunazi pale kwenda Mtukula ni kilomita 10 tu na Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kwamba itatupelekea umeme Mtukula. Ukiangalia Uganda umeme unawaka, Tanzania ni giza. Ni lini Serikali itatimiza hiyo ahadi ili kuondoa giza Tanzania wakati Uganda umeme unawaka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli na bahati nzuri nimewahi kupata bahati ya kwenda Mtukula na nikaona upande wa pili ulivyo na ambavyo fursa kwa upande wa kwetu ni finyu na ni dhahiri kwamba, tulikwisha kuzungumza na mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tunaweka umeme. Sina tu taarifa za sasa kuhusu nini kinaendelea katika mchakato wa taratibu za manunuzi katika mradi mzima wa kupeleka umeme Mtukula kama tutachukulia wapi na tutapeleka wapi, lakini naomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tuwasiliane ili tuone *status* gani ambayo wenzetu wa *REA* na *TANESCO* wamefikia.

Na. 103

**Wahitimu wa Fani ya Udaktari Kwenda Kufanya Kazi Nje ya Nchi**

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE RWAKATARE** aliuliza**:-**

Serikali hutumia fedha nyingi kusomesha Madaktari na Manesi, lakini wanapohitimu masomo yao huenda nchi za nje kama vile Botswana kufuata maslahi mazuri ya kazi na nchi inabaki bila Madaktari wa kutosha:-

Je, kwa nini Serikali isiboreshe maslahi ya Madkatari hao ili kuwavutia wabakie hapa nchini kutoa huduma kwenye hospitali zetu mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inatumia fedha nyingi kusomesha wataalam mbalimbali wa afya wakiwemo Madaktari na Wauguzi. Aidha, ni kweli kwamba katika kipindi cha miaka ya nyuma, baadhi ya wataalam hawa, hususani Madaktari na Wauguzi walikuwa wanaondoka kwenda kufanya kazi nje ya nchi kwa sababu za kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hilo kuanzia mwaka 2005-2012 Serikali ya Awamu ya Nne imefanya utaratibu wa kukabiliana na tatizo la uhaba wa wataalam wa afya nchini kwa kuboresha mishahara kwa kutoa nyongeza ya zaidi ya asilimia 400 ya kiwango walichokuwa wakilipwa awali. Mfano, mshahara wa Daktari mwaka 2005/2006 ulikuwa sh. 267,480/= kwa mwezi, mshahara huo kwa sasa 2012/2013 ni takribani Sh. 1,100,000/= kwa mwezi sawa na ongezeko la 412%.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho mshahara wa Afisa Muuguzi umeongezeka kutoka sh. 120,300/= kwa mwezi mwaka 2006, hadi sh. 781,000/= kwa mwezi mwaka 2012/2013. Ongezeko hilo ni sawa na 600%. Aidha, mshahara wa Tabibu umeongezeka kutoka sh. 70,870/= kwa mwezi hadi kufikia shilingi 535,000/= sawa na ongezeko la asilimia takribani 750%. Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wote wa Serikali wakiwemo Madaktari na Wauguzi kadri uchumi unavyoimarika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imeweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa huduma za jamii zikiwemo huduma za afya na hivyo kuongeza wigo wa upatikanaji wa ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, hivi sasa wimbi la wataalam wetu hususan Madaktari na Wauguzi kukimbilia kufanya kazi nje ya nchi limepungua. Aidha, baadhi ya wataalam wetu waliokuwa nje ya nchi wameanza kurejea nchini.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na pia naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Serikali yetu kwa maboresho ambayo yamefanyika kwa kiwango cha juu na jitihada mbalimbali ambazo bado zinaendelea kutolewa. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwanza, maboresho ya maslahi ya wafanyakazi ni pamoja na vitendea kazi, sasa hivi katika hospitali yetu ya Muhimbili mashine ya *CT Scan* ni mbovu kwa kipindi kirefu na mtu kabla hajaanza kupata matibabu inabidi apate vipimo vya *CT Scan*. Kwa sasa hivi wagonjwa wengi wanaambiwa waende *Regency* au waende Aga Khan ambako pesa zake ni nyingi na wengi

wanashindwa. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kununua *CT Scan machine* nyingine ya pili wakati tunangojea hiyo ya kwanza itengenezwe? (*Makofi*)

Pili, malipo ya kipimo cha *CT Scan* kwenye hizo hospitali inakuwa ni kama 250,000/= wakati Muhimbili ni 170,000/= au 180,000/= hivi. Kwa hivyo, kuna tofauti ya kama 70,000/=. Kwa sababu hao wagonjwa wengi hawana uwezo na bado wanangojea mashine itengenezwe au hii *CT Scan* nyingine inunuliwe, kwa hiyo, wanashindwa na wengi wataweza kufa na ugonjwa kabla hawajapata matibabu. Je, Serikali inaweza kuchangia hizo 70,000/= ambazo wale ambao hawajiwezi kabisa waweze kuongezewa ili wakapate vipimo kutoka hizo hospitali za nje? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kipimo cha *CT Scan* Muhimbili kimeharibika tena, kilitengenezwa, kikafanya kazi kwa muda mfupi, baadaye kimeharibika kwa mara nyingine tena. Lakini Wizara imechukua uamuzi wa makusudi kwamba tulete mashine mpya na utaratibu umeanza, tumeutaka Mfuko wetu wa Bima ya Afya kutoa fedha hizo ili tuweze kupata mashine mpya ya *CT Scan* pale Muhimbili. Lakini pamoja na kuleta mashine hiyo, tutaangalia upya gharama za kipimo hicho kwa nia ya kufanya wananchi waweze kuzimudu kuliko ilivyo kwa hospitali za binafsi. Kwa hiyo, hilo liko mbioni, tunalipa umuhimu na ustahili ili kipimo hicho kiweze kupatikana haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kutoa fedha kwa ajili ya kuwasaidia watu kufanya nje ya Muhimbili kwa sasa, utekelezaji wa jambo hilo utakuwa mgumu sana kwa sababu, kwanza hatuna uhakika wa idadi ya watu wanaohitaji hicho kipimo. Lakini pili kutoa fedha hizo kwa kweli kwa sasa ziko nje ya bajeti, kwa hiyo, haitakuwa rahisi. Cha msingi ni jitihada zetu za kufanya haraka ili tuweze kuleta *CT Scan* ya Serikali itakayotoa huduma kwa gharama nafuu kuliko hospitali za binafsi.

Na. 104

**Huduma za Kibenki- Tarafa ya Ngerengere**

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU (K.n.y. MHE. DKT. LUCY S. NKYA)** aliuliza:-

Wananchi wa Tarafa ya Ngerengere pamoja na Wanajeshi wa Kambi ya Sangasanga na Kizuka wanahitaji huduma za kibenki kwani wanalazimika kufuata huduma hizo Morogoro Mjini au Chalinze:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kuzishawishi Benki kama *NMB* au *CRDB* kufungua matawi yao katika Miji hiyo midogo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z.MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mbunge wa Morogoro Kusini-Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za benki kuwa karibu na maeneo ya wananchi. Hata hivyo, Serikali kwa sasa haijihusishi katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za kibenki kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kifedha nchini unaotekelezwa kiushindani tangu mwaka 1991. Wajibu wa Serikali ni kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili sekta binafsi iweze kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Hivyo basi, Serikali haiingilii moja kwa moja maamuzi ya mabenki, hususan mahali pa kuanzisha huduma zao za fedha.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi waweze kupata huduma za kibenki, ni lazima huduma hizo ziwe za faida kwa pande zote, yaani kwa mabenki na wateja. Hivyo basi, uanzishaji wa huduma za kibenki hutegemea upembuzi yakinifu ambao hufanywa na benki husika ukizingatia miundombinu, fursa na usalama wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali kwa kusaidiana na Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikihamasisha na kusisitiza umuhimu wa mabenki kupeleka huduma za kibenki karibu na wananchi. Aidha, Benki Kuu hutoa ushauri kwa taasisi au wananchi ambao wana mipango ya kuanzisha benki au taasisi za kifedha ili kuhakikisha kuwa taasisi hizi zinaanzishwa kwa kuzingatia sheria na taratibu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo tajwa kuunda taasisi yao ya kifedha itakayowasaidia kupata huduma za kifedha karibu na maeneo yao. Serikali ipo tayari kwa kushirikiana na Benki Kuu kutoa ushauri wa kitaalam wa namna ya kuanzisha benki jamii (*Community banks*) kwa wananchi wa Tarafa ya Ngerengere, Kambi ya Jeshi ya Sangasanga, Kizuka na maeneo mengine mara watakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya huduma za mabenki, Serikali inamshauri Mheshimiwa Dkt. Nkya na Waheshimiwa Wabunge wengine kushirikiana katika kuwahamasisha wananchi kujiunga na kuanzisha benki za kijamii (*community banks*) zinazozingatia mazingira halisi.

**MHE. MWIGULU L.M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli Serikali haiingilii moja kwa moja kwenye shughuli za kibenki, lakini Serikali ni mdau wa shughuli hizi za kibenki kwa mfano, mishahara ya watumishi wake huwa inapitishia kwenye mabenki na kuna maeneo ya kiutawala ambayo Serikali imeyagawa kwa mfano Wilaya mpya na zenyewe hazina huduma za kibenki. Kama Serikali akiwa mdau mkubwa, je haiwezi ikashauri mabenki kama *NMB* ambayo ina mpango wa kupatikana katika kila Wilaya iende hata kwenye Wilaya mpya ikiwemo Wilaya ya Mkalama kule Nduguti ili wananchi waweze kupata huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Serikali ni mdau mkubwa wa masuala ya kifedha nchini na vile vile Wizara yangu inasimamia masuala ya mabenki. Kwa mfano, kwa sehemu mpya, Wilaya mpya zilizoanzishwa tunashauri mabenki yale ambayo yana matawi jirani wajaribu kuweka mtandao wa benki zinazotembea *(mobile banks)* kwenda kuhudumia sehemu hizo hadi pale ambako mipango itakapokamilika ya kujenga mabenki. Lakini bado haiwaondolei mabenki ule umuhimu kwao wa kujenga mabenki kabisa au matawi katika sehemu hizo kama itawaleta tija ama la.

Mheshimiwa Spika, bado nasisitiza kuwa Serikali sasa hivi inasimamia na kuboresha *VICOBA* pamoja na *SACCOS* na mpango huo naamini ndio ambao kwa sasa hivi utatuletea nafuU katika kuhakikisha kuwa huduma za kifedha zinawafikia watu wengi pamoja. Lakini bado naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa Mikoa na Wilaya, kuhakikisha kuwa, wananchi wanahamasishwa kujiunga na *VICOBA* na *SACCOS* ili iwe njia mojawapo ya kuendelea katika kujenga *community banks*.

Na. 105

**Mbolea ya Ruzuku Kutowafikia Wakulima kwa Wakati**

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA** aliuliza:-

Msimu wa kilimo hutofautiana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, hali inayosababisha malalamiko mengi ya wakulima kuchelewa kupelekewa Mbolea ya Ruzuku ambapo huwafikia wakati msimu husika umepita:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kufanya utafiti wa misimu ya kilimo katika nchi yetu ili kupeleka Mbolea ya Ruzuku kwenye eneo husika katika muda muafaka?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwakopeshe wakulima mbolea hiyo ili wawe nayo kwa wakati unaofaa, kisha walipe baada ya kuuza mazao yao hasa ikizingatiwa kuwa, wakulima wengi hawana uwezo wa kununua mbolea hiyo, licha ya Serikali kuwapunguzia gharama?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti wa misimu ya kilimo nchini tayari umeshafanyika ambapo zimetambuliwa Kanda za kilimo kulingana na kiasi cha mvua zinazonyesha na aina ya mazao yanayopandwa katika kila Kanda. Serikali imekuwa ikiratibu mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo kwa kila Wilaya na Mkoa kwa aina na kiasi kinachowajibika. Baada ya kupokea mahitaji hayo, Serikali huwasiliana na Makampuni ya Pembejeo za Kilimo ili kuhakikisha uwepo wa pembejeo hizo kwa wakulima kwa wakati kabla ya msimu wa kilimo haujaanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013 mahitaji ya mbolea nchini yanakadiriwa kuwa tani 485,000. Pamoja na mahitaji ya pembejeo kujulikana na makampuni bado imekuwepo changamoto kwa baadhi ya Mikoa kutofanya tathmini ya mahitaji halisi ya pembejeo kwa maeneo yao na kuwahimiza wakulima kununua pembejeo mapema.

Changamoto hizo zimesababisha Mawakala kukaa muda mrefu bila kuuza kutokana na wakulima kusubiri hadi mvua zinyeshe ndipo wanunue pembejeo. Hali hiyo, husababisha Mawakala kuingia gharama kubwa za kulipa uhifadhi, kuchangia ucheleweshaji wa pembejeo kwenda kwa wakulima. Wizara yangu imeshajipanga kuhakikisha kuwa mbolea zinawafikia walengwa kwa wakati na pia itaendelea kuwahamasisha wakulima kununua pembejeo mapema kabla ya msimu kuanza.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wakulima wanapata mikopo kwa ajili ya pembejeo, Serikali katika msimu wa mwaka 2013/2014 mwaka unaokuja, inatarajiwa kuweka utaratibu wa utoaji wa mikopo ya pembejeo kwa wakulima ambao utahusisha mabenki. Utaratibu huo utafanyika kwa mabenki kuvikopesha vyama au vikundi vya ushirika vilivyosajiliwa ambavyo navyo vitawakopesha wakulima wao ambao ni sehemu ya wanachama wao.

Aidha, Serikali itavidhamini Vyama vya Ushirika vitakavyokopa katika mabenki hayo na riba kwa mikopo itakayotolewa inatarajiwa kuwa asilimia nane na mikopo hiyo itatolewa kwa wakulima kupitia vikundi vyao, hivyo wakulima wanahamasishwa kujiunga katika vikundi ili kuweza kunufaika na utaratibu huo kwa msimu ujao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari tani zinazokadiriwa 19,000 za mbolea ya kupandia aina ya Minjingu Mazao pamoja na Vocha 421,000 za mbegu na mbolea zimekwishapelekwa katika Wilaya zinazoanza msimu wa kilimo ikiwemo Kasulu.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Serikali imejitahidi kupeleka Mbolea Wilayani kwa wakati, lakini pia Kasulu mvua zinaanza kunyesha mwezi wa Tisa na mwanzoni mwa mwezi wa kumi wakulima wameanza kupanda mazao. Kitu cha kusikitisha Kamati ya Mbolea imekaa kikao tarehe 6 mwezi wa Kumi na Moja mwaka huu, wakati huu wakulima wanaanza palizi, naiomba Serikali itoe tamko mbolea hii ambayo iko Kasulu na mpaka leo hii ninapozungumza haijasambazwa kupelekwa kwa wakulima. Je, itakapopelekwa kwa wakulima italeta faida gani kwa maslahi ya Taifa?

Pili, nahitaji kujua uzembe uliofanyika mpaka kuwakosesha wakulima mbolea ni hatua gani zitachukuliwa kwa makampuni haya ambayo yamesababisha wakulima wa Wilaya ya Kasulu kupanda bila mbolea? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI A KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mbolea inayokwenda kama tulivyosema kwenye mfumo huu wa Vocha, ni mbolea ambayo Serikali imeingia makubaliano na makampuni haya ya mbolea. Kwa hiyo, tuna makubaliano na Minjingu Mazao lakini tulikubaliana na makampuni mengine ambayo yanaleta *DAP*, *KAN, UREA* na mbolea zingine ambazo zinakwenda kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, makubaliano haya yanataka mbolea hii iende kule kwa watumiaji. Tumeshatenga, kama tulivyosema kwa mujibu wa swali la msingi, Kanda hizi zinasababisha mbolea ziende kwa wakati huu kabla wakulima hawajaanza kupanda. Lakini ikifika kule, kuna Kamati za Mbolea ambazo wewe mwenyewe umesema Mheshimiwa Mbunge, ni Kamati zenu.

Kamati ya Mbolea ya kule, ni kama Kamati ya Wilaya; inasimamiwa na Mkuu wa Wilaya (*DED)* na watu wenu wote, pamoja na wewe mwenyewe kama Mbunge, unahusika kuwemo kwenye Kamati ile, ili kuhakikisha kwamba, mbolea zile na vocha zimefika, ziwaendee wakulima.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba, tumepata malalamiko ya kwamba, mbolea zimekwenda na vocha zimekwenda, lakini hazijaanza kugawiwa. Kwa hiyo, tumefika hatua ya kusema, sasa huu sijui kama ni uzembe au kama ni makusudi, lakini tunataka tuangalie tujue ni nini kilichotokea. Kwa sababu, inaonekana mabadiliko ya mwaka jana kwenda mwaka huu ni madogo sana, yanahusisha wajibu wa Mawakala tu. Mwaka huu tumesema yule mtu anayepeleka mbolea na Wakala, wote wawajibike kwa pamoja kuhusu kufikisha mbolea kwa wakulima; zamani Kamati hizi za mbolea ndio zilikuwa zinateua Mawakala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonekana hapo kuna jambo ambalo linaonekana linakwenda ndivyo sivyo. Lakini ni kweli, malalamiko aliyoyasema Mheshimiwa Agripina, yanaonekana yamejitokeza pia kwenye Wilaya nyingine za Tanzania. Mheshimiwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu, anawajibika kwenye Kamati hizi, na Wakuu wa Wilaya na Watendaji wao, tunataka tujue ni nini kilichotokea kwa vocha ambazo zilishafika na hazijagawiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda kama mnavyoona umekwisha sana, tuko karibu saa tano kasoro. Kwa hiyo, naomba niwatambue kwanza baadhi ya wageni waliopo.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wapo wafanyakazi watano wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa Zanzibar, wakiongozwa na ndugu Omary Khamis. Naomba wasimame mahali walipo, wote? Ahaa, wapo sehemu hii huku; ahsanteni, karibuni sana. Naamini mtakuwa na kitu cha kujifunza kutoka kwetu. *(Makofi)*

Kuna Kikundi cha ***Lufedha*** *Film Tanzania,* wakiongozwa na ndugu Mussa Omari Bukilo. Hawa **lufedha** wako wapi? Wasimame walipo? Hawa ni Wasanii; nadhani wamekosa nafasi, wataingia.

Tuna wageni kutoka Bunge la Kenya, watumishi kutoka Bunge la Kenya, naomba wasimame walipo? **Watumishi kutoka Kenya yupo ndugu Jeni Mkinda, yupo Palikap Mbori, yupo Caroline Wasirwa, yupo Elisabeth Manyai na Dereva wao Martin James. Karibuni sana, sisi ni wamoja tuna Umoja wa *Speakers* katika *East Africa* kwa hiyo, mnakaribishwa sana katika** shughuli mliyokuja kufanya. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 47 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wasimame walipo? Wanafunzi wa *UDOM?* Nafikiri kumekosekana nafasi.

Wapo wanafunzi 77 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi ya Sayuni, Manyoni, wakiongozana na Mwalimu wao **Valeria** Kitwange. Wanafunzi wa Manyoni wako wapi? Wasimame wote pamoja na Walimu? Wako wapi? Wako kule nyuma? Bahati mbaya. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 70 kutoka Chuo Kikuu cha **Sekuko**, Lushoto – Tanga. Naomba wasimame walipo? Sijawahi kukisikia hiki; hebu simameni Wanafunzi wa Chuo Kikuu hiki, wote na Walimu wao kama wapo na wao wamekosa nafasi. Watu wengi wana-*rush* dakika za mwisho kwa hiyo, nafasi zinakuwa chache.

Tunao Wanafunzi 22 kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Daudi **Nyalulu**. Hawa na wenyewe wako wapi? Eeh! Haya.

Tuna Wanafunzi wengine 82 na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari **Kanosa**, Dar-es-Salaam. Kama wapo humu ndani wasimame na Walimu wao? Ahaa, afadhali, ahsante sana; karibuni sana Kanosa, mmependeza sana. *(Makofi)*

Naona siku za mwisho kuna *rush time* ya Wageni. Kwa hiyo, wengine hawa hawakupata nafasi, watapata pengine mchana.

Tuna Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo Wageni wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, ambao ni Waheshimiwa Madiwani 15 wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, wakiwa pamoja na wataalam watatu na Madereva wao wawili, wakiongozwa na Mheshimiwa Andrew Mhagama, Diwani wa Gumbiro na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo. Makamu Mwenyekiti, kwanza asimame. Ahsante sana na Waheshimiwa Madiwani, msimame. Ahsante sana, karibuni sana; nyie ndio majirani zangu kule mahali, karibuni sana. *(Makofi)*

Ninao Wageni wanne wa Mheshimiwa Moses Machali, kutoka Chuo Kikuu Cha *Saint Augustine,* Mwanza, wakiongozwa na Ndugu **Fanuel** Sindika. Hawa wako wapi? Ahsante, karibuni sana. Ahsante sana na msome vizuri. *(Makofi)*

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Ezekiel Wenje, ambao ni ndugu Emmanuel **Mtaro** na Ndugu Venance Mayuki, sijui ni akina nani hawa? Wasimame walipo? Ni vizuri kusema Wadhifa wao kusudi tuweze kufaidika nao. Nafikiri wamekosa nafasi.

Kuna Mgeni wa Mheshimiwa Halima Mdee, ambaye ni Ndugu Daudi Wakota na yeye pia tungepewa wadhifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Mgeni wa Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe, ambaye ni ndugu Edward **Stephen** Mangi, Katibu wa Wazazi, Serengeti. Asimame huyu? Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Vincent Nyerere, ambao ni Viongozi na Wachezaji kutoka *Polisi Mara Sports Club,* wakiongozwa na *Inspector* David **Sungura**; hawa wako wapi? Naomba wasimame walipo? Nafikiri nao pia wamekosa nafasi.

Tuna Mgeni wa Mheshimiwa David Kafulila, ambaye ni Ndugu Adam **Suleiman**, yeye ni Mwenyekiti wa *NCCR* Mageuzi, Kata ya **Kalia**, Jimbo la Kigoma Kusini; asimame huyu alipo? Nafikiri pia ni tatizo hilo hilo.

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Paul Lwanji, ni Walimu kutoka Shule ya Msingi ya *Saint Vincent* ya Mitundu, Tarafa ya Itigi, wakiongozana na Sista **Salome** Timoti; hawa wako wapi? Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambao ni Wanakikundi 77 wa Jumuiya ya Akiba ya Mikopo na Maendeleo, inaitwa **JAMIIMADO** na Viongozi wawili kutoka Dodoma. Wenyewe wako wapi wa *JAMIIMADO?* Wako wapi? Nao pia inawezekana, wamekosa nafasi.

Wahesimiwa Wabunge, hawa ni baadhi ya wageni na wengine wote mnakaribishwa.

Sasa shughuli za kazi: Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo watakutana Saa 7.15 katika Ukumbi Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana, kutakuwa na Kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa B.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo Saa 7.00 mchana, baada ya kuahirisha Bunge. Kutakuwa na Kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Ofisi inatangaza kwamba, wale Wabunge, ambao hawajachukua Fomu za Maadili ya Viongozi wa Umma, wafike mapokezi Jengo la Utawala, ili waweze kuchukua Fomu hizo.

Waheshimiwa Wabunge, narudia; usipochukua na mwezi Disemba ndio mwisho wa kurudisha hizi fomu; wapo wengi pale hawajachukua, naona mafaili yamejaa pale mlangoni. Mjitahidi kila mmoja wenu awe na hizo fomu na zirudishwe kabla ya mwisho wa mwezi wa 12; siku zimekwisha, ukisema utafanya kesho, hautafanya na utafunguliwa kesi Mahakamani, mnajua hilo!

Halafu wale Wabunge wengine, ambao hawajapiga picha na kuchukuliwa alama za vidole kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa, wafike Ukumbi wa Msekwa, ili wapate huduma hiyo.

Huduma zote hizi mbili siku yake ya mwisho ni tarehe 9, maana yake kesho. Ili kuepuka usumbufu ambao Wabunge mnaweza kuupata mkitaka kupata huduma hii nje ya hapa Bungeni, ni vyema mkafanya hivyo mapema kwa sababu, hapa ni sisi wenyewe, mkikosa hapa maana yake mkatafute Ofisi ya Tume, mkatafute Ofisi ya *NIDA,* kitu ambacho ni usumbufu sana tukiwa Dar-es-Salaam; fanyeni hivyo leo, kadiri iwezekanavyo.

Katibu! Enhee, Mheshimiwa Machali, nini?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kuhusu nini sasa? Haya.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kuweza kuomba Mwongozo wako. Ninaomba Mwongozo wako kuhusiana na Hoja Binafsi ambazo tunategemea ziweze kuwasilishwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kuna Hoja takribani zipatazo saba na kwa kuwa, tunaona kwamba, hizi Hoja ni Hoja ambazo zinagusa mambo muhimu ya Taifa letu; kuna Hoja za Ardhi hapa na kumekuwa kuna changamoto nyingi. Ukienda pia kuna Hoja kwa mfano, Hoja ambazo zinahusiana na masuala ya elimu, sasa...

**SPIKA:** Mheshimiwa, naomba Mwongozo uwe mfupi; sasa ukianza kuhutubia, tunatumia muda. Uliza tu, halafu tutakupa Mwongozo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mwongozo wako kuhusiana na ni kwa nini, tusiweze kuhakikisha kwamba, pengine ziwasilishwe Hoja mbili, ili kuweza kuepuka suala la kulipua? Maana vinginevyo, itakuwa ni suala la aidha Hoja zisomwe, halafu kisha hakuna mjadala na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, kwa maslahi ya nchi yetu. Hili suala la kuweza kuwasilisha Hoja saba siku ya leo na wakati kumekuwa kuna Hoja za Serikali, zinakuja tunajadili siku moja mpaka siku mbili...

**SPIKA:** Jamani uliza swali, Mheshimiwa Machali, uliza swali, usijadili, shida yako ni nini?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako ni kwa nini tusiweze kujadili Hoja ambazo hazizidi mbili kulingana na uzito wa Hoja hizi, ni sababu gani ambazo zimesababisha tupangiwe ratiba ambayo ina Hoja nyingi?

**SPIKA:** Ahsante. Kwanza umetangulia mno kabla ya Kifungu kinachofuata. Katibu!

**KAULI ZA MAWAZIRI**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49 (1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kutoa Kauli ya Serikali, kuhusu tatizo la upungufu wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa wiki mbili sasa nchi imekabiliwa na upungufu mkubwa wa bidhaa ya mafuta ya dizeli na petroli katika maeneo mbalimbali ya nchi. Aidha, mahitaji ya nchi kwa matumizi ya siku moja ni wastani wa lita 1,700,000 za petroli 3,540,000 za dizeli na lita 200,000 za mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu?

**SPIKA:** Naomba amalize kusoma; Utaratibu gani? Anasoma Taarifa ya nanihii…

**WABUNGE:** Hawajagawa?

**SPIKA:** Hawajagawa? Nakala hamjagawa?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hatuna nakala.

**SPIKA:** Naona wamecheleweshа hawa. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, mwezi Agosti, 2011 hali kama hii ilijitokeza. Tofauti pekee ni kuwa, mwaka jana mafuta yalikuwepo na wafanyabiashara walikataa kuuza kutokana na bei kushuka. Hata hivyo, juhudi za pamoja kati ya Wizara yangu na *EWURA* zilifanikisha mgomo huu kwisha. Baadaye Wafanyabiashara walifungua kesi kwenye Mahakama ya Usuluhishi wa Ushindani wa Kibiashara *(The Fair Competition Tribunal)* wakipinga uamuzi wa *EWURA* wa kushusha bei za mafuta. Hata hivyo, mwezi uliopita Mahakama hiyo ilitoa hukumu kuwa uamuzi wa *EWURA* ulikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zilizosababisha upungufu uliojitokeza mwaka huu ni zifuatazo:-

(1) Kampuni ya uagizaji mafuta kwa pamoja *(Petroleum Importation Cordinator – PIC)* kutokuwa na mipango madhubuti ya uagizaji wa shehena za mafuta kulingana na mahitaji ya nchi.

(2) Uwezo mdogo wa miundombinu ya Bandari ya Dar-es-Salaam, kupokea shehena za mafuta, ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la sasa la mahitaji ya nchi yetu na majirani zetu wanaotumia Bandari ya Dar-es-Salaam.

(3) Kuwepo kwa matatizo ya uhaba wa mafuta kwa majirani zetu na kulazimika kutolewa Vibali Maalum *(Priority Bathing)* kwa meli zenye shehena za mafuta yaendayo nje, bila kuzingatia mahitaji ya ndani.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri ikaeleweka pia kuwa, Kampuni za Mafuta zinailalamikia *EWURA* chini chini kuhusu Kanuni ya Kupanga Bei za Mafuta. Mara nyingi malalamiko ya Kampuni za Mafuta, hujitokeza pindi bei za mafuta zinaposhuka na wakati mwingine hata kuficha mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* ilianzisha mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja, chini ya Sheria ya Petroli ya

Mwaka 2008 na kuunda Kampuni ya *PIC,* inayoongozwa na wafanyabiashara wa uagizaji wa mafuta ambayo ilianza rasmi kufanya kazi mwishoni mwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kabla ya utaratibu wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja kuanza kila kampuni iliagiza mafuta peke yake na kwa utaratibu wake na hivyo kuibuka kwa matatizo mbalimbali, ikiwemo kukosekana kwa udhibiti wa bidhaa ya mafuta yatumikayo ndani ya nchi na yasafirishwayo nje ya nchi. Kukosekana kwa udhibiti wa ubora wa bidhaa za mafuta na hivyo, kusababisha Serikali na watumiaji wa bidhaa hii kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, hali hii ilisababisha kuanzishwa kwa mfumo wa uagizaji wa pamoja. Pamoja na matatizo madogo madogo yaliyojitokeza, lakini mfumo huu umekuwa na faida kubwa. Maana pamoja na mambo mengine, tumeweza kubaini kiwango halisi cha matumizi ya mafuta nchini, kwani takwimu zinaonesha matumizi kwa siku ni zaidi ya lita milioni tano, kinyume na ilivyokuwa inajulikana kuwa ni chini ya lita milioni mbili tu za mafuta ya dizeli, petroli na ya taa.

Mheshimiwa Spika, tulipoanza utaratibu huu wa zabuni, ya kwanza ilikuwa ni ya miezi miwili, yaani Januari na Februari, 2012 ambayo kulikuwa na meli 17. Meli nane za kwanza zilipaswa kushusha mafuta Januari, 2012 na meli tisa zilipaswa kushusha mwezi wa Februari, 2012. Kutokana na miundombinu isiyokidhi mahitaji yetu na kwa kuwa pia tunahudumia meli za nje, jambo ambalo ni jema, hatukukamilisha ushushaji wa mafuta kwa wakati, hivyo kusababisha kuanza kuwepo kwa msongamano wa meli bandarini.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni ucheleweshaji wa wafanyabiashara kukamilisha taratibu za malipo katika zabuni ya pili na ya tatu, hivyo kusababisha meli kuchelewa kuingia bandarini kwa muda wa zaidi ya siku 10. Ucheleweshaji wa siku 10 ni siku nyingi sana kwa nchi kutumia mafuta bila kupakua mengine. Ucheleweshaji huu, ulisababisha hata mafuta ya kwenda nje ya nchi kuchelewa na kusababisha majirani zetu wa Burundi, Rwanda na Zambia, kuomba wapewe kipaumbele *(Priority Berthing).*

Mheshimiwa Spika, Bodi ya *PIC* nayo, haikutekeleza wajibu wake kama ipasavyo kwa kutokuwa na mipango madhubuti ya uagizaji wa shehena za mafuta, kulingana na mahitaji ya nchi. Jambo ambalo limechangia kwa kiasi fulani kuathiri upatikanaji wa mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo, Serikali, ikalazimika kuingilia kati, ili kuhakikisha hali ya upatikanaji wa mafuta inarejea nchini haraka iwezekanavyo. Tarehe 2 Novemba, 2012 Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Sospeter Mhongo, alikutana na Wadau wa Sekta ya Mafuta, ikiwemo Kampuni ya Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *PI,* na kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kwamba asilimia 50 ya mafuta yaliyokuwa yanakwenda nje ya nchi yaani *transit fuel* yauzwe ndani ya nchi;

(ii) Jitihada za makusudi zinafanywa na Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi, kuhakikisha kuwa boya jipya kubwa la kupakulia mafuta *SBM* linaanza kazi mapema kadri iwezekanavyo;

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini itaziangalia upya kanuni za uagizaji wa mafuta wa pamoja ili ziweze kukidhi matakwa ya mfumo wa uagizaji wa pamoja kwa maslahi ya Taifa. Kwa wakati huu Serikali imelazimika kuunda upya Bodi ya *PIC*, ili kurekebisha upungufu uliojitokeza.

(iv) Serikali inaendelea na juhudi zake za kuanzisha mpango wa Hifadhi wa Mafuta ya Taifa (*Strategic Petrolium Reserve)* kwa lengo la kujihakikishia uwepo wa mafuta nchini wakati wote kwa ajili ya usalama wa nchi wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya usambazaji wa mafuta nchi kwa sasa, kutokana na jitihada hizi zote za Serikali kuanzia tarehe 30 Oktoba, 2012 mafuta ya aina zote yameanza kuchukuliwa kutoka kwenye maghala ya mafuta Dar es Salaam kwenda katika maeneo mbalimbali ya nchi. Taarifa za usambazji wa mafuta kwa lita za ujazo tangu tarehe 30 Oktoba, 2012, hadi tarehe 5 Novemba, 2012 ni kama ifuatavyo:-

Tarehe 30 Oktoba, *petrol* iliyotoka Dar es Salaam kupelekwa mikoani ni lita milioni 1,636,000; *diesel* ni lita milioni 3,263,600 na mafuta ya taa ni lita 698,200.

Tarehe 31 Oktoba, *petrol* ni lita milioni 2,104,600; *diesel* ni lita ni milioni 4,389,380 na mafuta ya taa ni lita laki 446.

Tarehe 1 Novemba, *petrol* ni lita milioni 1,612,500; *diesel* ni lita milioni 5,104,700 na mafuta ya taa ni lita 233,500.

Tarehe 2 *petrol* lita milioni 2,475,500, *diesel* lita milioni 5,854,000 na mafuta ya taa ni milioni 2,072,000.

Tarehe 3, *petrol* ni lita milioni 2,192,750; *diesel* lita milioni 3,906,930 na mafuta ya taa ni lita 3,000.

Tarehe 4 *petrol* lita 47,000; *diesel* ni lita 632,500 na mafuta ya taa lita 23,500.

Tarehe 5, *petrol* lita milioni 2,184,300, *diesel* lita milioni 5,539,519 na mafuta ya taa lita 48,500.

Siku ya Jumapili ya tarehe 4 usambazaji ulishuka kwa kuwa baadhi ya Makampuni ya Mafuta hayafanyi kazi siku za mwisho wa wiki na mengi hufanya kazi kwa nusu siku.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na *EWURA* na Makampuni ya mafuta na wadau wengine wote muhimu ili kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mafuta nchini unarejea katika hali ya kawaida. Aidha, hali ya upungufu itakuwa ikiisha taratibu kwa kuwa upungufu ulishakuwa mkubwa kwenye baadhi ya mikoa nchini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya usambazaji wa mafuta kwa mikoa na kwa kiwango kilichopelekewa tangu tarehe hiyo niliyoitaja na mpaka tarehe 5 tumeambatanisha katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 49(2) ambayo inazungumzia kauli ya Mawaziri kwamba zinapaswa kuwa mahususi, halisi na zisizozua mjadala.

Mheshimiwa Spika, kauli iliyotolewa, kwanza naishukuru Serikali kwa kutoa kauli, lakini na mambo mengine ambayo si halisi na ina mambo yenye kuzua mjadala ambayo nitaomba mwongozo wako ili utumie mamlaka yako ama kuwezesha kauli hiyo kujadiliwa, au kuwezesha kauli hiyo kuelekezwa kwenye Kamati ya Bunge itakayoishughulikia, kwa sababu kuna taarifa ambazo Serikali imezificha kuzieleza kwa uhalisia wa hali halisi ilivyo, nikitoa kwa mfano, tu ukurasa wa pili..

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika wewe sema tu umeficha wapi, we sema unachotaka kusema, maneno mengine ambayo yana…..

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Unaonyesha kwenye taarifa hii ya Serikali…

**SPIKA:** Sema siyo kamili lakini amefika, nasema siyo kamili…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Siyo kamili.

**SPIKA:** *Okay*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Siyo kamili kwa mfano, ukurasa wa pili kwenye suala la uhaba wa mafuta kutokana na kupeleka nchi jirani kwa maana ya *priority bathing* undani wa taarifa na ukamilifu wa taarifa ni kwamba, kulifanyika utaratibu vile vile wa kutoa kipaumbele kwa makampuni machache ya mafuta katika mazingira yaliyokuwa na viashiria vya upendeleo kwa ajili ya kufanya biashara yao ya kupeleka mafuta mazito na hivyo kuathiri zoezi la usambazaji wa mafuta kwa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Lakini kwenye aya inayofuatia Serikali inasema…

**SPIKA:** Kwa hiyo usijadili we sema unataka kuniuliza nini, si mwongozo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ninachotaka Mwongozo wako kwa ujumla wake ili nisipoteze muda wa Bunge katika hatua ya sasa hii kauli ina maeneo mengi ambayo yameficha baadhi ya uhalisia wa mambo na yana mambo yenye kuzua mjadala.

Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako ama hii kauli ijadiliwe au ipelekwe kwenye Kamati ya Bunge kwa haraka ili ukweli halisi ukaelezwe na Bunge litumie mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 kuishauri na kuisimamia Serikali ili tatizo hili lisijirudie kwa kuzingatia tulishaazimia Agosti, 2011 lakini hali hii imejirudia tena.

**SPIKA:** Sawa nimesikia. Sasa nitoe mwongozo kuhusu lile alilozungumza Mheshimiwa Machali, yeye Machali alikuwa ametangulia tu kwenye kazi ya leo aliwahisha ratiba, kwa mujibu wa kanuni siyo sawa.

Sasa leo hii tumepanga hoja binafsi ziko kama saba na tumeziweka tu lakini zinajadiliwa leo na kesho siyo kwamba hizo zinapaswa zijadiliwe leo. Tumeweka zote kwa sababu huwezi kujua mnaweza mkafika mahali watu wengine hawajadili, mmekwisha hakuna wa kujadili sasa mnabakia mnaachia kumbe hoja zingine zipo. Kwa hiyo, tunakwenda kadri tutakavyokwenda, lakini hizi zinaendela mpaka kesho.

Utaratibu wa kujadili kuna mmoja hapa ameniuliza, ni vizuri hapa tungeangalia jinsi kanuni yetu inavyotuhitaji. Hoja ya Mbunge binafsi yeye mwenyewe atasimama mahali pake

atakapoitwa na kutoa hoja yake pale alipo halafu akiungwa mkono ndiyo atakuja, yaani ukitamka tu pale lazima kwanza wakuunge mkono wenzio, wakishakuunga mkono basi unaweza kuendelea na maelezo yako.

Lakini hoja hiyo hiyo inaweza pia kufanyiwa mabadiliko ama na wewe mwenyewe mwenye hoja au wengine. Unaweza kuifanyia mabadiliko wewe mwenyewe mwenye hoja au kwa maana ya kuondoa maneno ama kuongeza maneno bila kuondoka kwenye msingi wa hoja inayostahili.

Baada ya mjadala kama watu wengine hawapo wanaotaka kujadili hoja ile basi yule aliyetoa hoja atajibu baadhi ya yale maneno yaliyozungumzwa na halafu ataomba kutoa hoja, tutapiga kura, huo ndiyo utaratibu wa kujadili hoja hizi ambazo zipo.

Tumeziweka hapa zote si kwamba kwa ajili ya leo tu, tumeweka kwa sababu inawezekana zingine zikawa na wazungumzaji wengi, lakini pale tutakapofikia leo, tutaendelea na kesho. Kwa hiyo, tutaanza kadri itakavyofuata na wale wanaoleta mabadiliko lazima yaletwe kwa Spika yakiwa yameandikwa na yamesainiwa na wanaohusika kama wapo. Katibu!

## HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

### Hoja Binafsi juu ya Kusitisha Ugawaji wa Ardhi hadi Tathmini ya Kina Itakapofanyika Kujua Kiasi cha Ardhi Kilichoko Mikononi mwa Wageni

**SPIKA:** Tunaanza na Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 54(1), 54(2) na 54(3) za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 naomba kutoa hoja binafsi ya kuitaka Serikali kusitisha zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje, mpaka pale tathmini ya kina itakapofanyika kuweza kubaini kiwango gani cha ardhi kiko mikononi mwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni kufuatia mtikisiko wa uchumi duniani uliokwenda sambamba na upungufu wa chakula tumeshuhudia wimbi kubwa la wawekezaji kutoka nje wakinunua na kumilikishwa au kukodishwa maeneo makubwa ya ardhi nchini kwa maelezo kwamba wana nia ya kuwekeza kwa manufaa ya wananchi wenyeji na Taifa kwa ujumla. Hali ambayo itaweza kusaidia upatikanaji wa ajira, kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji wanaona ardhi kama biashara nzuri na yenye tija katika miaka ya baadaye na kwa nchi tajiri zinazoagiza vyakula toka nje yaani China, Japan, Korea Kusini, Saudi Arabia na kadhalika wanaona umiliki wa mashamba makubwa kama njia ya kujihakikishia usalama wa chakula katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo makampuni binafsi makubwa ya Kimataifa wanaiona hii kama fursa ya kujitanua kibiashara na kutengeneza faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kwamba, kati ya mwaka 2001, kulikuwa na maombi ya ardhi ya zaidi ya hekta milioni 203, katika nchi zinazoendelea. Hii ni sawa na maombi ya heka 55,616 kila siku katika kipindi cha miaka kumi. Hali kadhalika nchini Tanzania katika miaka ya karibuni, takribani hekta milioni nne zimeripotiwa kuombwa na wawekezaji wa nje wa kilimo cha mazao ya mafuta (*Agrofuel)* na chakula.

Mheshimiwa Spika, kasi ya maombi ya ardhi na hatimaye kumilikishwa ardhi wageni imegeuka shuruba kwa wananchi wengi wao wakiwa ni wakulima wadogo wadogo ambao wamejikuta wakiondolewa katika maeneo yao ya asili ili kuwapisha wageni. Wengi wao wakiwaachwa hohehahe na katika lindi la umaskini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na ukweli kwamba kumekuwa na tafsiri ambayo siyo sahihi kwamba ardhi wanayopewa wawekezaji haina wenyewe wakati ukweli ni kwamba maeneo mengi kama siyo yote yalikuwa yanatumiwa na wakulima wadogo*. (Makofi)*

Hali halisi inaonyesha kwamba ni sehemu ndogo sana ya ardhi inayochukuliwa na wageni inatumika kwa manufaa ya kutatua ama kupunguza matatizo ya njaa katika nchi husika. Halikadhalika maeneo mengi ya ardhi yanayochukuliwa na wawekezaji huwa hayaendelezwi kama inavyopaswa na yale ambayo yanaendelezwa, yanaendelezwa kwa kiwango kidogo sana huku wananchi wengi wakiachwa pasi na ardhi ya kutosha kwa kilimo na katika hatua nyingine wawekezaji baada ya kupata ardhi husika kwa bei ya kutupwa hawaitumii wanaisubiri ipande thamani kisha kuiuza kwa faida kwa wawekezaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako Tukufu likubaliane na hoja ya kuitaka Serikali kusitisha zoezi la ugawaji wa ardhi ili kuweza kutoa fursa kama nchi kuweza kujitathmini kwa kina, wapi tumekosea ili tuweze kujipanga upya kwa manufaa ya wananchi na nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na ukweli kwamba, hata Wizara ya Ardhi leo, wakitakiwa kutoa taarifa sahihi ya ardhi kiasi gani iko chini ya miliki ya wageni hawana takwimu sahihi. Zaidi ya zile chache zilizopatikana kupitia *Tanzania Investment Center* (*TIC)* na ambazo pia zimethibitika kuwa na mgogoro mkubwa kutokana na taratibu kutokufuatwa.

Mheshimiwa Spika, mifano mingi inaonesha kwamba, kumekuwa na ubabaishaji mkubwa sana kwa kuumizwa sana kwa wananchi na mbaya zaidi katika mazingira mengine Serikali imekuwa kuwadi dhidi ya wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge kutambua kuwa matatizo ya ardhi yanayoikumbuka Rufiji, Kilombero, Bagamoyo, Kisarawe, Lugufu, yanaikumba pia Muheza, Pangani, Katavi, Meatu, Kinondoni, Njombe na Ngorongoro. *(Makofi)*

Hivyo basi, kuna haja kubwa ya kujenga mshikamano kwa kuunganisha nguvu ili kulinda maslahi na rasilimali za umma. Nitatoa mifano michache kuonesha uzito wa tatizo hili. Bonde la Mto Rufiji, Rufiji *River Basin*, hili ni eneo lenye ukubwa la kilomita za mraba 176,000 linajumuisha Rufiji *Delta*, Luwero, Kilombero na Mto Ruaha. Asilimia 93 ya wakazi ya maeneo haya wanaozunguka eneo hili wapatao laki tano wanajishughulisha na kilimo kama wakulima wadogo wadogo.

Kutokana na umuhimu na unyeti wa eneo husika kumekuwa na wimbi kubwa la makampuni ya kigeni wakipeleka maombi moja kwa moja kwa vijiji ama kupitia baadhi ya vyombo vya Serikali kama *RUBADA (*Rufiji *Basin Development Authority)* ambapo vimeacha majukumu yake na kugeuka kuwadi wa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makampuni yafuatayo: *SEKAB Tanzania Limited* ya Sweden, *African Green Oil Limited, SAP Agriculture Limited (Turkey), RUBADA, na Korean Rural Community Corporation, Kilombero Plantation Limited ya Britain, Kilombero Valley Teak Company Limited ya Britain, Kilombero Sugar Company Limited* ya South Africa, Kilimo cha Yesu ya Uswiss na

*Eurovistas* ya India ni kati ya makampuni yaliyomilikishwa ardhi iliyokuwa inatumiwa na wanakijiji kwa shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi wao walitolewa kwa nguvu ili kuwapisha wawekezaji kwa kurubuniwa kwa kauli tamu wakiahidiwa kuletewa maendeleo ahadi ambazo nyingi zimegeuka za uongo huku tayari vijiji vikiwa vimepoteza uhalali wa kutumia ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kwamba katika ukanda huu ukiacha makampuni ya Kilimo cha Yesu ya Uswiss na Kilombero *Sugar Company*, Kilombero *Plantation Company* na Kilombero *Valley Teak* ya Britain wawekezaji wengine wakabidhiwa maelfu ya ardhi ya Watanzania wameyaendeleza kidogo sana au kuyatelekeza kabisa. Inawezekana wakisubiri ardhi ipande thamani wawakabidhi wenzao kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mfano mwingine ni wa Kisarawe. *Sun Biofuel Limited* ni kampuni ya Kiingereza inayojishughulisha na kilimo cha Jatrofa, wanahisa wake wakubwa ni kampuni *Sun Biofuel Plc* ya Uingereza yenye hisa asilimia 88 *Julian Ozanne* (Mwingereza) mwenye hisa kumi na Watanzania wawili Daudi Mwakobore na Herbert Marwa wenye hisa mbili yaani hisa moja kila mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasemekana mwekezaji huyu alipanga kuwekeza kiasi cha shilingi milioni 25 za Kitanzania lengo likiwa kujenga mtambo wa kufulia mafuta na kilimo Jatrofa pamoja na mihogo kwa ajili ya kuwalisha vibarua.

Mheshimiwa Spika, ilikadiriwa kutokana na uwekezaji huo zingepatikana ajira za kudumu 1500 na ajira za ziada hasa wakati wa uvunaji. Mwaka 2009 kampuni ilifanikiwa kupata eneo lenye ukubwa wa hekta 8200 kutoka Vijiji 11, Mtamba, Muhanga, Malumbo, Palaka, Kidugalo, Kurui na asilimia 40 ya eneo la Kijiji cha Kurui ilichukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwezi Oktoba, 2011 mradi husika ulisimama kutokana na ukosefu wa fedha na mustakabali wa ardhi za vijiji haujulikani. Mwanakijiji mmoja wa Kijiji cha Palaka, Kisarawe alinukuliwa akisema kwamba, walikubali kuachia wawekezaji kwa mdomo pasipo kuandika popote kwa sababu waliziamini ahadi zao za kutoa huduma za jamii bure yaani maji, barabara na kadhalika. Lakini hakujua ni kiasi gani cha eneo lake kinapaswa kuchukuliwa kwa sababu hawakuwa na nyaraka zozote za kuonesha mipaka ya shamba lake, hakuwa anafahamu haki zake za kisheria. Hivyo, hakujua madhara ya kile alichokikubali mpaka alipoteza ardhi yake yote bila kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, Rukwa, eneo hili linahusisha hekta 80,317 eneo la Katumba na hekta 219,800 eneo la Mishamu kwa ajili ya kampuni ya Kimarekani *Agrisol,* majadiliano yanaratibiwa na viongozi wakubwa sana, Serikali ikiwemo Waziri Mkuu mradi huu umejikita kwenye uendelezaji wa mashamba makubwa na matumizi ya mbegu yenye viini tete yaani *GMO*.

Mheshimiwa Spika,Ili kufanikiwa kwa mradi huu wakulima wadogo wapatao 162 walitakiwa kuhama kumpisha mwekezaji kwa tafsiri ambayo inatumika kwamba ni wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, licha ya kelele nyingi kupigwa juu ya makosa ya kiufundi ambayo Serikali inayafanya kwa kutaka kulikabidhi eneo kubwa na lenye rutuba kwa wageni na licha ya aliyekuwa mshirika mkuu wa *Agrisol IOWA State Univervisty College of Agriculture* na aliyekuwa mhimili muhimu kwa mwekezaji huyu hasa katika kuwasaidia wakulima wadogo kujitoa baada ya kugundua kwamba mwekezaji huyu hana dhamira ya kuisaidia nchi wala wakulima wadogo zaidi ya kujinufaisha kibiashara na kwamba alitumia chuo husika ili apate uhalali wa kukubalika kirahisi kama mwekezaji mahiri, lakini Serikali inaonekana bado imeziba masikio*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wawekezaji walionunua ardhi Mkoa wa Kigoma ni *Agrisol* na *Felisa*, *Felisa* amenunua ekari 3000 katika Wilaya Uviza Kijiji cha Basanza, Kata ya Uviza, wawekezaji hawa wamewakuta wakulima na wafugaji katika maeneo hayo. Wafugaji na wakulima wakagoma kuondoka kwa kuwa walikuwa wakiendesha maisha yao kutegemea ardhi hiyo. Huu ni ushahidi dhahiri kuwa, hakuna ziada ya ardhi ukilinganisha na mahitaji. *(Makofi)*

Mwekezaji kwa kushirikiana na vyombo vya dola alianza zoezi la kuwatoa wananchi mwezi Mei mwaka huu, alitumia vikosi vya Mgambo kwa kuchoma nyumba, kuharibu mazao, hali kadhalika kuwafungulia wananchi mashitaka. Ushahidi ni kesi ambayo tayari iko Mahakama ya Mwanzo Mwandiga Kigoma kati ya wakazi wanaogoma kuhama na mwekezaji *Agrisol*. Mwekezaji huyu amepewa hekta 10,000 eneo la Lugusu Kigoma huko huko. Eneo hili ndilo lilikuwa Kambi ya Wakimbizi na eneo hili ndilo limetengwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya.

Kwa mujibu wa Mbunge wa Kigoma Kusini ambaye eneo lenye mgogoro lipo ndani ya Jimbo analoliwakilisha, Mheshimiwa David Kafulila, alipozungumza na Watendaji wa Halmashauri walikiri kuwepo kwa shinikizo kutoka kwa ngazi ya juu na Watendaji husika wakimtaja Waziri Mkuu. Hii inatokana na mantiki ya kawaida tu kuwa uamuzi wa kumpa mwekezaji huyu eneo hili ni sawa na kuamua Makao Makuu ya Wilaya ya Uvinza yazungukwe na shamba la mwekezaji.

Hivyo, Mji ambao ni Makao Makuu hautatanuka kwa sababu utakuwa eneo dogo sana lililozungukwa na shamba. Nasema eneo dogo kwa sababu mpaka sasa haijafahamika Makao Makuu yatawekwa wapi wakati eneo lote kashapewa mwekezaji. Labda Serikali imwombe *Agrisol* eneo la kujenga Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya mkanganyiko huo, pia kuna tatizo la mahitaji ya ardhi. Wakazi wa eneo la jirani wanaotakiwa Uvinza na Mwamila wanahitaji kulima katika eneo hili, lakini wanazuiwa. Taarifa ya mahitaji ya eneo hili kwa wakulima wa kawaida ipo Ofisini kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. Mkuu wa Mkoa anakiri kuwa ni tatizo na kupendekeza kwamba labda watu walime kwa muda wakati mwekezaji hajafika. Hii ni aibu! Wakazi wa Mwamila walifanya jaribio la kutaka kulima mwaka huu, wakafukuzwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa *Agrisol* kupewa eneo haukuridhiwa na wanakijiji, Halmashauri na Wataalamu walishinikizwa, na isisitizwe kuwa uamuzi huu unakinzana na juhudi za Serikali yenyewe kusukuma wananchi katika kilimo, kwani Wilaya ya Uvinza hivi sasa Mbunge amekopa trekta nne ili kusukuma kilimo kwa sababu ya wakulima na wananchi kulimiwa kwa bei ya chini kuliko bei ya Serikali. Halmashauri awali ilikuwa na kituo chenye trekta mbili hapo Lugufu, kama Kituo cha Huduma za Matrekta ya Kilimo Kwanza. Pia Halmashauri imenunua trekta tano kwa ajili ya kusukuma kilimo Wilaya hii. Juhudi zote hizi ambazo ni matunda ya mkopo wa *SUMA JKT* inakwamishwa na uamuzi wa Serikali kuuza ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu ikaeleweka kwamba hakuna anayepinga umuhimu wa mwekezaji, lakini ni muhimu vilevile ikaeleweka kwamba hatutaweza kuendelea kama tukikabidhi kila kitu kwa wageni. Sote tunajua kwa namna gani dhahabu, almasi na tanzanite, zimetumika kujenga uchumi wa mabeberu. Hatuwezi kufanya makosa tena kwenye raslimali hii muhimu ya ardhi inayopanda thamani kwa kasi sana. Uchumi hauwezi kuachwa uendeshwe na watu wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua kutokana na uwekezaji wa Makampuni, uchumi wa Tanzania unarekodiwa kukua kwa 7%. Hiki ni kiasi kikubwa kinachoifanya nchi hii kuwa miongoni mwa nchi 20 kileleni kwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi duniani. Lakini wakati huo huo inasikitisha kuona nchi hii ni miongoni mwa nchi 20 duni duniani, maskini kabisa. Hii inatokana na ukweli kuwa kilimo kinachoajiri asilimia 70 ya Watanzania kimeachwa. Njia ya kuondokana kwenye mlinganyo huu ni ardhi, wakulima wadogo wagawiwe ardhi na wawezeshwe zana za kilimo na ufundi wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa Tanzania tukawa hatujafikia hali mbaya kama ilivyo kwa nchi nyingine, kwa mfano Liberia ambayo asilimia 30 ya ardhi yake imekabidhiwa kwa wakulima wakubwa wa nchi za Magharibi, hali kadhalika nchi ya Cambodia ambayo inakadiriwa kati ya asilimia 56 na asilimia 63 ya ardhi yake yote inayotumika kwa kilimo iko mikononi mwa Kampuni binafsi ya kigeni. Hivyo basi, Serikali ya Tanzania ina fursa ya kujipanga mapema kabla hali haijawa mbaya. Lazima kuwe na mjadala mpana wa Kitaifa ili tuweze kupata njia bora ya kusonga mbele. Hatutakuwa wa kwanza kufanya hivyo, jirani zetu wa Msumbiji wamefanya hivyo, hali kadhalika na nchi ya *Papua New Guinea. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kufanya maamuzi sasa. Maamuzi tutakayofanya sasa yatakuwa na athari chanya ama hasi kwa kizazi kijacho. Inakadiriwa ifikapo mwaka 2050 Watanzania tutakuwa milioni 150, kama leo ardhi yetu tunagawa kwa wageni kwa miaka 99, tunaweka akiba gani kwa kizazi kijacho? Nini usalama wa chakula na uchumi kwa Tanzania ya kesho?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa raslimali ardhi ndiyo urithi pekee wa asili wa Tanzania, kwa Mtanzania katika kujitafutia riziki na kuendelea na maisha yake;

Na kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka wakati ukubwa wa ardhi hauongezeki jambo ambalo linaonyesha dhahiri kwamba kuna hatari ya kiasi cha ardhi kilichopo kisitosheleze mahitaji halisi ya wananchi;

Na kwa kuwa kumekuwa na ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji hasa wa nje usiojali mahitaji ya ardhi kwa wananchi siku za mbeleni;

Na kwa kuwa imebainika kwamba uwekezaji wa ardhi unaofanywa na Makampuni ya nje haujawasaidia wananchi kwa maana ya fursa za ajira na upatikanaji wa chakula kwa kiwango kilichoahidiwa na Serikali na Makampuni hayo;

Na kwa kuwa ugawaji huu wa ardhi kwa wawekezaji unakwenda sambamba na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na wananchi waliokuwa katika maeneo hayo kupigwa, kuvunjiwa nyumba zao na kufukuzwa bila kulipwa fidia;

Na kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji linakiuka sheria za nchi ambazo zinataka wananchi waarifiwe mapema juu ya ugawaji huo wa ardhi na kushirikishwa kikamilifu ili waweze kufanya maamuzi sahihi kwa maendeleo yao, jambo ambalo halifanyiki;

Na kwa kuwa mikataba ya ugawaji wa ardhi inafanyika kwa usiri mkubwa sana, jambo ambalo linaashiria mazingira ya rushwa na kutia shaka kama maslahi ya nchi yanazingatiwa;

Na kwa kuwa Serikali inapata kodi kidogo sana kutokana na uwekezaji katika ardhi, yaani Sh. 200/= kwa hekta kwa mwaka na ikizingatiwa muda wa kukodisha ardhi kisheria ni miaka 99;

Na kwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanategemea ajira katika Sekta ya Kilimo ambacho msingi wake ni ardhi;

Na kwa kuwa, Ibara ya 63(2)(c) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasema kwamba: "Kwa madhumuni ya utakelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu na muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya kusimamia mpango huo na kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwepo kwa Sheria";

Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani, lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji na kwamba tathmini ya kina ifanyike ili kuweza kubaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za Vijiji kinyume na matakwa ya Sheria za Ardhi Na. 4 na Na. 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Mdee kwa hoja yake ya msingi, hoja ambayo inagusia mambo muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba mambo kadhaa, matatizo kadhaa na kero kadhaa kama anazoziainisha katika hoja yake, Serikali inazitambua na Wizara ya Ardhi tayari inashughulika nazo. Maana yake, kimsingi katika mambo yote anayoyaeleza ya wananchi kuwa wanawakuambatia wageni, wanawapeleka vijijini kinyume cha taratibu na sheria wakidai kwamba watawapatia ardhi, lazima tukiri kwamba kuna namna ya utapeli unaokuwa unaendelea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wizara ya Ardhi na ninaweza kusema kwamba Serikali tunafanya kazi ya kina ya kutoa elimu. Kwanza, naomba elimu hiyo ianzie ndani ya Bunge hili Tukufu. Sheria za Ardhi, kwanza ardhi ya Tanzania inatawaliwa na sheria kubwa mbili au niseme tatu.

Sheria namba nne ya mwaka 1999 Ardhi ya Kawaida, sheria namba tano ya mwaka 1999 Ardhi ya Vijiji na Sheria Mama, Sheria ya mwaka 1967 ya utoaji ardhi. Sheria hizi ni muhimu, lakini hapo hapo kuna sheria nyingine nyingi ambazo pia zipo katika himaya nzima ya utawala wa ardhi.

Sasa sisi tunachofanya chini ya Kamishna, hali halisi tuliyonayo ni kwamba lazima tutoe elimu kwamba, kwanza tuelewe tunapozungumza ardhi, Tanzania ina ardhi ya aina tatu kwa mujibu wa sheria.

Kuna ardhi za vijiji na hii ni asilimia 70 ya nchi yetu. Asilimia 70 ya nchi yetu iko chini ya ardhi ya vijiji. Ardhi ya Kijiji kusudi uipate kisheria au kihalali ni lazima sisi tuone kwamba

palikuwepo na Mkutano Mkuu wa Kijiji uliokuwa na akidi ambao ulikugawia ile ardhi. Sasa mimi naomba kwamba hili likieleweka, hoja na mambo ya msingi ambayo anayasema Mheshimiwa Mdee, tutayaelewa vizuri. *(Makofi)*

La pili, ardhi asilimia 28 ni ardhi za hifadhi. Hapa tunazungumzia misitu, mbuga za wanyama, maeneo oevu na kadhalika. Asilimia 28 ya ardhi Tanzania iko chini ya aina ile.

Mwisho, tuna ardhi ambayo tumezoea kusema kwamba ni *public land* ambayo ni ardhi za kawaida, yaani ardhi za Miji. Ardhi ambazo kimsingi zipo chini ya utawala wa Serikali ni 2% tu sasa hivi. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiria kwamba tunapotoa hoja, kwanza kuelewa kitu tunachokizungumza ni suala la msingi sana. Sasa kama nilivyosema, tabia iliyoibuka ya watu fulani kudai kwamba wamepewa ardhi, nikiri kwamba mimi hapa nimekabidhiwa kazi na viongozi wa Serikali, Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu. Mimi kazi yangu ni kusimamia ardhi. Hao watu ambao mnasema wamepewa ardhi, wamepewa na nani kama siyo mimi? Maana yake niseme kwamba, kisheria ardhi inagawiwa, kama unataka hati tuseme kwamba ukitoa hatimiliki za vijiji ambazo nazo zina uhuru wa kutoa ardhi isiyozidi ekari 50, kijiji kinaweza kikagawa ardhi isiyozidi ekari 50.

Kila Wilaya ina Kamati ya kugawa ardhi ya Wilaya, Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi wa Halmashauri, anakaa na Afisa Ardhi, Afisa Kilimo na Wajumbe wengine kama Madiwani. Kamati ile ndiyo inagawa ardhi isiyozidi ekari 500. Zikishavuka ekari 500, ardhi ile itagawiwa na Kamati ya Taifa ya kugawa ardhi, Kamati hii imeundwa kwa mujibu wa sheria, ni *statutory* na ina Wajumbe hususan Wajumbe wa Wizara ya Kilimo, Mifugo, Biashara, Maliasili na kadhalika.

Kwa hiyo, katika kuchangia hoja hiii ya msingi, niseme kwamba Mheshimiwa mwenzangu ambaye ni Waziri kivuli, Mheshimiwa Mdee, ungekuja tukateta nisingesimama kutoa hotuba hii hapa Bungeni, ingesaidia sana. Kwa sababu hali halisi tuliyonayo ndiyo hiyo sasa, tunakuja kwenye uwezo, yaani *capacity* ya kufanya *administration*. Sasa hivi Tanzania ina ukubwa wa *square metre* za mraba ni laki elfu tisa na arobaini na tano *square kilometre* za mraba. Ardhi yetu ni kubwa sana! Kati ya hizi, ni asilimia 10 tu zilizopimwa, lakini ardhi nyingine yote haijapimwa. Tulichofanikisha kupima, sasa hivi takribani mipaka ya vijiji inakaribia 12,000. Sasa mipaka yake imepimwa na imepimwa kwa sababu kwa kutumia *satellite* tumeweza kuweka mipaka ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda nichukue nafasi hii kwa ridhaa yako kuwaelezea wananchi wanaosikiliza, na ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba mkirudi nyumbani nisaidieni kuwaelezea wananchi kwamba hata angekuja nani, awe wa Waziri wa Ardhi au awe sijui nani, huwezi kwenda ukalazimisha Mkutano wa Kijiji kugawa ardhi yake. Yaani kama kuna mtu anayekwenda pale anadai kwamba ana madaraka ya kisheria kufanya hivyo, hakuna, ila Serikali inaweza ikatoa ardhi kama inahitaji chini ya Sheria ya Utoaji Ardhi ya mwaka 1967. Serikali inapolazimika kutoa ardhi, hapo sasa sheria ile inaipa mamlaka kutoa ardhi na ikitwaliwa kwa sheria ile, ni lazima ilipe fidia kwa bei ya soko. Kwa hiyo, hii ndiyo hali halisi. Sasa Wizara ya Ardhi, sisi kazi yetu ni nini? Kuongoza, kutoa elimu na mchakato huu unaendelea. Nadhani hili limeeleweka.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo la pili ambalo ni la msingi na ambalo Mheshimiwa Mdee analizungumzia ni wageni. Sasa nimefurahi sana kwamba na yeye anakiri kwamba tunahitaji wageni kutusaidia kuboresha tija ya ardhi yetu, yaani *productivity*. Maana yake hali halisi ni kwamba Taifa hili na Bara la Afrika kwa ujumla tunasema ni *net food importing,* yaani tunaagiza chakula kutoka nje, mwisho wa siku ukifanya *balance sheet* tunaagiza chakula kutoka nje,

yaani *net food importing country* pamoja na kuwa na ardhi hii kubwa; kwa maneno mengine kama meli zisipokuja na siyo salama sana katika Bahari ya Hindi na Maharamia wapo. Kwa mfano, wangezingira nchi hii, hapa kufa kwa njaa yaani ni *guarantee* kwa sababu bado hatujitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni aibu kwamba nchi yenye ardhi nzuri namna hii haijitoshelezi. Kusudi hili lifanyike na Mheshimiwa Mdee analizungumzia, ni lazima tukubali kuendeleza ardhi. Sasa kuendeleza ardhi maana yake nini? Kuendeleza ardhi ni kuweka miundombinu ya kilimo cha kisasa na miundombinu ya ufugaji wa kisasa. Sasa kama huna miundombinu hiyo, usahau! Ardhi haitakusaidia kitu chochote! Wakati wa njaa, kila mtu anahama. Kama hakuna chakula, hiyo ardhi yako unaiacha mwenyewe bila kufukuzwa na mtu wala kuporwa na yeyote, unakwenda mjini kutafuta mahali utakapopata chakula. Kwa hiyo, ni dhahama kabisa! *(Makofi)*

Sasa katika hali hiyo, Serikali ina mkakati ambao na Mheshimiwa Mdee nimeona kimsingi unaukubali kwamba ni lazima tuboreshe ardhi. Sasa wale wageni wana raslimali, *capital* na utaalamu kwa sababu sisi tuna ardhi ila wao wana fedha, lakini ni *capital* na wana *expertise* au utalaamu. Sasa sera ya Serikali ni kukutana katikati na ninadhani nimeelezea wakati wa bajeti kwamba Sera ya Serikali kuhusu ardhi ni *land for equity,* yaani sasa hivi Serikali itachukua asilimia au *shares* katika mashamba makubwa. Hiki ni kitu ambacho mchakato ndiyo unakamilika na wakati ukifika hata Bunge hili Tukufu mtakuja kuamua sasa, nani anachukua *share* gani? Hiyo ni juu yenu, lakini sisi kazi yetu ni kuamua kwamba ni *land for equity.* Mheshimiwa Rais amesharidhia sera hii tunayoifanyia kazi.

Sasa Mheshimiwa Mdee katika hoja yako unazungumzia Makampuni kadhaa, mojawapo ni *SEKAB* ya Sweeden. Kwanza kampuni ile haiko tena katika nchi hii. Kampuni ile imebadilika sasa hivi imeandikisha kampuni yake hapa ambayo ndiyo *Bagamoyo Equal Energy,* na kampuni ile imekubali kufanya *modal* yaani *pilot* katika sera mpya ya mashamba yatakayoitwa *The State Farms,* mashamba ya Serikali ya Kisasa ambapo Serikali inabaki na *shares* katika mashamba yale.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba, cha msingi hapa ni kwamba kwa kweli Serikali hii haijalala. Haya imeyaona na hakuna mtu atakayekubali kwamba ardhi itaporwa na wageni. Wakulima wakubwa sasa hivi, Bunge lako Tukufu ilizungumzwa humu humu kwamba kodi ya ardhi iko chini. Katika bajeti ya mwaka huu tumerekebisha viwango vya kodi, lakini utashangaa kuna watu wengine tayari wameshaanza kulalamika.

Sasa watu wanasema *you can't have your cake and eat it,* yaani huwezi kuwa na keki lakini hujaila, kama umeila imekwenda iko tumboni. Sasa hivi kwa ardhi za kilimo gharama imepandishwa, *land rent* imetoka shilingi 200 kwa heka imekuja 800 kwa heka. Sasa hilo ni ongezeko mara nne na huwezi kuweka *shock therapy* kwa sababu makampuni au wakulima pia lazima uwape nafasi. Tunaanza kwenda taratibu, lakini hatutakomea hapo, tuta-*introduce performance bond*, kama mwekezaji anachukua ardhi kulima na yeye kwanza atupe kidogo ziada tukae na fedha kiasi fulani, si unakwenda kuzalisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unakuta Serikali iko katika mikakati mikubwa ambayo ina maono makubwa na *principles* kubwa ambazo zitasaidia kufanya *complete transformation*. Ila tu pia nielezee kwamba unaposema Watanzania miaka 99, kama unataka watu wasituchezee ni lazima uwape muda wa kutosha kuendeleza hiyo ardhi. Ili kusudi ardhi iwe na tija *(productive)* unahitaji kuwekeza takribani kama Dola 2000 kwa kila heka milioni moja au milioni mbili, kusudi hapo uwe na maji, mifereji, *farm layout*, yaani una vyombo vya kisasa.

Kama mnavyojua, hali siyo hivyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hatuwezi kusema Watanzania watakaa kwenye ardhi milele. Wanetu, ndugu zetu watakaa kwenye ardhi milele. Kwa hiyo, ndiyo watakuwa wakulima wadogo wadogo. Tuachane na fikra za namna hiyo! Ili nchi iendelee lazima watu waache kuwa wakulima. Hiyo ndiyo inaitwa *economic transformation.* Watu wanatoka kwenye kilimo wanakwenda kwenye viwanda, wakitoka kwenye viwanda wanakwenda kwenye *services.* Wakulima wanabaki wadogo wadogo. Hiyo ndiyo *trajectory* ya *economic transformation*, yaani sasa wachache wanaobaki kwa mfano Marekani, jeuri yake ni nini? Ni mkulima wa kwanza duniani, lakini asilimia ya Wamarekani walio kwenye ardhi ni watu wangapi kwa namna ya kilimo? Ni asilimia tatu, kwa sababu wengine wameshatoka kwenye kilimo, wako kwenye sekta nyingine, kwenye *services.* Naomba hili nalo lieleweke. Sasa hii miaka inaweza kuwa 33, inaweza kuwa 66, inaweza kuwa 99 au inaweza kuwa chini ya hapo.

*Tanzania investment center* kwa utaratibu tulionao sasa hivi kabla ya *land for equity* kuanza tulikuwa tunapeleka Tanzania *investment centre.* Sasa hivi hakuna haja ile, maana yake Serikali inabaki kwenye yale mashamba. Sasa zile *shares* za Serikali ambazo tumeanzia kwamba asilimia 25 ni lazima ibaki kama *share* ya Serikali katika shamba, mapendekezo yapo yatajadiliwa, yataletwa hapa na ninyi pia mtayajadili kiasi gani kibaki Serikali Kuu, kiasi gani kibaki Halmashauri yenye shamba na kiasi gani kiende kwenye wanakijiji wenye shamba. Hayo yanajadilika. Pendekezo letu sisi ni kumi na tano, kwa tano, kwa tano. Sasa asilimia tano zile tunapendekeza ziuzwe kwa *stock exchange,* Watanzania nao wapate nafasi kushiriki katika mashamba haya kwa kuchangia fedha wale ambao wana fedha.

Mheshimiwa Spika, nimefafanua kwa kirefu kwa sababu hili suala ni muhimu sana na ningependa tulichukulie kwa ujumla wetu, *by partisan,* maana yake suala hili haliwezi kuwa na itikadi *(ideology)*. Hapa hakuna itikadi! Ardhi tunaihitaji wote. Hapa hakuna itikadi. Yaliyosemwa yamesemwa na Mheshimiwa Mdee tungekuwa tumekutana kabla hujaleta hayo, nadhani mambo yangebadilika.

Mheshimiwa Spika, bado sijamaliza hoja yangu na mimi niweze kuijadili. Kwa kuwa nimeelezea yale niliyoyaeleza kwamba matatizo yanatokana na watu kutotambua taratibu, na kwa kuwa Serikali sasa hivi kama nilivyoelezea, tayari jambo hili inalifanyia kazi, naomba kutoa hoja kwa kupendekeza chini ya Kanuni ya 57 na 58 kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, mtoa hoja anatambua umuhimu wa ardhi katika nyanja zote za uhai na uwepo wa Taifa hili hususan kilimo, ufugaji, makazi na kadhalika, ninapendekeza kufanya mapendekezo yafuatayo katika maazimio mawili anayopendekeza Bunge Tukufu liazimie kama ifuatavyo:-

Azimio la kwanza katika hoja ya Mheshimiwa Mdee napendekeza...

**SPIKA:** Ambayo inasemaje hoja yenyewe? Samahani Mheshimiwa Waziri, naomba utoe *notice* kwamba, kabla ya kufika mwisho utafanya marekebisho. Tutakuita wakati huo. Sasa hivi tuendelee na majadiliano. Kwa hiyo, umetoa hoja kwamba, utafanya marekebisho katika maazimio ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kama ni hivyo, basi nihitimishe kwa kusema kwamba, wakati ukifika utaniona, nitaomba kutoa hoja**.** Ahsante**.**

**SPIKA:** Sawasawa. Yaani yeye ametoa *notice* kwamba, wakati utakapofika kabla ya kufanya maamuzi ya maazimio haya, nitamwita huyu anayetaka kufanya mabadiliko kwanza,

atatoa badiliko analofanya, tutalizungumza kama tunalikubali, basi linabadilisha azimio la Mheshimiwa Mdee. Kama hatulikubali, basi linatoka, tunaendelea na azimio la huyu ambaye alileta hoja yake. Kwa hiyo, muwe makini katika eneo hilo.

Kwa hiyo, kuna *notice* ya kufanya mabadiliko katika azimio la Mheshimiwa Mdee. Mchangiaji mwingine! Mheshimiwa Machali! Ndiyo Mheshimiwa Joseph Machali, vipi!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, umechanganya majina kidogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimechanganya! Nimeandikiwa hapa, watakaojadili hoja ya Mheshimiwa Mdee ni Mheshimiwa Joseph Machali. Siyo?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wamenikosesha hawa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Halima James Mdee kwa kuwasilisha hoja nzuri ambayo hakika ukiiangalia inakusudia kuweza kuhakikisha kwamba changamoto mbalimbali ambazo zinalikabili Taifa letu kwenye Sekta ya Ardhi nchini, zinaweza zikatatuliwa, kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kama siyo kuondolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, leo ukipita katika maeneo mbalimbali kwa kusikia kwa kuambiwa na kuona, ni ukweli usiopingika kwamba Sekta ya Ardhi hapa nchini inakabiliwa na tatizo kubwa sana. Wazawa wa nchi yetu wanaonekana kupuuzwa na maslahi yao kutokuheshimiwa hususan haki ya kupata ardhi na kuweza kuitumia kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Taarifa ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Mbunge imezidisha kuonesha katika maeneo fulani fulani ya nchi yetu, lakini hali ni mbaya sana katika maeneo mbalimbali. Yako makampuni mengine ambayo pengine mtoa hoja hakuweza kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge, lakini ukiweza kumsikia Mbunge mmoja na akaamua kukueleza ni matatizo gani ambayo yanapatikana katika Majimbo ambayo wanatoka, hali inafedhehesha sana.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano. Kigoma, katika Wilaya ya Kasulu, haya ambayo ameyaeleza Mheshimiwa Halima Mdee yanajitokeza vilevile. Yapo maeneo ndani ya Jimbo la Kasulu Vijijini, Kampuni moja ya kutoka India ambayo imeonesha *interest* ya kutaka kuwekeza kwenye kilimo cha miwa na hatimaye baadaye waje kuzalisha sukari wamepewa ardhi kubwa, wananchi wanapiga kelele, hakuna suala la ushirikishwaji wa wananchi. Jambo hili ninalipinga binafsi kwa nguvu zote na Serikali tuseme kupitia kwa viongozi ambao wamepewa dhamana ya kuhakikisha kwamba ardhi inagawiwa kwa utaratibu ambao umewekwa, wanakiuka taratibu hizo na wanastahili kwa kweli kuweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ili kukomesha ukiritimba ambao umekuwa ukifanyika.

Mheshimiwa Spika, mnatueleza hapa, tumekuwa tunaimba kila siku, Sheria za Ardhi zipo, tena unazitaja Profesa umekuwa mtu wa kwanza kuweza kuzitaja hizo sheria kila siku hapa, sijui sheria namba ngapi, kifungu cha ngapi; utekelezaji wake uko wapi? Sheria hizo zinatusaidia nini sisi Watanzania? Kwa hiyo, suala la kuendelea kusema tuna sheria, tuna kanuni, na taratibu halafu waliopewa dhamana ya kuzisimamia wanazipuuza, wananchi wanapuuzwa halafu tunakuja hapa tunaendelea kuambiana maneno matamu matamu yale yale, wawekezaji

wanatoka huko wao wana mitaji, wana teknolojia, wata- *invest* vizuri, matokeo yake tutaweza kuondokana na tatizo la njaa. Tanzania hatuna njaa, njaa tuliyonayo ni ya kujitakia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu! Nikijaribu kunukuu baadhi ya maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ambaye ameweza kutoa hoja kwamba hekta zaidi ya milioni 203 zinaonekana kunyemelewa na mataifa ya mabeberu, miongoni mwa nchi ambazo zinaendelea. Hekta milioni nne zinakadiriwa kunyemelewa na nyingine huenda zimechukuliwa na hao watu ambao tunawaita wawekezaji ndani ya Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hekta milioni nne ni ardhi kubwa sana. Sasa naomba nijikite tu kuzungumzia hili suala la kuendelea kuwapuuza wananchi. Ardhi ya wananchi imekuwa inavamiwa na kuchukuliwa pasipo ushirikishwaji wa wananchi. *(Makofi)*

Ningependa tuunge mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge, Serikali ikubali kusitisha suala la kugawa ardhi kwa hawa watu mnaowaita wawekezaji wa kigeni, maana yake *concept* ya mwekezaji hapa nchini, tumeamua kuona wawekezaji ni wageni wa kutoka nje *as if* hapa nchini hatuna watu ambao wanaweza wakakopeshwa na benki zetu wakawa ni *investors* wakubwa na uchumi mkubwa ukaweza kubakia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii itakwisha lini? Tungependa kuona Serikali hii inatwambia kama hoja iliyokuwa inataka kutolewa na Mheshimiwa Waziri ni ya kutaka kupinga suala la kutokusimamisha ugawaji wa ardhi na hatimaye Serikali ikubali kwenda kufanya tathimini au kuundwa kwa Kamati maalum ya Bunge kwenda kufanya tathmini? Naomba niseme kwamba Serikali hii na Waziri hatakuwa na dhamira njema ya kuhakikisha kwamba matatizo ambayo yapo hapa nchini yanayohusiana na ardhi, hayana dhamira na nia njema ya kuona kwamba matatizo haya yanatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, imetolewa mifano mingi hapa na tumepata kusema Mkoani Kigoma ndani ya Jimbo la Kasulu Mjini kwamba wawekezaji wanaonekana pia kupewa nafasi ya kwanza kuliko wananchi ambao wanatoka katika maeneo hayo. Kwa mfano, itakumbukwa mwaka 2011 wakulima wa Wilaya ya Kasulu ambao wamekuwa wanalima katika mapori yaliyo katika vijiji vya kule Kavilankanda, Mvinza, Chenkenya na maeneo mengine wamekuwa wakilima kwa takribani zaidi ya miaka 20 wakiwa huko kwamba ni maeneo ya hifadhi kumbe kuna watu wamepita mlango wa nyuma wanajiita ni wawekezaji, wanataka kuanzisha vitalu vya uwindaji na kwamba hayo ni maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, yapo maswali mengi ya kujiuliza, hivi muda wote wakati watu hawa walipokuwa wanalima zaidi ya miaka 20, hawa Maafisa wa Maliasili, Ardhi na Mazingira ambao wanapatikana katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Wakuu wa Wilaya ambao wapo na wamekuwa wakibadilishwa kwa nyakati tofauti, hawakuona na kupata taarifa kwamba kuna wakulima ambao wanalima katika maeneo hayo? Serikali imewachukulia hatua gani? Wananchi wamepigwa, wamenyang'anywa raslimali zao, hata maelekezo na ushauri ambao ulitolewa na Serikali umesema kwamba Serikali inawaondoa wale watu na sasa wanawapatia ardhi mbadala. Suala hilo halikufanyika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 tumetoka hapa na aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii wakati huo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala ambaye alipata ajali mbaya katika wale Mawaziri waliopata ajali mapema mwaka huu.

**SPIKA:** Ajali inahusika nini na mchango wako? *(Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ni ajali ile ya wale Mawaziri ambao walionekana kwenda kinyume na utaratibu, wakapumzika kidogo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ooh, nilifikiri ni ajali ya gari! Ahsante umeeleweka. *(Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 baada ya Bunge kama hili ambalo tunaendelea nalo la mwezi Kumi na Moja...

**MJUMBE FULANI:** Ni ajali ya kisiasa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Naambiwa kwamba ni ajali ya kisiasa!

Mheshimiwa Spika, tulitoka na Mheshimiwa Waziri tukafuatana kwenda kuangalia tatizo hili la wakulima ambao wamekuwa wanahitaji ardhi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo ambayo wamekuwa wanaitumia na kulima huko kwa zaidi ya miaka 20, mwaka 2011 wanafukuzwa chini ya Mkuu wa Wilaya ya Kasulu aliyepo hivi sasa, Bwana Danhi Makanga, naomba nimtaje kwa sababu imefikia mahali wananchi wanaandika hata barua, ndiye ambaye amekuwa anachochea migogoro ya ardhi ndani ya Wilaya ya Kasulu na ziko barua mkitaka ushahidi nitazileta.

Mheshimiwa Spika, moja ya makubaliano chini ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utaalii ilikuwa ni kwamba, kwa kuwa wale wananchi wameondolewa kule, basi Serikali Mkoani Kigoma chini ya Mkuu wa Wilaya iratibu kuhakikisha wananchi hawa wanapatiwa ardhi mbadala kama fidia ya eneo lile. Tangu mwaka 2011 mpaka leo tumeanza msimu mwingine wa kilimo na niliuliza swali hapa wakati wa Bunge la Bajeti na Waziri wa Kilimo akasema atalishughulikia kwa kuwa naye anatoka Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba hakuna shughuli yoyote ambayo imefanyika na matokeo yake wakulima wale wameamua kwenda kule kwenye yale maeneo kulima, leo wanapigwa, wananyang'anywa baiskeli na kuomba rushwa ili kusudi waachiwe wanapokuwa wamekamatwa.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ni mambo ya ajabu sana na yanatia aibu, kichefuchefu, chini ya viongozi ambao mmewapatia dhamana, wakuu wa Wilaya wako pale, Wakurugenzi wako pale, Wakuu wa Idara ya Maliasili, Ardhi na Mazingira wako pale katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Kazi ni kusubiri watu wanakwenda, wakishawakuta wako mashambani wanakwenda kuwapiga halafu wawekezaji wanakuja, mnakwenda kuwapatia ardhi. Huu ubinadamu gani? Kuna sababu gani za kupinga hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge na kutaka kubatilisha baadhi ya mambo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameomba Bunge lako Tukufu liweze kuridhia?

Mheshimiwa Spika, naomba hata mama yangu Prof. Anna Tibaijuka ukubaliane na kila kitu ambacho kimezungumzwa na Mheshimiwa Mbunge. Kwenda kinyume na suala hili huwatakii mema Watanzania na wala huisaidii Serikali yako ya Chama cha Mapinduzi, badala yake Watanzania wanaona na wanatusikia kwamba ni kitu gani ambacho kimesemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kabisa tuweke pembeni masuala ya kuwakumbatia baadhi ya viongozi ambao sio waadilifu. Masuala mtambuka kama haya ambayo yanahusiana na ardhi, kama hatuwezi kuyashughulikia mapema iwezekanavyo, tunajiandalia bomu lingine linaloweza kusababisha machafuko. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mmmhhh!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kataeni! Huko kwenu kama hayapo, kwetu kule yapo, na mkae kimya, ni wakati wangu mimi nachangia. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, mbona unachanganya mambo? Zungumza hoja yako sisi tuielewe. Hawa wanaosema ni wa kwangu mimi. Eeh, zungumza, acha wanaosema shauri yao.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, waache tabia ya kuzomea, ndiyo ambao wanasababisha haya, kwa sababu siyo muda wao na hawana haki ya kunizomea wakati nachangia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali fuata utaratibu na amri yangu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, *message sent* na wamenisikia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo ukija hata kwenye masuala ya ugawaji wa viwanja ndani ya eneo la Kasulu Mjini ni matatizo na ninashangaa. Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wanauliza maswali hapa, wamekuwa wanalalamika, leo mmepewa nini? Waheshimiwa Wabunge ambao wanapingana na masuala haya wamepewa nini? Watu wanapigana, wanatishiana maisha kwa sababu ya ardhi; uzembe, mmewapa dhamana baadhi ya viongozi kwenda kusimamia mambo haya hawafanyi, halafu hapa mnakuja kusema vitu gani?

**SPIKA:** Naomba ukae kwanza. Mheshimiwa Machali inaonekana huna hoja, maana yake sasa unachanganya weee! *(Kicheko)*

Mimi nilielewa utachangia kikamilifu kuunga mkono hoja ya mtoa hoja na ukifika mwisho unasema unaomba kuunga mkono hoja. Sasa mbona mara unamsemea nani, mara wapi! Mheshimiwa Mdee hakusema hivyo katika hoja yake. Kwa hiyo, tafadhali mjielekeze kwenye hoja zilizowekwa hapa. Sasa malizia hotuba yako.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba naunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge na tunawajibika kuweza kuwa *serious* na kusemea mambo ambayo…

*(Hapa microphone ilizimwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya. Naomba mjadili hoja za Waheshimiwa, acheni habari zenu huko vijijini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kujadili hoja hii muhimu inayohusu ardhi ambayo ni muhimu hasa katika mustakabali wa Taifa letu na katika maslahi ya kizazi hiki na kizazi kijacho ambacho ni vijana wenzangu walionituma kuwawakilisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuna mambo ya msingi mtoa hoja ameyasema, nakubaliana nayo. Lakini pia na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa *statement* yake ambayo ameitoa, kuna vitu ambavyo nimepata ufafanuzi wa kina. Lakini pia mbali ya ufafanuzi wake, kuna mambo ya msingi ameyaongelea kwamba kuna sheria ngazi ya juu haiwezi kuingilia mamlaka ya vijiji, lakini kuna haja ya msingi ya kurekebisha sheria zetu kubadilisha mamlaka makubwa ambayo wamepewa Serikali ya vijiji kwa ukizingatia umuhimu

wa ardhi ya Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, nadhani hilo pia ni jambo la msingi sana kuangaliwa. Je, hizi Serikali zetu za *level* ya vijiji, wana uelewa wa kutosha katika masuala ya utoaji ardhi? Kwa sababu leo hii inafikia tunajadili hoja hii inawezekana kabisa tulichelewa kutoa elimu ya kutosha, ni jinsi gani taratibu zifuatwe katika suala zima la utoaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambayo yanalalamikiwa na mimi nakubaliana na mtoa hoja kwamba hatuwezi kukataa uwekezaji unaogusa ardhi, lakini pia hatuwezi tukaruhusu uwekezaji ambao hauna tija kwa Watanzania. Nakubaliana kabisa kwamba Tanzania tuna ardhi ya kutosha, lakini pia lazima tuwe na angalizo kwamba Mataifa ya wenzetu yanatamani ardhi yetu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia ni wawekezaji gani ambao ni wa dhati, wana nia ya kuwekeza kwa maslahi ya Watanzania. Lakini vilevile hata wale ambao hawana uwezo wa kuwekeza na wanatumia ardhi hii kupata mikopo Benki, ambapo kuna Watanzania ambao walikuwa wana uwezo huo, ni kiasi cha Serikali kuwawezesha wakapata fursa ya kupata mikopo na kuendeleza ile ardhi yao kwa maslahi ya kuendeleza kilimo cha kisasa na hata wao wenyewe pia kujipatia kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja ya kina kwa kweli ya kufanya tathmini ya utoaji ardhi kwa wawekezaji wetu wa ndani na wa nje ili kuona ni jinsi gani ambavyo huu uwekezaji tulioutoa mbali na changamoto zake umetunufaisha kiasi gani. Lakini pia ni kiasi gani uwekezaji ambao hauna tija umesababisha hasara kwa Taifa letu. Kwa hiyo, hivyo ni vitu vya msingi vya kuzingatia. Lakini pia napenda kupongeza Wizara ya Afrika Mashariki, mbali na kwamba tuliridhia Mkataba wa Afrika Mashariki, lakini nimepitia suala la ardhi; halipo! Hilo ni jambo la msingi sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kuna suala katika Mkataba wa Afrika Mashariki, suala la ardhi halijazungumzwa. Sasa hivi kuna upatikanaji wa ardhi kwa njia ya kinyemela. Wenzetu wageni wamekuwa wakija na kuingia kwa *gear* ya kuwaoa Watanzania au kuolewa na Watanzania, baadaye anapata fursa ya kupata ardhi, na baada ya muda kadhaa wanaachana na matokeo yake anayeathirika ni Mtanzania kunyang'anywa mali zake kwa sababu watagawana. Lakini lengo lake halikuwa mapenzi ya kweli. Lengo lake ilikuwa apate fursa ya kuingia nchini, apate fursa ya kumiliki ardhi na mwisho wa siku unakuja kuzuka mgogoro, wanagombana na Mtanzania anabaki hana lake. Kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi la kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia leo hii tunazungumzia migogoro hii kwa sababu ardhi yetu haijapimwa kwa kiasi kikubwa, na lenyewe hilo ni jambo la msingi. Kama ardhi ingekuwa imepimwa kwa kiasi kikubwa, na ardhi yenye rutuba, Watanzania wakapata na wakaweza kumilikishwa, leo hii tusingekuwa tunalumbana kwenye matatizo ya migogoro ya ardhi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri changamoto kubwa iliyokuwepo hapa ni kuhakikisha ardhi yetu inapimwa na kuhakikisha kiwango kile kile cha utoaji ardhi kwa wawekezaji wa nje na wa ndani ndiyo kiwe kiwango kile kile cha Mtanzania wa kawaida kumilikishwa ardhi yake. Ni jambo tu hapa la Serikali kuhakikisha tunawawezesha wakulima wetu wadogo wadogo kutumia ardhi yao kupata hati ya kuweza kupata mikopo na kuweza kufanya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kabisa kama leo hii Taifa letu tunategemea asilimia 70 ya Watanzania, wameajiriwa kwenye Sekta ya Kilimo, wakulima wetu wakiwezeshwa vya kutosha, nina uhakika kabisa wana uwezo wao wenyewe wa kuhakikisha wanalisha Tanzania, wanalisha Afrika Mashariki na hata bila ya kuwategemea wawekezaji wakubwa ambao wengi wao wanakuwa wanachengachenga kidogo. Hata juzi Mheshimiwa Chiza alikiri, kuna baadhi hata ya wawekezaji wameshindwa kuendeleza mashamba yao na yapo na Serikali imeyachukua. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuangalia kwa kina suala hili.

Mheshimiwa Spika, hao wawekezaji ambao wanakuja, wanachukua ardhi na wengi wao wameshindwa kuwalipa fidia Watanzania. Hii pia imekuwa ikileta malalamiko. Mtanzania kwa nia njema anampisha mwekezaji ardhi aweze kuendeleza, lakini ile fidia anayopewa na thamani ya ardhi ambayo ameitoa ni vitu viwili tofauti na haya malalamiko yako maeneo mengi. Sasa ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa kina suala hili. Vijana wa Tanzania, vijana wenzangu na wenyewe wanatakiwa kukuta ardhi yetu bado ikiwa na rutuba, wana changamoto ya ajira, wanahitaji kuwezeshwa vijana wa vijijini waweze kupewa ardhi na wenyewe wajikomboe na tatizo la ajira na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kulizungumzia suala hili ambalo ni nyeti.

Mheshimiwa Spika, aliyetoa hoja, yako mambo ya msingi, lakini vilevile majibu ya Waziri yana msingi. Katiba yetu inampa Rais mamlaka ya kusimamia masuala ya ardhi. Sasa nieleze ni wapi tunalo tatizo na nieleze tufanye nini katika kuondoka katika tatizo na tuepuke kutoa majibu rahisi kwa maswali magumu. Ni rahisi kutamka kama alivyosema Waziri, lakini hata angekuja malaika, masuala ya ardhi yamezungumzwa hata katika vitabu vitakatifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa busara za Baba wa Taifa alitamka: “Ili nchi iendelee inahitaji mambo manne; ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora.” Hayo mambo ni muhimu sana na watangulizi wa Taifa hili waliyasema. Sasa nitamke yale mazuri ambayo yamezungumzwa na aliyezungumza hasa aliyetoa hoja kwamba ni vizuri tukakaa chini tukatafakari na kuangalia mwenendo wa matumizi na ugawaji wa ardhi katika nchi yetu. Hilo ni busara na imetamkwa hata katika sera zetu na siasa yetu. Sasa tufanye nini? Mzungumzaji aliyezungumza alitamka kwa kifupi sana; ardhi hutawaliwa kwa misingi ya sera na sheria. Sera yetu ni nzuri kwamba ardhi ni yetu sote na tunampa Rais mamlaka ya kuitunza kwa niaba yetu Katiba na sera ndivyo inavyosema. Sasa tunakosea wapi? Wala siyo makosa, ni ku-*review* sheria zetu ili ardhi imilikiwe vizuri na itawaliwe vizuri kwa manufaa ya watu wote.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali na katika Azimio litakalotoka Serikalini, Serikali ikubali kuwekeza katika masuala ya ardhi. Tatizo kubwa linatokana na kwamba katika nchi hii, kama alivyosema Waziri eneo lililopimwa ni asilimia 10 tu, asilimia 90 haijapimwa. Katika nchi ya namna hiyo lazima upate mkoroganyo, mwenye nguvu atamnyang’anya asiye na nguvu. Sasa Serikali iwekeze.

Serikali iliamua, bahati nzuri nilipokuwa Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Babati na Wilaya ya Bariadi ziliwekwa katika mpango wa kupima matumizi bora ya ardhi, hatimaye kutoa hatimiliki za mila na wananchi waweze kupata haki ya kumiliki ardhi yao. Mpango huu hatuelewi umeishia wapi. Maana hata huko Babati kwenyewe taarifa za mwisho hazijatoka. Bariadi taarifa za mwisho hazijatoka na mpango huu ukiwa kwa nchi nzima nawahakikishia matatizo tunayosema hayatakuwepo. Maana tunachohitaji ni kuunda Benki ya Ardhi. Tuwe na Benki za Ardhi ijulikane Wilaya ina kiasi gani cha akiba ya ardhi kwa kuwekeza. Wilaya ina akiba gani ya ardhi kwa vijiji vyake na Wilaya ina ukubwa gani wa ardhi kwa mahitaji ya Serikali Kuu? Bila kuwekeza hapo, tutagombana.

Mheshimiwa Spika, jibu siyo kuwakataza wawekezaji. Duniani kote walioendelea ni wale waliokaribisha wawekezaji. Hakuna mitaji; tupate wapi mitaji kama hatukuwaleta wenzetu kutoka nje? Lakini tuwalete kwa utaratibu. Mimi nachelea sana kwenda kwa haraka kusema

naunga mkono hoja. Nasema tukubaliane, utaratibu mzuri uwekwe, Serikali iwekeze katika masuala ya ardhi, vijiji vipimwe, Benki za Ardhi zijulikane, ardhi ya kuwekeza ni ipi kwa wageni, ardhi ya kuwekeza ni ipi kwa wananchi na ardhi ipi itawekezwa katika viwanda na ardhi ipi itawekezwa katika mifugo na kadhalika. Bila hilo hatutapata majibu. Tutatafuta majibu rahisi kwa maswali magumu. Leo ukisema umkataze mwekezaji, unakataa kwa nguvu zipi?

Sawa ardhi ni yako, lakini Waziri amesema wewe kama una kipande chako cha ardhi na wewe unataka kuja kuwekeza, basi hii ardhi yangu na mimi ichukuliwe kama mtaji. Usiniondoe ukanifukuza ukaniweka pembeni wewe ukala matunda ya ardhi ile; ndicho Serikali inachotamka. Sasa litatekelezwa lini, hilo ndilo jambo. Tusiahirishe sana. Mambo haya ndiyo yanaleta kichefuchefu. Mimi naamini Waziri atakuja na tamko zuri la kiasi gani tutawekeza katika ardhi tuondokane na tatizo la ardhi ambayo kwa kweli mara nyingine tunaweza kufikiria inaporwa ambavyo inaweza isiwe kweli maana itaporwaje wakati tumegawiwa wote! Huyu mtu tumemwalika akaja sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kama alivyosema mzungumzaji aliyepita, naamini waliopewa mamlaka ya kugawa ardhi, uwezo ni mdogo na elimu ni ndogo. Kwa hiyo, tukubaliane kwamba mamlaka ya vijiji, ile sheria itamke na kwa haraka sana matumizi bora ya ardhi nchini yapimwe na mamlaka husika zipewe tujue ni ipi ardhi ya uwekezaji kwa wageni na ni ipi ardhi itakayotumika kwa ajili ya wananchi wetu na ni ipi ardhi itakayostumika kwa viwanda na uwekezaji mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni huo. Mimi siungi mkono hoja rejareja kama ilivyokuja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante. Mheshimiwa Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nampongeza aliyeleta hoja. Hoja ya ardhi ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Lakini pia na sisi humu ndani ni viongozi, tunalo jukumu kama Watanzania. Tuyaangalie mambo katika upana wake. Ukiliangalia tatizo tulilonalo Tanzania, la ardhi, nadhani tatizo ni moja tu. Ardhi yetu bado haijapimwa. Nimekuwa nasema na ukienda kwenye *Hansard* utaona nimesema kwamba ni vizuri sasa kama nchi na sisi viongozi tuiombe Serikali itafute fedha, ardhi yote nchi hii ipimwe. Ardhi kwa ajili ya kilimo ijulikane, ardhi kwa ajili ya ufugaji ijulikane, ardhi ambayo itakuwa ni *reserve* ijulikane, ardhi ya mtu mmoja mmoja kama una kiwanja chako uwe na hati, una shamba lako uwe na hati ili tujue ardhi iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, kama tumemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, ameeleza sheria tatu muhimu na namna unavyoweza kupata ardhi Tanzania, sheria hizi zinafuatwa. Sasa kama liko tatizo mimi nadhani turudi kwenye kuhakikisha ardhi yetu inapimwa kama nchi. Tukishajua ardhi tuliyonayo, tutajua sasa ardhi hii tumlete mwekezaji, ardhi hii hapana, ni kwa ajili ya vizazi vijavyo. Lakini unaona hapa kama walivyosema wenzangu, tunataka kutoa *solution* na jambo gumu kirahisi rahisi hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza rafiki yangu mmoja Mheshimiwa Machali ameeleza kwamba ardhi ya Kasulu inatakiwa kuchukuliwa na watu kulimwa miwa. Mimi nimeona aibu sana. Tulikuwa kwenye *RCC* wote, Mheshimiwa Zitto alikuwepo kwenye *RCC*, jambo hili limejadiliwa kwenye *RCC*, utaratibu umefuatwa, lakini zaidi ya hayo mbili ya tatu ya ardhi ile ni *outgrowers* ambao ni Watanzania na mpaka leo tunavyoongea mtu huyo wala hajapewa hati, bado utaratibu wa Kiserikali unaendelea. Leo tunakuja hapa kwa sababu kwenye TV tunaonekana, tuacheni! Mimi nasema ni uzalendo uchwara! Nchi hii haiwezi kuendeshwa kwa kupiga kelele. Tunasema wawekezaji wanakuja kutuibia ardhi, lakini jamani mimi nasikitika sana.

Mheshimiwa Rais wetu anatembea duniani kote kuleta wawekezaji, anaomba watu waje kulima, leo tunakuja tunasema kila anayekuja kulima anataka kutunyang'anya ardhi! Anatuibia ardhi!

Mheshimiwa Spika, hii hapana!

**TAARIFA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Taarifa!

**SPIKA:** Hebu, unasemaje Mheshimiwa Machali?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(8) kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anaendelea, kwamba katika kikao cha *RCC* anasema kwamba tulikuwepo na mimi nilikuwepo. Sikuwepo nilikuwa Jimboni kwangu nashughulikia matatizo haya haya ya migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, unapozungumza mambo haya, mimi najua kwamba Kasulu kuna matatizo makubwa sana.

**SPIKA:** Kumbe ulikosea mwenyewe kutokuhudhuria kikao cha maamuzi? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza taarifa yake siikubali. Lakini angalau amethibitisha kwamba *RCC* walijadili jambo hili ambalo kwangu ni jambo kubwa zaidi. Maana ungemsikiliza mwanzo ni kama vile jambo hili ni mtu tu amekwenda anawaambia watu ondokeni, naomba ardhi, mwondoke.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, Mheshimiwa Halima Mdee amesema vizuri sana, liko tatizo la ardhi. Mimi ningeomba Serikali ianze kuthamini upya ardhi hii, ipime upya ardhi hii, lakini pale ambapo nasema jamani hii habari kwamba kuna mtu anakuja kutunyang'anya, kutupora; kuna watu makuwadi, hapana! Hii siyo lugha hata siku moja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amesema Profesa Tibaijuka, njaa ikija, hata shamba ulilonalo utalikimbia.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Huu ndio ukweli, hatuwezi kusema tuna ardhi halafu kila mwaka tunasema tuna njaa. Litakuwa Taifa gani hili?

Mheshimiwa Spika, bado naamini hakuna Mtanzania ambaye amenyang'anywa ardhi yake, naamini yako maeneo ardhi ya kulima ni chache. Kwa hiyo, tufanye utaratibu ili watu wengine wapate maeneo mengi zaidi ya kulima. Ninachotaka kusema, narudia kwa kumalizia kwamba ningeomba Serikali iende kupima ardhi yetu ili tutambue ardhi tuliyonayo, benki tuliyonayo, tujue ardhi hii tunaleta mwekezaji, ardhi hii ni kwa ajili ya vizazi vijavyo, ardhi hii ni kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI**: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika hoja hii muhimu ambayo imeletwa na Mheshimiwa Mbunge, hoja inayohusu masuala ya ardhi ambayo inatugusa Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi wakati anatoa maelezo yake, yeye alisema kabisa kwamba sisi tunahitaji wawekezaji kwa sababu wawekezaji katika ardhi wanatuletea ajira, kwa sababu kutakuwa kuna viwanda vya usindikaji na vinginevyo. Lakini pia wawekezaji watatuongezea uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Lakini cha kusikitisha, Serikalia imekuwa ikitoa ardhi kwa wawekezaji ambao moja kwa moja kwa kweli hatuoni kama wanatuletea tija hiyo ambayo wao wanaielezea.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge wakati anatoa hoja yake aligusa kidogo katika maeneo ya Bonde la Mto Rufiji. Mimi nitolee mfano wa Rufiji kule kwetu, kuna Waturuki kule wamepewa ardhi takriban miaka zaidi ya mitano sasa. Ardhi ipatayo ekari 6,000 lakini mpaka leo hii ukienda pale eneo la kijiji cha Ikwiriri na Nyamwage pale katikati hakuna chochote kinachoendelea, isipokuwa inaleta mgogoro baina ya wananchi wa Rufiji ambao sasa wanatamani watumie ile ardhi, lakini ardhi inasemekana ipo kwa mwekezaji, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelezwa katika ardhi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia walikuwa Maafisa wa *RUBADA* baada ya migogoro baina ya wananchi na eneo la wawekezaji. *RUBADA* wanatuhakikishia wananchi wa Rufiji kwamba wale wawekezaji Waturuki walishapewa mpaka mkopo kutoka Serikalini kwa ajili ya kuendeleza ardhi ile. Lakini mpaka sasa pesa wamepata, na wananchi hakuna chochote walichonufaika kutoka kwenye ile ardhi ambayo ameichukua.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Waziri alikuwa anazungumzia hapa kwamba utaratibu wa Sheria uko wazi. Kwa mfano suala la kijiji wanaruhusiwa kutoa ardhi siyo zaidi ya ekari 50. Mimi nasikitika, kwa mfano kule kwangu katika Kata ya Umwe kuna muhtasari unaonyesha kwamba Mwana mmoja aliomba ardhi. Akapewa kwanza ekari 200, muhtasari wa kijiji unaonyesha hivyo. Lakini cha kusikitisha, Wilaya sasa imeleta barua kwamba huyu Bwana amepewa ardhi ya ekari 750. Sasa tunashangaa. Ina maana Maafisa Ardhi hawajui utaratibu au taratibu zinafuata kwa mtindo gani?

Kwa hiyo, inaonekana hapa kuna rushwa za waziwasi kabisa, kwamba Maafisa wetu wa Ardhi wanachukua pesa, wanachukua hongo kutoka kwa watu hawa ambao wanajiita wawekezaji, wanatoa ardhi ambayo sasa inaleta mgogoro baina ya wananchi na hao wawekezaji. Sasa mimi nashangaa, ekari 750 anapewa, lakini yeye aliomba ekari 200, muhtasari wenyewe wa kughushi, wamekwenda, wananchi wachache, akidi Mheshimiwa Waziri kasema inatakiwa itimie, akidi haijatimia; wamekwenda wananchi wachache, wengine wamewekwa majina, wametiliwa sahihi za dole gumba, wenyewe hawapo, hali ya kuwa wenyewe wanajua kusoma. Sasa mimi bado napata taabu kidogo.

Mheshimiwa Waziri naomba atueleze, tatizo ni nini? Ni Maafisa wetu wa Ardhi au ni hiyo elimu kwa hao watu wa vijijini ambao wanakubali wachache wao kupewa hizo biskuti, kupewa maji na kupitisha hizo *documents* za watu kupewa ardhi.

Pia suala ambalo watu wengi wamelizungumzia hapa, ni la upimaji. Hii imekuwa ni kero. Kama kweli Serikali ingejikita na naomba Serikali ijikite katika kupima ardhi. Wakipima ardhi hii ikajulikana kuwa ardhi ile ni ya wawekezaji, matumizi yao ya kawaida; kwa mfano, kule sasa hivi kuna mifugo, kule kila siku Mheshimiwa Waziri unasikia ni kero kwa sababu wafugaji hawapimiwi ardhi. Kwa hiyo, wafugaji hawajapimiwa ardhi. Kwa hiyo, wafugaji wameingia kwenye bonde, kwenye maeneo hayo hayo.

Kwanza mmeshawapa wawekezaji. Kwa mfano, kuna hawa *Euro Visitor* na hao wengine. Lakini hao sasa hivi wafugaji wamekwenda wanaingia, hakuna mpango bora wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ardhi inatolewa pasipokuwa na mpango. Sasa mimi nashangaa, hawa Maafisa Ardhi wanatoaje ardhi bila kuwa na ule mpango bora wa matumizi ya ardhi? Sasa Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie kwa kweli, imekuwa ni kero sana. Lakini pia kwa mfano ukienda Rufiji, kuna sehemu inaitwa Mkongo, kuna hawa watu wanaitwa *Euro – Visitors,* walipewa ardhi takribani ekari 6,000 ambayo ni nusu ya ardhi ya Kijiji. Sasa utaratibu uko wapi? Sasa kizazi kinaendelea kukua, watu wanahitaji kwa ajili ya matumizi ya kilimo, matumizi ya makazi na vitu vingine, mwekezaji kapewa ekari 6,000 huyo *Euro Visitor,* lakini mpaka sasa hivi hayupo, hakuna chochote kinachoendelea.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tatizo la ardhi ni kubwa na mimi naungana kabisa na Mheshimiwa Mbunge ambaye katoa hii hoja kuona sasa ipo haja ya makusudi kwamba huo mpango bora wa matumizi ya ardhi ufanyike, Serikali ijikite huko ili kuondoa matatizo, maana bila ya Serikali kujikita katika huo mpango wa matumizi bora ya ardhi, kila siku tutakuwa tunalalamika ardhi, ardhi, ardhi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa mfano ushirikishwaji wa wananchi, kule kwetu pia kuna sehemu ya Kilimani, takribani ekari 1,500 zimetolewa, wananchi hawajashirikishwa hata kidogo! Kwa hiyo, sasa hivi ni ugomvi baina ya wananchi na mwekezaji, wananchi hawajashirikishwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hiyo ni changamoto kubwa kama mwenyewe ulivyosema, unatakiwa uifanyie kazi zaidi kwa sababu Sheria Na. 4 na Na. 5 za Ardhi za mwaka 1999 zipo wazi, lakini zinakiukwa kwa makusudi.

Kwa hiyo suala la elimu pia linahitajika kama ulivyosema kwamba unajikita katika hilo eneo la kutoa elimu, hasa kwa sisi Waheshimiwa Wabunge na wengine kwa ajili ya vijijini kule kwenye *level* ya chini watu wajue nafasi yao na ukomo wao katika kutoa ardhi, maana inaonekana watu hawatambui mpaka sasa. Lakini pia hawa Maafisa Ardhi maana wao wanajifanya Miungu watu, kwa sababu sehemu nyingine mihutasari wanavijiji wanakataa lakini wao wanasema, sasa wanapitisha kwa kutumia zile Kamati za Ardhi za Wilaya ambazo zinakuwa zipo na Mkurugenzi. Kwa hiyo, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri aangalie zaidi hapo.

Pia, nataka Mheshimiwa Waziri aangalie kidogo hapo. Hii Sheria ya Ardhi inatakiwa iboreshwe. Kuna mambo ambayo yanatoa mwanya kwa hawa wawekezaji na hawa Maafisa kuitumia vibaya. Kwa hiyo, naomba hii Sheria ya Ardhi iangaliwe upya. Kuna hizi nafasi ambazo wao wanazitumia za kutoa ekari 50, ekari 500 mpaka ngapi, wao wanazitumia vizuri sana kwa kutambua kwamba wale watu ambao wako chini kule wengi wao hawana ule ufafamu. Kwa hiyo, wanaitumia nafasi hiyo hiyo ya udhaifu wa ufahamu wa watu ambao wako chini kutumia Sheria hizo Na 4 na Na. 5 kwa wao kupata maslahi.

Kwa hiyo, naomba hizi Sheria ziangaliwe vizuri, sehemu ambazo zinatoa mianya zibanwe vizuri sana ili kutotoa fursa kwa hawa Maafisa Ardhi na watu wengine kutumia vibaya hiyo nafasi.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu yalikuwa ni hayo machache tu, lakini naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Waziri uiangalie kwa uzito kwa sababu suala la ardhi ni rasilimali pekee iliyobakia kwa Watanzania na tusiruhusu rasilimali hii pekee ambayo inamnufaisha Mtanzania mnyonge kunyang'anywa, kupewa wawekezaji uchwara ambao

hawaendelezi na hawaleti tija inayokusudiwa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri aangalie hasa suala la upimaji wa ardhi katika maeneo yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niongee machache kuhusu hoja hii ya Waziri Kivuli, Mheshimiwa Halima Mdee. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, hakuna Mtanzania yoyote ambaye siku ya leo amesikiliza hii hoja ajitokeze kutokuunga mkono hoja hii. Labda kwa sababu tu tumezoea kukataa au kutokuunga mkono hoja hata bila ya kutafakari. Lakini ninasema hili kwa sababu ukiangalia nchi nzima, haijalishi ni Mkoa upi; nenda Bagamoyo, nenda Shinyanga, nenda Dar es Salaam, nenda Rukwa, nenda Sumbawanga, nenda Manyara, nenda popote, utakuta migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri tukubaliane tu kama Wawakilishi wa Watanzania ambao wametuleta mahali hapa. Tuna sababu ya kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mdee kwamba ushauri unaotolewa katika hoja hii ni jambo moja tu dogo sana, lakini ni la msingi kwamba, hebu tujitafakari tulipotoka. Tuna *database* ya ardhi tuliyonayo Tanzania? Ni wapi ambapo leo tunaweza tukasema huu ukanda ni wa kilimo, huu ni wa viwanda, huu ni wa wafugaji? Hakuna kitu kama hicho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hili kwa sababu ni kweli hata tulivyopitisha bajeti ya Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ilitengewa fedha chache kama unakumbuka. Nikasema hapa hapa kwamba hizo Shilingi bilioni 47 hazikutoshi chochote. Mheshimiwa Waziri ni vizuri ukarejea haya yote. Lengo la hoja hii ni kuijenga Wizara yako, ni kukuwezesha uweze kukabiliana na matatizo yote ambayo yanaikabili Wizara yako. Kwa hiyo, nafikiri mwisho wa hoja hii, Mheshimiwa Waziri ataliunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Chakula Duniani *(FAO),* wametumulikia nchi za Afrika taa nyekundu kwamba ifikapo mwaka 2015, nchi za Afrika tutakuwa na hali ya hatari ya njaa na wametushauri sana kwamba tuanze kulima mazao ambayo yanastahimili ukame kama mihogo, mtama na mazao mengine. Wamesema haya wanaonyesha kwamba ni jinsi gani Afrika tujipange na rasilimali hii nzuri ambayo Mungu ametujalia ya Ardhi. Tanzania tumejaliwa maeneo mazuri ya kilimo, lakini tunayatumiaje? Tunakwenda vipi kukabiliana na tatizo hili la njaa ambako wenzetu walioendelea wameshatumulika wametuambia mjiandae?

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni wakati muafaka wa kushauri Wizara hii na Mheshimiwa Waziri kwamba sasa kumbe tunahitaji kupanga hii ardhi. Tunapanga vipi? Tuwe na *data bank* na ni kweli hili halijatekelezwa sana kwa sababu ukienda kwenye ngazi za Halmashauri ambako Mheshimiwa Waziri ambaye anapewa hizi taarifa yeye mwenyewe ana zile taarifa. Mfano mzuri ni pale Babati. Taarifa ya *quarter* hii ni ardhi ngapi zimepimwa? Ambapo leo wapo kwenye Baraza la Madiwani wanajadili, waliopewa hatimiliki hawazidi watu wanne. Uone ni jinsi gani ambako hata upimaji umekwenda *slow* sana. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwenye hizo Halmashauri hakuna vitendea kazi. Hakuna vitendea kazi vya kuwasaidia wataaam wake na mara nyingi akisema kwamba Halmashauri zijitahidi, wanunue hivyo vifaa, lakini uwezo wanao?

Mheshimiwa Spika, zile pesa ambazo zinatumika au zinatoka katika upimaji wa maeneo, hizo pesa katika Serikali za Vijiji, zile pesa zote hazipelekwi kwenye ngazi za Halmashauri, zikaja kwenye mlolongo wa Wizara. Zile pesa zinaingia kwenye mifuko ya watu wachache, mtendaji na mwenyekiti. Ardhi ikiuzwa, ile asilimia inayopatikana inapita kwenye mfumo wa rushwa.

Ni vizuri tukaishauri Serikali kwa uwazi tu kwamba tukubaliane na hii hoja. Tunahitaji tupime ardhi yetu, tunahitaji tuwe na *data bank,* tunahitaji tupangilie ni maeneo gani ambayo tunakwenda kulima, ni maeneo gani ya viwanda na ni maeneo gani ya viwanja?

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha, hata yale maeneo ambayo ni *green belt* kwenye Halmashauri mbalimbali au maeneo mbalimbali katika nchi yetu, wataalam watu wa Mipango Miji wanathubutu hata kupima hayo maeneo yakawe maeneo ya makazi. Lakini yale maeneo ya mashamba yangeachwa yakaendelezwa, watu wakalima kilimo cha kisasa, wakazalisha. Hata hili suala la kuomba mahindi ya njaa kila mwisho wa mwaka lisingekuwepo, na nasidhani kama hii nchi tunaweza tukaendesha kwa *population* ya watu milioni 45 na kuendelea kwa kupeleka galoni mbili za mahindi kila mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji tujiangalie kama Taifa, lazima tukubaliane na hili. Ni wazo zuri na mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi au upande wa pili, wala msione aibu kuliunga mkono hili kwa sababu linagusa Majimbo yenu, linagusa Wilaya zenu, migogoro ya ardhi kwenu ipo na sijui kwanini tuone aibu katika hili wakati ukienda huko unakutana na migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la hatimiliki zile ambazo zimetolewa katika nchi yetu kwa muda mrefu sana, hati zile za miaka 99. Katika nchi hii kuna mashamba mengi sana ambayo hayaendelezwi. Mheshimiwa Waziri kupitia hoja hii, maana yake yeye anakwenda kupata *brake* ya kwenda kufanya kazi, kuangalia na anakuwa na *holiday* ya mwaka mzima, hapana kelele za ugawaji ardhi kule chini kwenye ngazi zote, watu wanatulia, hawahangaiki kugawa hizo ardhi. Unakwenda kuangalia zile hatimiliki kwa miaka hiyo *99, it is ok* wamemilikishwa, lakini twende kwenye *reality* ni wawekezaji wangapi wanaendeleza hayo mashamba?

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mzuri kwenye Mkoa wangu wa Manyara Wilaya ya Hanang' yale mashamba ya *NAFCO* yamemilikishwa kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi, wamefika kwenye yale mashamba ya ngano wanawakodishia wananchi, hawaendelezi wao, Mheshimiwa Waziri hili analijua yeye. Kuna sababu gani ya watu kutoka Kenya au nchi nyingine kwenda pale Hanang', mashamba makubwa yale wananchi walikuwa wanalima wananyang'anywa, yale mashamba sasa yule mwekezaji anaanza kuwapimia kidogo kidogo anavyojua yeye. Tuangalie na nafikiri ni jambo zuri sana na siku ya leo nilifarijika sana kwa sababu Mkoa wangu wa Manyara kila siku nikisimama ni migogoro hiyo ya ardhi.

Tuna mashamba mengi, Mheshimiwa Waziri unafahamu na ulishafika kwenye bonde la Kiru. Uliona ule mgogoro wa tangu mwaka 1998 kama sikosei. Miaka mingi sana mpaka leo! Lakini hakuna maamuzi yanachukuliwa. Mheshimiwa Waziri, nakukumbusha, ni jambo zuri sana hili siku ya leo na naomba tuliunge mkono na hususan kwa Mkoa wangu wa Manyara. Nakuomba uangalie yale mashamba yote na nitoe mfano wa shamba lingine. Ni shamba la *breweries,* lipo pale maeneo ya Singu, kama unakwenda Dareda. Lile shamba tangu ninakua naona baba zangu, mama zangu, wanakwenda kukodi pale, wanakodishiwa yale mashamba, ngano hailimwi tena, lakini wananchi wanakwenda kukodishwa, wanakwenda kulima mahindi, lakini hao hao *breweries* wao hawahangaiki kulima tena ngano. Kuna sababu gani ya wao kuendelea kumiliki hayo mashamba?

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kwa unyenyekevu sana kwamba hii nchi ni ya kwetu sote, Watanzania wametupa dhamana ya kuwawakilisha na tufanye maamuzi ya busara kuelekea mustakabali wa maisha yao. Nafikiri ardhi inagusa kila kitu. Nafikiri hatuna sababu ya kubishana juu ya hili, tunahitaji kama Taifa tuwe na *database*, tuwe na *data bank* ya ardhi tujue ni wapi tunakwenda kukodisha wawekezaji, tujue ni wapi Watanzania wanakwenda kulima,

tujue wapi wananchi hawa Watanzania wakajihifadhi wasijione wao ni manamba katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji ambao sasa hata imefikia hatua mnaona kuna migogoro ya ufugaji kila mara. Wafugaji hawana maeneo ya kufugia mifugo yao, lakini imefikia hatua Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji kwa sababu tu ya tamaa ya kupata fedha na kugawa viwanja, imefikia hata wafugaji katika nchi hii wamekosa mahali pa kulisha mifugo yao. Lakini sisi tunazungumza sana kuhusu kutunza mazingira, vyanzo vya maji, wasichunge kando kando za bahari, mito na vitu kama hivyo. Lakini angalia hawa wafugaji wametengewa maeneo gani. Nilikuwa naongea na Mwenyekiti mmoja wa Kijiji, anasema sasa Mheshimiwa hili shamba lote unaloliona, tunakwenda kupima viwanja. Nikamhoji mwenyekiti ni wapi wafugaji hawa wanakwenda kufuga ng'ombe wao? Lakini haya matatizo yote yanasababishwa na Watendaji wa Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali sasa iangalie, Watendaji wa Ardhi wa ngazi za Halmashauri mpaka ngazi za Vijiji wanasimamia hizo Sheria tatu ambazo Mheshimiwa Waziri humu ndani anasema kwamba Wabunge labda hatuna elimu. Wao wanasimamia?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikawaelimishe wale Watendaji ambao wanahusika moja kwa moja kuhakikisha kwamba ardhi zile zinagawanywa kwa busara, wale Watendaji Mheshimiwa Waziri Ofisi yako imepeleka elimu gani? Hizi Sheria tatu naamini kwamba kabla ya kuanza na Wabunge ambao wao wana hizo *copy* na wamezipitia, basi ile elimu iende kule kule chini moja kwa moja kwa hawa Watendaji na Wenyeviti wajue kabisa, tunahitaji kupanga ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, nirejee tu kwa kusema kwamba yeyote anayepinga hoja hii, mimi nachelea kusema labda sio Mtanzania. Kama ni Mtanzania ana sababu ya kuiunga mkono asilimia mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mbona unawakandamiza wenzio katika Kanuni ya kujadili. Waache wajadili kila mtu anavyoona. Acheni kusema kila mtu, ndiyo maana tunawanyamazieni. Kanuni ya 100 inasema wana uhuru wa kujadili wanavyoona inafaa. Kwa hiyo, habari ya kushawishi haipo. Baada ya hayo, nilisema nitamwita Mheshimiwa Wasira, atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi nitoe mawazo machache kuhusiana na suala hili. Nataka nikubaliane na wewe vilevile kwamba Utanzania wangu hauwezi kupimwa kwa kuunga au kutounga mkono hoja ya Mheshimiwa Mdee. Utanzania wangu ni zaidi ya hapo na uzalendo wangu ni zaidi ya hapo. Kwa hiyo, natoa mawazo tu lakini huwezi kusema kwa sababu una mawazo haya, basi Utanzania wako ni batili. Kwa kuanza, nataka kukataa hilo kabisa ili nisipimwe Utanzania wangu kwa mawazo nitakayosema.

Mheshimiwa Spika, nataka kujikita zaidi katika utaratibu. Sina haja hata kidogo ya kubisha kwamba kuna matatizo ya ugawaji wa ardhi au hayapo. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ametusaidia, ameeleza Sheria na Sheria ndiyo inayoweka utaratibu. Sasa kama utaratibu unavurugika, mahali tuna-a*ddress problem* ya kuvurugika kwa utaratibu; lakini Sheria ya Ardhi ya vijiji ambayo ndiyo asilimia 70 ya ardhi yote ya Tanzania imeweka utaratibu mgumu sana ambao ukifuatwa kama ulivyo katika ile Sheria, ni vigumu sana wanavijiji kuporwa Ardhi yao. Narudia kusema kwamba ni vigumu sana kama Sheria ile inafuatwa ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ile kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, inawapa baada ya kupima Kijiji na kuweka matumizi halisi ya Ardhi ndiyo Sheria ile inasema kijiji kinaweza kikatoa mpaka heka 50. Nami siwezi kuamini kuna mwekezaji kutoka nje anaweza kwenda kwenye Kijiji akataka kuwekeza fedha kwa kutoa ekari 50. *Actually* anaweza akajaribu kwa ekari 500 lakini hata 500 hawezi kuwekeza kama hapewi hati ya kumiliki ardhi hiyo. Hakuna mwekezaji wa nje ambaye anaweza kupewa ekari 500 na Halmashauri ya Wilaya akawekeza bila kupewa hati ya kumiliki ardhi ile. Ni vigumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani? Utaratibu ule unasema, ukitaka kuchukua ardhi ya Kijiji na kubadilisha matumizi kufanya ardhi ya Kijiji isiwe ardhi ya Kijiji, iwe ardhi ya kawaida chini ya Sheria ya Ardhi ya kawaida, mlolongo wake ni kwamba ni lazima upate kwanza kibali cha Wizara ya Ardhi, na Wizara ya Ardhi haiwezi kutoa hati ya kukumilikisha na kubadili matumizi ya ardhi ya kijiji mpaka ipate kibali cha *custodian* wa ardhi kwa mujibu wa Sheria ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inawezekana katika nchi yetu kuna mkoroganyo katika utaratibu, na inawezekana kuna watu hapa Tanzania wanamiliki ardhi bila hati. Ana *minute* tu ya Kijiji anasema ardhi hii ni yangu, lakini kwa *minute* ya Kijiji. Kama ni kwa *minute* ya Kijiji, huyo tunaweza kumwambia na tukawaelimisha wanakijiji kwamba hapa hakuna mtu aliye na ardhi, maana ardhi hii inamilikiwa kwa Sheria. Haimilikiwi kwa *minute* ya Kijiji kwasababu ukitaka kubadili matumizi ya ardhi ya Kijiji, kwanza Halmashauri ya Kijiji lazima ikubali na lazima Mkutano Mkuu wa Kijiji tena ukubali na waliohudhuria wote waweke saini kwenye muhtasari unaotaka kumpa huyo mtu ardhi na kubadili matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo utaratibu, baada ya *minute* hizo kufikishwa kwa Waziri wa Ardhi, Waziri wa Ardhi akiridhika, ninarudia; akiridhika kuwa zile *minutes* ni sawa, anazipeleka kwa Mheshimiwa Rais ili akubali ardhi ya Kijiji sasa iwe ardhi ya kawaida na ndipo Wizara ya Ardhi inapotoa hati ya kumiliki ardhi hiyo kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini *experience* tuliyonayo unaonyesha kwamba watu wanakwenda kwenye Kijiji, wanafika wanaitisha Mkutano, wakati mwingine na Mkutano haukutani, Waswahili wanapigwa rushwa kidogo wanaandika muhtasari tu. Wanaandika waliohudhuria, wanahudhuria mpaka waliokufa wanaorodheshwa kwa majina hata Marehemu wanaorodheshwa halafu unakuja na *signature* inawekwa kidole ambacho mwenyewe alishakufa, hizo *minutes* zinakwenda mpaka Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, mimi ninafanya kazi Ikulu Ofisi ya Rais. Kuna vituko hivyo vya mafaili na Mheshimiwa Rais ni *very careful* katika jambo hili. Tena haidhinishi kama kuna jambo gumu ambalo hafanyi, ni kukubali kwa haraka juu wa umilikaji wa ardhi ya Kijiji, kwa sababu ni sera ya nchi yetu na labda kwa Katiba ijayo lazima tufanye jambo la kikatiba kwamba ardhi ya wananchi wa kawaida ilindwe na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu haiwezekani! Sisi sio *industrial country,* sisi ni nchi ya kilimo na ni nchi ya wakulima wadogo. Tukienda na mfumo huo wa kumiliki ardhi kiholela, tutakuwa na *landless* katika nchi yetu. Lakini nilichotaka kusisitiza hapa ni kwamba, watu wanaosema wanamiliki ardhi ya vijiji huko, hawamiliki ardhi kisheria.

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kweli kwa Azimio la Mheshimiwa Halima Mdee, siyo kusitisha, nakubaliana naye juu ya kutathmini ili tuone kuwa hivi ni halali wewe unasema una ardhi? Je, una hati? Tupe hati tujue! Hilo tunaweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spik, lakini kwa mujibu wa sheria ya nchi hii na kwa Sera ya msingi Ardhi ya Vijiji, ni ardhi ya vijiji na haiwezi kubadilishwa matumizi yake mpaka wapate kibali kwa *custodian*

wa ardhi ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi nimeshuhudia uchunguzi unafanywa kabla Mheshimiwa Rais hajatoa uamuzi, wanakwenda mpaka kwenye Kijiji wanauliza, Mkutano tarehe hii mlihudhuria? Wanakijiji wenyewe wanasema sisi huu Mkutano hatujahudhuria na huyo mtu anayesema alipewa ardhi sisi hatumjui. Habari zikirudi, faili lile linaishia hapo hapo na ziko nyingi zilizoishia hapo hapo kutokana na utapeli ambao unatumika katika matumizi haya ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka kusema hapa kuwa elimu juu ya matumizi ya ardhi isiwe kazi ya Serikali au Wizara ya Ardhi. Nadhani sisi Wabunge wote tunao wajibu wa kujua Sheria ya Ardhi na vilevile tunao wajibu wa kuwaelimisha Watanzania wenzetu utaratibu wa kugawa hiyo ardhi ni nini, ili tuondokane na utapeli huu unaoweza kufanywa na watu wengine. Lakini lingine ambalo ningependa kulisema kabla dakika zangu hazijaisha, ni kwamba tusipingane sisi wenyewe katika mambo tunayoamua. Tulipoleta Mpango wa Maendeleo wa Mwaka jana, tuliainisha maeneo ambayo tulitaka kulima mpunga na kulima miwa kwa ajili ya kuongeza sukari na mchele ambayo ni mazao muhimu yanayotakiwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kama ardhi inayosemwa siyo ya Kijiji, ni ardhi ya kawaida, hiyo tukikataa watu wasilime, sasa tunasema nini hapa? Maana ni lazima tukubaliane, kama tumesema walime na hawanyang'anyi vijiji vile ardhi yao na kuwafanya wale wanakijiji wawe *landless* na hilo nalo tukikataa tutakuwa tunapingana wenyewe kwa wenyewe. Nadhani tukubaliane kwamba kuna ardhi ambayo ni *public,* ile inaweza ikapewa tena kwa *jointventure* na wenyeji, na tunaposema wawekezaji hatuzungumzi wageni peke yao, tunazungumza na wenyeji wa hapo vilevile. Hivi tutapata mashamba makubwa bila kuwa na wawekezaji wa ndani na wa nje kweli? Haiwezekani! Lakini tufikie hapo bila kuwafanya Watanzania wakulima wadogo kunyang'anywa ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo ninaweza kusema, lakini utaratibu wetu ni mgumu na hata wawekezaji wamekuwa wakilalamika kuwa hatuwezi kupata ardhi hii, mlolongo ni mrefu na mimi nadhani mlolongo kuendelea kuwa mrefu ni sawa kwa ajili ya mahitaji ya ardhi ya Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee na ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya ardhi haina itikadi. Ardhi haina Chama, ni ya wananchi wote, uwe mwanachama wa Chama chochote au usiwe na Chama, inawezekana Jimbo lolote kesho likawa la CCM ambalo ni la CHADEMA leo, au likawa la Chama chochote.

Serikali imeweka Sheria nzuri sana ya Ardhi. Wanaokiuka Sheria ya Ardhi ni sisi wenyewe na wananchi ndio wamepewa majukumu ya kutawala ardhi yao kama Sheria inavyosema. Bunge hili hatuna Mamlaka ya Ardhi ya Vijiji. Hakuna Waziri mwenye mamlaka ya ardhi ya Vijiji, wenye mamlaka ni wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni sisi ndiyo tunapindisha Sheria. Kwa hiyo, ardhi yoyote ambayo imechukuliwa kinyemela, ni viongozi ndio wako nyuma ya ajenda hiyo. Ni viongozi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna siku Mheshimiwa Rais alifanya ziara kule kwetu akazungumzia suala hili la ardhi, akasema, kama kuna ardhi yoyote ambayo imetolewa kinyemela bila Mikutano ya Wananchi, bila Mikutano Mikuu ya Wananchi, ambayo kwa udanganyifu ikachukuliwa kinyemela, leteni, niambieni nifute hiyo hatimiliki kama ipo. Mimi ndio nina dhamana ya kufuta hatimiliki yoyote. Kwa hiyo, hawa tunaowaita wawekezaji ndio wafanyabiashara ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano tu. Kuna mwekezaji mmoja aliwachukua watu wa Kijiji kimoja kule kwangu akawapeleka Dar es Salaam Serikali nzima ya Kijiji, tena kwa ndege, akaenda kuwalaza hoteli kubwa kubwa huko Dar es Salaam kwenda kuwaomba ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, wananchi wenyewe hasa Wamasai ambao hata hawajawahi kuona ndege, siku hiyo wakaingia ndani ya ndege. Siku hiyo wakapanda ndege na kupelekwa Dar es Salaam Serikali nzima ya Kijiji, pamoja na Mwenyekiti wao na Mtendaji wakaenda kutoa ardhi na mihuri wamekwenda nayo. Lakini waliporudi, tulikuja kuwaambia kuwa haiwezekani! Hiyo ardhi haitolewi! Tena wamewapa kila mmoja Sh. 200,000/=, wakarudi na ndege. Nikawaambia kuwa nyie mna bahati, kwa sababu mmekwenda kutalii, lakini ardhi haitolewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaambia ndugu zangu, Wabunge wenzangu, kila Mbunge awe mbogo katika eneo lake! Siyo kuja kuwa mbogo hapa! Ukiona wawekezaji wamekuja katika eneo lako bila wewe kujua, nenda kwa wananchi unaowawakilisha, Madiwani wote tukishikamana na Viongozi na Serikali za Vijiji na wananchi ndiyo wenye mamlaka ya kuwanyima wawekezaji ardhi yao, hata aletwe na Waziri yeyote, waambieni hakuna! Sasa hapo ndiyo tuna mamlaka. Wananchi ndiyo wenye mamlaka! *(Makofi)*

Kwa hiyo, nadhani hii ajenda tuirudishe vijijini kule, ni ajenda ya vijijini kule, kwa sababu ardhi ni ya nani? Ardhi ni ya kwetu. Kwa hiyo, nilitaka kusema machache kwamba ukali huu mnaoonyesha hapa, maana hii hoja ni ya kule vijijini, wanavijiji ndiyo watamaliza haya mambo ya ardhi. Kwa hiyo, naomba wale walanguzi wafanyabiashara wakubwa ni hawa watu wanaosemekana wawekezaji na nyinyi Serikali acheni kuwaabudu hawa wawekezaji. Mkiona wawekezaji wamekuja kutoka nje, mnaanza kutetemeka, mnasema ardhi iko wapi ya kuwapeleka wawekezeji? Mnatuambia tutafute *land bank;* iko wapi hiyo *land bank?* Itapatikana wapi? Mkija katika vijiji vyetu, hakuna ardhi mpaka wananchi wenyewe wakubali, na wananchi wenyewe wana akili.

Mheshimiwa Spika, wananchi nao wanataka kilimo kikubwa lakini wananchi wakubali ndiyo ardhi itolewe.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hizi dakika za mwisho na mimi nitoe ufafanuzi kuhusu mambo machache.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba ardhi ya Tanzania ni ya Watanzania wenyewe na ndiyo maana hata mwekezaji anapopewa ardhi anapewa kwa masharti maalum. Lakini ardhi, rasilimali ya msingi, kuiangalia hivi hivi haitaondoa njaa na wala haitamnufaisha mwananchi. Ardhi inaweza kumnufaisha mwananchi pale ambapo ana mtaji wa kuitumia na kuiendeleza. Kwa bahati mbaya, sisi Watanzania tulio wengi hatuna hiyo mitaji, lakini vilevile kutokuwa na mitaji, haitoshi kumpapatikia kila mwekezaji anayekuja hata kama ni tapeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji wawekezaji, lakini wawekezaji ambao kwa kweli wataleta mitaji na kwa kujua kuwa ardhi ni ya Watanzania, na kwa hiyo, wanapowekeza mitaji yao lazima Watanzania nao wanufaike na ardhi yao kama raslimali ya msingi. Mimi naliomba Bunge lako Tukufu kwamba, sisi tuwakatae wawekezaji matapeli na wasiokuwa na mitaji, lakini hatuwezi tukakataa wawekezaji wenye mitaji na ambao watafuata taratibu ambazo tumeziweka zikiwemo Sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, tukisema tuwakatae wawekezaji kwa ujumla wao, sidhani kama tutakuwa tunaifanyia haki nchi hii. Kuna mitaji mingi duniani, inayokuja Tanzania ni kidogo sana. Wawekezaji ambao sio mtapeli ambao ni dhahiri wanataka kwenda mahali ambapo Sera zao zinatabirika na Sheria zao zinaeleweka, kwa hiyo, jambo lililo muhimu hapa kwetu ni kuhakikisha kwamba Sera zetu zinatabirika kwa kutokuleta mabadiliko ambayo siyo ya uhakika. Nami nina hakika, hoja hii ya leo kama tukiipitisha itaidhihirisha Tanzania kuwa ni nchi ambayo haitabiriki na ndiyo maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kusema kwamba tufanyie mabadiliko hii hoja ya Mheshimiwa Halima kwa kuhakikisha kwamba ardhi yetu haiendi mikononi mwa wawekezaji matapeli wa ndani na wa nje, isipokuwa inakwenda kwa wale wenye mitaji na kwamba Watanzania watanufaika na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa kuhakikisha na kwa mujibu wa kuwa nchi ambayo inatabirika, tusifanye mabadiliko ambayo yataifanya nchi hii iogopwe na wawekezaji ambao ni dhahiri na badala yake watakuja wawekezaji matapeli, kwa sababu wao hawajali kuwa mnatabirika au hamtabiriki. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Waziri atakapoleta mabadiliko haya, ayakubali kwa manufaa ya nchi yetu kwa sababu tunahitaji mitaji. Akiba ya Watanzania ni kidogo, tunahitaji usalama wa chakula na uhakika wa chakula, tunahitaji kuondokana na umasikini. Kuangalia mapori, haitaondoa umasikini wala haitaleta uhakika na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuwaomba Watanzania kupitia Bunge lako kuwa, ni kazi yetu sisi kuona kuwa Sera na Sheria tunazoweka ni zile ambazo zitatuhakikishia wawekezaji ambao watakuja na mitaji na watakaoheshimu Sheria zetu. Ni kweli kabisa kuwa tuna Sheria mbili za Ardhi na tatu kwa mujibu wa Waziri. Lakini Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi Vijijini hasa Sheria ya Ardhi, ina Kanuni yake. Lakini Sheria ya Ardhi Vijijini nafikiri tunahitaji tuwe na Kanuni zinazoeleweka ili kila mmoja asiwe na tafsiri yake. Mwenyekiti wa Kijiji anatafsiri yake, Mbunge ana tafsiri yake, Mwananchi ana tafsiri yake, tuangalie na kuhakikisha kuwa upungufu uliopo unaondoka, lakini tusilete sura ya kutokutabirika kama nchi ili tupate mitaji hasa kwa wale ambao wanaaminika na wale ambao wataheshimu utaratibu wa nchi yetu na ambao watajua kuwa Ardhi ya Watanzania ni ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ardhi ya wawekezaji kule Hanang, mimi Mbunge na wananchi wa Hanang tumeshawaambia wawekezaji kwamba mwaka huu kama hawatalima ardhi yote waliopewa, tutashirikiana na vyombo vya Serikali vinavyohusika kuona kuwa wanarudisha ardhi ama walime. Lakini siyo hivyo tu, hatuwezi kukubali wawekezaji wanaokuja kungojea mvua kama wananchi ambao hawana mitaji. Tungependa na wao waanzishe umwagiliaji kusudi kilimo chetu kiwe na uhakika, walete viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya mazao ya kilimo na vilevile walete Vyuo ambavyo vitawafundisha wananchi kama *Cooperate Social Responsibility* ya wale wawekezaji ambao wanakuja Hanang na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe ufafanuzi huo. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho na nina hakika Mheshimiwa Halima atakuwa amekubaliana nami na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, analeta mabadiliko, na kwamba mimi na yeye tutakaa pamoja kuona kuwa kuna Sera nzuri hasa hii ya umiliki wa Watanzania wanapoingia ubia na wale wenye mitaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sina uhakika kama hoja ya Mheshimiwa Halima imegawiwa. Sina uhakika! Mmegawiwa?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** *Okay,* sawa ninashukuru.

Mheshimiwa Halima ameelezea mambo ambayo anayafahamu yote, lakini mwisho hoja yake inasema hivi: "Hivyo basi, naliomba Bunge liazimie kwamba zoezi la ugawaji ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kiko mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji."

La pili, Azimio hilo linasema kwamba: "Tathmini ya kina ifanyike kuweza kubaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za Vijiji kinyume na matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999."

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee. Kwa hiyo, tukirudi hapa napenda Mheshimiwa Halima Mdee ajibu haya waliosema wenzie, lakini wote mkizingatia hili. Mnaweza pia kutumia nafasi hii ya kupumzika Mheshimiwa Halima na Waziri na mwingine yeyote anayetaka kufanya marekebisho mkazungumze, kwa sababu wakati mwingine hapa tunabishana kitu ambacho wala siyo cha msingi sana, ni kwamba hoja hii ukiisoma ina mantiki yake. Sasa kama ni maneno maneno tu, mkaangalie. Kwa hiyo, wengine mliokuwa mnasema yote yale ndiyo kwenu huko kuko hivyo, lakini hatuwezi kumaliza humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, tunachotakiwa kufanya hapa ni Azimio hili tuliangalie vizuri. Hii ndiyo hoja ya Mheshimiwa, siyo vinginevyo. Mlivyokuwa mnasema mnajifurahisha wenyewe na mnakumbuka yale yaliyokuwa kwenu. Kwa hiyo, ninashawishi kabisa kama watakubaliana Serikali na Halima waangalie namna ya kufanya, tutapata maelezo baada ya mchana. Lakini nikirudi hapa niyameita Mheshimiwa Halima Mdee ata- *windup* hoja yake.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu cha jioni. Sasa kwa mujibu wa maelekezo ya Kiti, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Halima Mdee aweze kusimama mahali pake na aanze kuhitimisha hoja yake kwa kuzingatia michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Halima Mdee kwa Mujibu wa Kanuni, inasema utasimama mahali ulipo hapo hapo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja ili Bunge lako Tukufu liweze kupitisha Azimio kwa malengo ama mustakabali mpana wa ardhi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote waliochangia, wa pande zote mbili. Wamechangia kwa uzalendo mkubwa sana! Ninaamini uzalendo huu utatuwezesha kama Bunge, tutoke na kitu ambacho itakuwa ni historia kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ilivyo utamaduni, naomba nianze kwa kuwatambua waliochangia. Waliochangia kwa kusema kwanza ni Mheshimiwa Anna Tibaijuka,

Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Stephen M. Wassira, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Moses J. Machali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekili, lakini waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango yote ya Wabunge wa pande zote mbili imeonesha haja pana ya kufanya tathmini. Kuna Wabunge walichangia wakizungumzia umuhimu wa kuwa na *land bank.* Huwezi kuwa na *land bank* bila kufanya tathmini.

Vile vile Waheshimiwa Wabunge walizungumzia haja ya kila Wilaya kuweza kutambua kiasi gani cha ardhi tulichonacho ili kuweza kuamua sasa, katika hii ardhi tuliyonayo ipi inakwenda kwa wawekezaji, ipi inabaki kwa matumizi ya kijiji, na ipi inabaki kwa matumizi ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba Wabunge wote tumekiri uwepo wa tatizo la ardhi. Nafurahi zaidi nilivyoona pia na Serikali imekiri, kwa sababu mjadala huu umechangiwa na Mawaziri watatu kama sikosei; Waziri wa Ardhi, Waziri wa Mahusiano na Waziri wa Uwekezaji, na wote katika mazingira tofauti wamekiri kwamba, kwanza, kuna tatizo la matapeli wa ardhi; pili, kuna wawekezaji matapeli, lakini tatu kuna ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ardhi Na. 5 ya Vijiji ambayo inataka Mkutano Mkuu wa Kijiji utoe ekari 50 lakini wanakuja kugundua kwamba zinatolewa ekari zaidi ya 50.

Kwa hiyo, kimsingi, Serikali imekubaliana na hoja kwamba kuna tatizo kubwa sana na hiyo inapelekea haja ya kukubaliana na hoja hii ili tuweze kufika sehemu ambako tunataka kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuja hoja kubwa sana ya hofu, inawezekana hatutaki uwekezaji, na kama kuna mtu amesoma hotuba yangu vizuri, nimesema sipingi uwekezaji, lakini hoja ya msingi ni kwamba hawa wawekezaji wanapokwenda kwenye maeneo husika, kwanza utaratibu wa kupata ardhi unafuatwa, lakini ni kwa namna gani wananchi waliokuwa kwenye maeneo ambayo huo uwekezaji unataka kufanyika, wasipokwe ardhi yao na kugeuzwa manamba kwenye Kijiji chao. Kwa hiyo, hoja ya uwekezaji hakuna anayepinga, lakini uwekezaji uendane na kunufaisha wananchi. Ni lazima uendane na kunufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mmoja alinitumia ki-*note* akaniambia kwenye Jimbo lake la Kwela kuna Mwekezaji amepewa eneo, lakini katika eneo hilo alilopewa limejumuisha Vijiji saba. Kijiji cha Sikangu, Songambele, Azimio, Muungano, Musanda, na Kancha. Kwa hiyo, Mwekezaji amepewa eneo na inawezekana kwa tafsiri ya Serikali utaratibu ulifuatwa, lakini uwekezaji wa kuingiza wanavijiji wawe sehemu ya ardhi ya Mwekezaji, hiyo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwa mara ya kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Wassira, amesema Tanzania ni nchi ya Wakulima wadogo wadogo, hatuwezi kukwepa kwamba Tanzania ni nchi ya wakulima wadogo wadogo. Kwa hiyo, wakati tunajiandaa kwenda kwenye ukulima mpana utakaowajumuisha pia wakulima wadogo wadogo, ni lazima wakulima wadogo wadogo tuwatambue, lazima tuwawezeshe, waweze kufika kuwa wakulima wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema leo kwamba itafika mahali watabakia wakulima wawili watatu ama kumi wakubwa wanaohodhi maeneo halafu hawa wakulima wetu waende

wakafanye kazi za vibarua kwa sababu tu ya kutengeneza ajira, wakati tunajua mishahara inayolipwa kwenye haya mashamba ni kima cha chini; sasa hatutaki kutengeneza Taifa la vibarua. Vibarua wawepo, lakini pia itengenezwe *middle class* itakayotokana na wakulima hao hao kutokana na maeneo ambayo mwekezaji amekwenda. Ndiyo maana wenzetu wa India wameyafanya haya na Zambia wanaiga. India wamekubali kabisa katika kila *project* yoyote ya masuala ya ardhi, hata Uganda juzi, mradi wowote lazima uwe na umiliki wa wazawa.

Kwa hiyo, kama anakuja mwekezaji atakuwa na hisa yake, wenzetu wa India wanafanya asilimia 30 mwekezaji, asilimia 20 Serikali. Kwa hiyo, inaweza ikawa ama Serikali ya Mtaa ama Serikali Kuu kutegemea na utaratibu ambao tutaufanya. Asilimia 50 wanakijiji wa eneo lile ambao wanakuwa kama *out growers*, hii ndiyo Tanzania tunayoitaka ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema tunaitaka Tanzania ya kilimo wakati hata hao watu ambao wanazalisha kwenye hayo mashamba tukapata chakula cha kutosha, kumbe kuna Watanzania ambao hawatakuwa na uwezo hata wa kununua hivyo vyakula vinavyozalishwa. Kwa hiyo, kama tuna nia ya kujenga ambayo ninaamini tunayo kwa sababu Wabunge wengi sana tumechangia kwa uchungu, mimi nadhani tathmini ndiyo itatufikisha mahali muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki uwekezaji ugeuze Watanzania manamba. Katika hoja yangu, nimezungumza kwamba mbali ya wawekezaji wa nje, lakini pia wazawa wamepata ardhi kinyemela. Wakati Mheshimiwa Lekule anachangia alisema, sisi ndiyo sehemu ya tatizo. Mimi nina uhakika tukikubaliana leo, tukaenda tukafanya hiyo tathmini tunayotaka kuifanya, mtagundua ni miongoni mwetu wanasiasa tuna hekta elfu tano, elfu tano huko kwenye vijiji! Ni sisi ambao tumekiuka sheria!

Kwa hiyo, naomba hizi hoja mbili zikipitishwa zitasaidia kwa kiasi kikubwa sana, siyo kwa wawekezaji wa nje tu, bali kwa watu wa ndani, Watanzania ambao mbali na kupata ardhi kinyemela, ardhi kubwa hawaiendelezi wakati mamilioni ya Watanzania hawana ardhi. Tukipata taarifa sahihi, tutajipanga upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo wawekezaji, kuna tatizo lingine, wawekezaji wanapewa eneo kwa ajili ya kilimo, wanageuza matumizi. Amepewa eneo lina rutuba kubwa, malengo yakiwa wakazalishe. Tuna mifano Arumeru *Doll Estate*, eneo lina rutuba kapewa mwekezaji amekwenda kugeuza *Zoo* na Uwanja wa *Golf.* Hiyo ni kejeli kwa Watanzania ambao leo kupata kipande wa ardhi ni mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu Kawe kuna migogoro ya ardhi mikubwa sana. Masikini hawana vipande, lakini ukienda kule, Baba yangu Sumaye ana heka zake kule, Karamagi ana heka zake kule, mapori hayaendelezwi, wananchi wakivamia wanaambiwa wahalifu. Lakini nashukuru kitu kimoja; nimesikia kauli ya Waziri wa Uwekezaji, amesema Hanang' wamewapa mwaka mmoja wawekezaji wasioendeleza maeneo. Sasa na mimi mwaka huo mmoja kwa kuwa kauli imetoka kwa Waziri, maana yake ndiyo kauli ya Serikali, kwa mwaka huo mmoja kwa watu wenye maeneo kwenye Jimbo la Kawe makubwa wakati masikini wengi hawana maeneo; wakiwa hawajayaendeleza, habari itakuwa kama ya Hanang' na wala tusiulizane. Lakini siyo Kawe tu, ni kwa Majimbo ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu sisi tunawakilisha wananchi. Hapa Bungeni ni sehemu tu ya majadiliano, kwa hiyo, ni lazima tuangalie tulikotoka wametutuma nini. Kwa hiyo, hata kama Peramiho kuna mambo kama haya, nadhani tumeshapata kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni mabadiliko yaliyoletwa na Waziri wa Ardhi. Kwanza, nashukuru kwamba umekiri kuna tatizo na pili niseme kwamba nina tatizo dogo na hoja yako ambayo ninaamini kabisa hapa ndani tunaweza tukalipatia muafaka. Mheshimiwa Waziri anapendekeza kwamba, zoezi lisisitishwe, badala ya kusitisha iandikwe tathmini, ifanyike. Lakini Mheshimiwa Waziri anajua kwamba tukisema tunafanya tathmini wakati hakuna zuio lolote ambalo tumeliweka, tutatoka Tabora tutakwenda Arusha wakati tuko Arusha, Tabora yanafanyika mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu vile vile ikaeleweka kwamba, dhamira ya hoja siyo kwamba tusitishe moja kwa moja. Dhamira ya hoja ilikuwa tusitishe kwa muda. Kwa hiyo, tunaweza tukajipangia kwamba miezi miwili hatutagawa maeneo Tanzania kwa watu wapya mpaka pale tathmini ya kina tutakapoweza kuifanya. Hiyo ndiyo ilikuwa dhana ya hoja. Nashukuru kwamba hiki ambacho nilikuwa nakizungumza hapa, nilipotoka nje nikapata simu kutoka kwa Wabunge wa Mkoa wa Tanga, wanasema kwenye *RCC* yao wamekubaliana kimsingi kwa sababu ya ongezeko kubwa sana la *land grab* wasifanye mgawo wowote ama utaratibu wowote ama *negotiation* zozote zinazohusiana na ardhi mpaka tathmini yao ya muda ambao wamejiwekea wafanye, wajue ardhi ipo kwa nani, kwa kiwango gani ili waweze kujipanga upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba hoja ya kusitisha tunaweza tukaiweka iwe ni hoja ya kusitisha kwa muda, iwe ni miezi sita, iwe mwaka, iwe miaka miwili, lakini hatutaki tuende mbali huko, kwa sababu ikiwa miaka mingi zaidi na ninyi ambao mnapenda wawekezaji waje, inawezekana mkapata athari. Kwa hiyo, tutafuta utaratibu ambao tutakaa katikati na kukubaliana. Tunajua kwamba mfanyakazi akifanya kosa; nilipewa mfano na Mwalimu wangu kwamba leo Mkurugenzi akifanya kosa, ama mtumishi mwingine yeyote, ili uchunguzi uwe huru na kuweza kuleta matunda sahihi, anaambiwa kaa pembeni. Siyo! Sasa kwenye hili la ardhi, wakati tunawachunguza hawa watu, wakati huo huo tunaruhusu virusi viingie, tutapata ukweli kwa kiwango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru kwa mabadiliko, lakini mabadiliko yazingatie hayo ambayo nimeyazungumza. Vilevile mabadiliko yazingatie muda, lakini zaidi mabadiliko yatambue kwamba, kwa kuwa hiki ni chombo cha wawakilishi, taarifa, ama *findings* zozote zitakazopatikana kwenye hiyo tathmini, lazima ziletwe Bungeni ndani ya muda ambao tutakubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu hii nia ambayo tumeionyesha tokea mwanzo, tuifanyie kazi. Ni muhimu wananchi wa Lubufu ambao Makao Makuu yao ya Wilaya yamepewa kwa mgeni, Makao Makuu yao ya Wilaya mpaka sasa hatujui mustakabali ukoje. *(Makofi)*

Upatikanaji wa Makao Makuu ya Wilaya unategemea Serikali iende ikapiga magoti kwa mwekezaji, beberu kutoka Ulaya, hatuwezi kuruhusu! Lazima tujibu ama lazima tutoe tumaini kwa Watanzania, na ninaamini kabisa Bunge letu la leo litafanya hivyo. Hatutaki kinachotokea Zimbabwe sasa, kinachotokea Afrika Kusini sasa kitokee Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nafasi tuliyonayo tukipitisha haya Maazimio na ni muhimu tukapitisha Maazimio tukawa tumetatua tatizo na tutatatua tatizo kama Azimio ambalo tunapitisha leo litatamka kabisa kwamba, kuanzia sasa tunasitisha kwa muda fulani, tufanye tathmini fulani, tuje tuione tathmini, tusonge mbele. Tusipofanya hivyo, tutakuwa tumetwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi halina itikadi. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa. Watanzania wanatuangalia, leo tuonyeshe Utaifa kwanza, itikadi baadaye. Utaifa kwanza tutauonyesha kwa kukubaliana mapendekezo ambayo yatakuwa na nia ya kulitatua tatizo kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane katika hili. Tumeungana tokea tunatoa hoja mpaka kwenye michango yetu, ardhi ya sasa ni nyeti na duni. Ni jukumu letu kutumia fursa hiyo ya unyeti wa ardhi na kuwatumia hao wadau ambao mnasema wana fedha, wawekezaji, ili uwekezaji wao wa fedha uendane sambamba na thamani yetu ya ardhi ili Tanzania kama nchi, ili Wanavijiji wanaokaa kwenye hizo ardhi wawe na *equal share*. Suala la mwekezaji kupata *share* kubwa kuliko mzalendo, haliwezi kuvumilika. Kwa hiyo, nisisitize tu kwamba naomba Wabunge wakubali mapendekezo bila mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Waheshimiwa Wabunge. Mtoa hoja amehitimisha hoja yake kwa kutoa hoja na ameungwa mkono. Kama mlivyopata taarifa ya tangazo la asubuhi, tumeshapokea hoja ya kufanya marekebisho katika hoja hiyo ya msingi na taarifa hiyo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri na kwa mujibu wa Kanuni, sasa namwita Mheshimiwa Waziri aweze sasa kuwasilisha hoja hiyo ya mabadiliko katika hoja ya msingi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 57 na 58 za Kanuni za kudumu za Bunge toleo la 2007, naomba kutoa hoja ya kutaka kufanya marekebisho na mabadiliko katika hoja ya Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge juu ya kusitisha ugawaji wa ardhi hadi tathmini itakapofanyika kujua kiasi cha ardhi kilichoko mikononi mwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mtoa hoja ametambua umuhimu wa ardhi katika Nyanja zote za uhai na uwepo wa Taifa hususan kilimo, ufugaji, makazi, na kadhalika, ninapendekeza kufanya mabadiliko yafuatayo katika Maazimio mawili yanayopendekezwa Bunge liazimie kama ifuatavyo:-

Katika Azimio la kwanza la Mheshimiwa Mdee ukurasa wa 15 kuondoa maneno “lisitishwe hadi hapo”…

**MWENYEKITI**: Ukurasa wa 12 Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu ni ukurasa wa 15, katika kitabu cha hoja binafsi za Wabunge kilichotolewa leo kama mnacho, naona ni ukurasa wa 15. Azimio la kwanza linapendekeza kuondoa maneno “lisitishwe hadi hapo” na badala yake kuweka maneno “lifanyiwe tathmini”; na kuondoa neno “itakapofanyika” na badala yake kuweka neno “ ili”. Kwa hiyo, Azimio hili litasomeka kama ifuatavyo:-

“Kwamba zoezi la ugawaji ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani lifanyiwe tathmini ya kina ili kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la pili, ukurasa huo huo wa 15, napendekeza kuondoa maneno yanayosema, “ya kina ifanyike kuweza kubaini” na badala yake kuweka

“itakayofanyika ibaini”. Kwa hiyo, Azimio hili la pili litakuwa kwamba “tathmini itakayofanyika ibaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za Vijiji kinyume na matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kazi yangu iliyobaki ni kuhoji kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni, mtoa hoja ameshapata nafasi ya kutoa hoja yake, wachangiaji wameshapata nafasi ya kuchangia na baada ya mchango wao kukamilika, mtoa hoja ametoa nafasi sasa ya kujibu zile hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge. Sasa baada ya zoezi hilo, sasa ni hatua ya kuhitimishwa hoja hii na uhitimishaji wa hoja sasa itakuwa ni ku...

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Sendeka?

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua unaelekea kwenye kuhitimisha kwa mujibu wa Kanuni, lakini nilikuwa nafikiri kwamba kwa mujibu wa Kanuni pia kwamba ningeweza kuunga mkono pendekezo, siyo kwa kusimama kama tulivyofanya kuruhusu kuunga mkono hoja aliyotoa Mheshimiwa Anna Kajumulo Tibaijuka, kwamba msingi wa hoja hiyo ambayo na mimi nataka kuendelea kulishawishi Bunge liuone ukweli wenyewe ni kwamba kimsingi hoja ya mtoa hoja Mheshimiwa Halima Mdee ni ya msingi, ila inahitaji kutambuliwa jambo moja, unaposema kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sendeka, naomba kwanza uketi.

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Sawa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni, sasa tutakachokifanya kwanza ni kuhoji kile ambacho kimeletwa na Mheshimiwa Waziri hapa. Nitawapa nafasi Waheshimiwa Wabunge, maana yake lazima tuelewane kabla hatujahitimisha hii hoja, wala msiwe na wasiwasi. Ngoja tu nitawapa wote nafasi, mtaeleza kile ambacho kila mtu anakifikiria, halafu mimi nitafanya maamuzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Sendeka wewe unachokisema ni kwamba baada ya hoja hii kutolewa na Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa imeungwa mkono inapaswa angalau wale waliounga mkono wachangie maneno mawili, matatu kuona namna gani wanaiunga mkono.

Sasa bado sijatoa *ruling* hiyo. Ngoja nisikilize kwanza wale Waheshimiwa Wabunge wote waliosimama ili tuweze kuhitimisha kwa utaratibu unaofaa. Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami naomba mwongozo wako kuhusu hatua inayofuata. Kanuni ya 57(5), kwanza fasili ya nne inakataza mabadiliko yoyote ambayo yanapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa na hoja

ya msingi ya Mheshimiwa Halima Mdee. Kama nimeielewa sawa sawa ni kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji lisimamishwe mpaka tathmini itakapofanyika ya kubaini hayo ambayo yamesemwa katika Azimio na mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri ni kuruhusu ugawaji wa ardhi kuendelea, lakini tathmini ifanyike. Kwa maoni yangu, hiyo inapingana moja kwa moja na hoja ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ya pili, iko kwenye Kanuni ya 57(5) kwamba inataka kuwe na mjadala, hayo marekebisho lazima yajadiliwe. Hiyo fasili ya tano inasema: "Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kutoa maneno fulani na kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kufanya mabadiliko unaweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yanayopendekezwa yaondolewe na maneno ambayo yanapendekezwa yaingizwe." Kwa hiyo, hili pendekezo la kuondoa maneno na kuingiza mengine lenyewe linahitaji lijadiliwe kwa mujibu wa Kanuni hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, fasili ya sita, vile vile isisitiza kwamba lazima kuwe na mjadala. Iwapo hoja inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno, mjadala utahusu tu uondoaji na uingizaji wa maneno mapya kadri itakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako ili tunapofanya maamuzi ya hizi hoja mbili, twende vile vile sambamba na Kanuni za Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Tundu Lissu. Unajua Waheshimiwa Wabunge, nilichokifanya, kwa mfano kwa Mheshimiwa Sendeka, ndiyo maana nimemwambia nafahamu alikuwa ana hoja ya kimsingi ya fasili ile ya tano ya kwamba kwa sababu hoja imeshaungwa mkono ni lazima ijadiliwe na huko ndiko nilikokuwa naelekea. Mheshimiwa Sendeka tusingefika kwenye kuhoji kabla ya hapo.

Kwa hiyo, hiyo najibu pamoja na mwongozo wa Mheshimiwa Tundu Lissu katika maeneo yale mawili. Lakini katika eneo lile la kwanza unalosema, badiliko lolote halitaruhusiwa kama kwa maoni ya Spika linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa. Mheshimiwa Tundu Lissu ilikupasa uingie kabisa moja kwa moja kwenye ile kanuni ya 57(1) pale inaelezea namna gani utaratibu wa kubadili hoja. Kwa sababu ile ya kwanza inakwambia hoja imeshatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine, kuondoa maneno fulani bila kuongeza maneno mengine ama kuingiza au kuongeza maneo mapya.

Kwa hiyo, unaona kabisa kwamba alichokifanya Mheshimiwa Waziri, anasimamia pia vizuri kwenye Kanuni hii na ukiangalia *logic* ya Mheshimiwa Waziri habadilishi msingi wake wa hoja, lakini amesimama kwenye ile Kanuni ya 57 akizingatia hivyo vifungu vidogo nilivyovisema na ameleta na halafu inaendelea kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu ule ukurasa wa 36 bado unaendelea kum-*guide* yule anayeleta mabadiliko kwamba kabla ya kutoa hoja hiyo, mtoa hoja atamkabidhi Katibu maandishi yenye saini yake na yanayoonyesha mabadiliko anayotaka yafanywe.

Kwa hiyo, hapa nilishapokea na tangazo tulishalipokea toka asubuhi na mnaona Waheshimiwa Wabunge wote tulishakabidhiwa hilo kusudio na namna ya kufanyiwa mabadiliko. Tayari tumeshampa Mheshimiwa Waziri nafasi ya kutueleza ni maeno gani anayokusudia kutufanyia mabadiliko.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Waziri yuko sahihi kabisa kwa utaratibu alioutumia wa Kinanuni na badiliko hili aliloleta hapa limesimama vizuri kimsingi kwa utaratibu wa Kikanuni. Hatua nyingine sasa zitafuata baada ya haya yote ambayo hasa yaliyotolewa na Mheshimiwa Sendeka pamoja na wewe mwenyewe yatakapokuwa yamemalizika. Halima Mdee?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli yako, ina maana sasa tunaelekea kujadiliana mabadiliko yaliyopendekezwa na Mheshimiwa Waziri. Kwa kauli yako. Kama ni hivyo, sina nyongeza, majadiliano nadhani yangeendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja hii ilipotolewa na Mheshimiwa Waziri niliwaona Wabunge kadhaa wamesimama ili kuweza kuiunga mkono ama kujenga hoja katika hoja hiyo ya Waziri. Nilikuona Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kimsingi nilikuwa naokoa muda wa kurejea vifungu vile ukizingatia kwamba uzoefu wa Bunge hili limenifikisha mahali pa kuelewa Kanuni. Sasa naomba nitumie nafasi hii kuunga mkono hoja ya Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka ya kuondoa maneno aliyopendekeza na msingi wake ni huu, kwamba pendekeza la mtoa hoja linasema kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji.

Unapozungumza habari ya kusitisha ugawaji wa ardhi ili kwanza ufanye tathmini, kwanza Bunge hili linajua kwamba kufanya tathmini ya ardhi ya nchi nchi nzima ni fedha na muda. Kwa hiyo, unahitaji muda, unahitaji fedha. Bunge hili halijatenga fedha ya kufanya tathmini ya masuala hayo ya ardhi kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ugawaji wa ardhi ya Tanzania uko kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa an Bunge hili. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 55(9) kama Bunge hili litabariki, maana yake litakuwa limepitisha Azimio litakalokuwa limekiuka Kanuni ya 55(9) ambayo kimsingi hoja nzima kama ingelikuwa siyo busara ya Spika, ilipaswa iwe imeondolewa, maana inakiuka Sheria ambayo ipo. Kwa sababu ugawaji wa ardhi una mamlaka mbalimbali.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba nadhani Bunge hili halijatenga fedha, na unahitaji muda! Ni gharama, ni kinyume cha Kanuni ya 55(9)!

Naomba niungane na Mheshimiwa Prof. Tibaijuka kwamba tufanye marekebisho haya madogo na nimsihi sana Mheshimiwa Halima Mdee kwamba nia yake na nia ya hoja, ni njema kabisa, tuendelee na suala la kufanya tathmini ya kubaini haya, lakini bila kusitisha shughuli nyingine za Kisheria ambazo zinaendelea na tukumbuke tuna Mpango na Sera nzuri ya MKURABITA ya kurasimisha mali na upimaji wa ardhi ya wananchi inaendelea. Unaposema sasa tusimamishe, maana yake mipango yote inayoendelea ya kurasimisha ardhi na kuwapa watu haki itabidi isimame kwa nchi nzima.

Kwa hiyo, bado nataka kusema kwamba jambo hili tulione tu kwamba ni muhimu kufanya tathmini ili ardhi hii ya wananchi tubaini iliyoko mikononi mwetu, iliyoko mikononi mwa wageni na kwa maana hiyo nakubaliana na mapendekezo yote mawili ya Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka na naliomba Bunge lote liunge mkono hoja hii, maana haiondoi maana halisi ya hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Mdee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Nilikuona Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na watoa hoja wote wawili kwa mantiki ya kuona na kuzingatia umuhimu wa wananchi kupata huduma au kupata ardhi inayowatosha katika maisha yao. Nakubaliana pia na Azimio la Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, kwa misingi kwamba nchi hii tunaendesha shughuli zetu kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna kazi ambazo zimeshaanza zenye nia njema kwa ajili ya Taifa hili. Sasa pamoja na maumivu tunayoweza kuwanayo, lakini haitakuwa na maana pale tutakapofanya maamuzi ya haraka. Yanaweza yakawa yanapunguza sana kasi na dhamira njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maisha yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsifu sana na kumpongeza Mheshimiwa Halima kwa sababu wengi tumekuwa tukiyaona hayo matatizo ya ardhi na wengine wamekuwa wakizungumza katika sura mbalimbali, lakini hawakuchukua jukumu la kuleta Azimio kama hili hapa Bungeni. Hapo ndipo tunapozungumza kwamba inapotokea suala la kimsingi linalowahusu wananchi, wote tunakuwa katika msimamo ulio sawa. Isipokuwa lazima msimamo wetu pia tuujenge kiasi kwamba uwe ni ule ambao utakuwa ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtaazamo wangu, kwanza katika mchango wake pia alikugusia eneo ambalo liko katika Jimbo la Kwela. Napenda pia kwa sababu jambo hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara katika Bunge letu, hususan katika shamba la Efatha na Vijiji vilivyotajwa. Kinachotutesa zaidi katika nchi hii, mimi nadhani Sera zinakuwa ni nzuri, Sheria ni nzuri, lakini watekelezaji ni sisi wenyewe. Tunapopata nafasi ya kutekeleza majukumu yetu, hatuyachukulii uzito na kukaa katika nafasi ya wananchi. Matokeo yake tunajikuta tumefanya maamuzi au utekelezaji usio mzuri na huo ndio unaosababisha leo sasa tunajadiliana hapa kwa kuona kwamba wananchi hawapatiwi haki zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la uwazi kabisa wakati Mwalimu Nyerere anaanzisha vijiji vya Ujamaa, ardhi iliyotengwa kwa ajili ya vijiji, ilikuwa inatosha kwa kuzingatia wakati ule lakini sasa hivi idadi ya wananchi hasa vijana imeongezeka sana na hawana ardhi, ardhi nyingi inamilikiwa na wazazi wao matokeo yake wanakosa maeneo ya kuendeleza na kukimbilia mjini. Ndipo ninapounga mkono kwamba tufanye hiyo tathmini ya kina bila kuathiri zoezi la uendelezaji wa ardhi linaloendelea ili kupata muafaka au kupata jambo ambalo litakuwa ni jema na endelevu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kuwafahamisha kwa wale wa Mkoa wangu wa Rukwa na Ruvuma kwamba kimsingi ni vema tusitumie sheria mkononi, tufuate taratibu ili tusijiingize kwenye vitendo ambavyo vitaonekana ni vya kihalifu badala ya kufuata taratibu ambazo zitatutoa katika tatizo tulilonalo na kupata jibu linalostahili kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno yangu haya, nizidi tu kuwaomba sana kwa upande wa wenzetu wa Upinzani na upande wa Chama Tawala kwamba wote tushirikiane kuona kwamba suala hili ambalo leo tunaliona ni tatizo, linapata muafaka wa kudumu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tumeshuhudia Bunge likichukua nafasi yake…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unachangia?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tumeshuhudia Bunge likichukua nafasi yake kama wawakilishi wa wananchi kwa sababu namna ambavyo Wabunge tulivyojadili suala hili la ardhi, tumeonesha uzalendo wetu na tumeonesha ni namna gani ambavyo tunataka kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba *spirit* ambayo tumeanzanayo asubuhi tusiiuwe hivi sasa. *Spirit* ya kujadiliana na kukubaliana jambo ambalo tunaliona ni kwa maslahi ya nchi yetu, ni kwa maslahi ya kizazi hiki na vizazi vinavyokuja na vinavyoendelea kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja ametoka kuzungumza hapa, rafiki yangu Mheshimiwa Ole- Sendeka, anasema kwamba tathmini itahitaji pesa kwa sababu Mheshimiwa Halima amesema tathmini itahitaji pesa lakini anakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri kwamba tuondoe kusitisha tubakie na tathmini. Sasa hiyo tathmini anayoisema yeye Mheshimiwa Ole-Sendeka, hizo pesa zitatoka wapi? Kwa sababu kusitisha hakuhitaji pesa, hakuhitaji pesa kabisa; kusitisha kunatupa muda wa kupumua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 55(9), inasema kwamba uoneshe maeneo gani ya Kanuni au Katiba au Sheria ambayo yanakuwa yamevunjwa. Hakuna Kifungu chochote cha Sheria zote za Ardhi, Sheria Namba 4 na Sheria Namba 5, itakayokuwa imevunjwa iwapo tutaweka *moratorium* ya muda fulani, wakati kama nchi tunajiangalia upya. Hakuna sababu yoyote ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma haya mapendekezo ya Mheshimiwa Halima, Waziri Kivuli wa Ardhi na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, *Substantive Minister* wa Ardhi, hawana tofauti, hawana tofauti yoyote. Ukiruhusu uendelee kufanya tathmini wakati bado unaendelea kugawa ardhi, utakuta umeshaigawa ardhi, utarudi tena kuanza tathmini; utakuwa unapoteza pesa za nchi. Mheshimiwa Tibaijuka, Mheshimiwa Halima, angeweza kuja hapa na Azimio la kutaka watu wote ambao ni wawekezaji ambao wamepewa ardhi, wanyang'anywe; hakusema hivyo, amekuwa *very nationalistic,* amekuwa *very pragmatic,* anasema hebu tusitishe, twendeni tukafanye tathmini.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize…

**MHE. CHROSTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sendeka ameongea, hakuna mtu aliyesimama kumpa Taarifa. Naomba tu nimalize.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sendeka, utaratibu unasimama kimya mahali ulipo na jicho la Spika, linakuona. Mheshimiwa Zitto, naomba uendelee.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninachokiomba kama namna ambavyo tulianza asubuhi kwa kuwa wamoja, tuendelee kuwa wamoja kwa maslahi ya hii nchi. Tusiruhusu tofauti za vyama kutu-*guide* kwenye maamuzi yanayohusu nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tunalolisema hapa linarekodiwa. Watoto na wajukuu wetu watakuja kutuhukumu kwa haya ambayo tunayasema hapa. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, bila kujali uko upande gani wa chama, bila kujali kadi yako ni ya rangi gani, tukubaliane twende tukafanye tathmini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sendeka!

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama chini ya Kanuni ya 68(8) inayosema:-

*"Vilevile, Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema "taarifa" na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema, ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi na kusikiliza taarifa hiyo."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye taarifa. Mheshimiwa Zitto Kabwe, rafiki yangu na rafiki yangu mkubwa sana na ninayemheshimu, wakati anajaribu kueleza yale niliyoyasema ameweka kwa namna ambayo aliyezungumzia habari ya kufanya tathmini ni Mheshimiwa Anna Tibaijuka peke yake. Azimio na Pendekezo analopendekeza Mheshimiwa Halima Mdee, linasema hivi, namba 1, kwamba, zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani, narudia, na ndani lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji. Tathmini ya kina itakapofanyika, maana yake wote wawili wanazungumza habari ya tathmini ya kina. Kwa hiyo, kama kufanya tathmini ya kina ni fedha na kwamba sio tathmini tu ya kina anayoizungumza Mheshimiwa Tibaijuka ndio inahitaji fedha, hata hii anayoizungumza Mheshimiwa Halima Mdee inahitaji fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachogombana na Mheshimiwa Zitto Kabwe, ni habari ya kusitisha, zoezi hili lipo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge na ndio hoja yangu mimi. Mazoezi yote yanahitaji fedha, yanahitaji muda na Bunge hili halijapitisha bajeti ya kufanya tathmini na kwa maana hiyo, mnasubiri bajeti ya mwaka unaokuja. Kama hapana, basi mngetoa hoja fedha maalum zitengwe; tupitishe Azimio la kutenga fedha hizo hapa na baada ya hapo tungekwenda kwenye zoezi la tathmini na hilo lisingesitisha zoezi la kisheria lililopitishwa kwa mujibu wa sheria liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa ambayo ninampa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe, taarifa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa umepewa?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea Taarifa ya Mheshimiwa Ole-Sendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema mimi Waheshimiwa Wabunge, hatuna sababu ya kutoka povu, kubishana kwa jambo ambalo lina maslahi ya nchi yetu sisi wote kwa pamoja, hakuna sababu yoyote. Ukifuata anachokisema Mheshimiwa Ole-Sendeka, maana yake ni kwamba hata pendekezo la Mheshimiwa Waziri halina maana kwa sababu hatujapanga bajeti, ndio maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema mimi ni kwamba kuna maoni ambayo Mheshimiwa Halima ameyapendekeza hapa. Kuna maoni ambayo Mheshimiwa Tibaijuka ameyapendekeza hapa. *Argument* ya Mheshimiwa Halima ni kwamba usipositisha ukaenda kufanya tathmini, utamaliza leo Mkoa wa Kigoma wakati Mkoa wa Tanga ardhi wanaigawa. Kwa hiyo, tunachokisema tuwe na muda, tutoe muda tathmini ifanyike kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri anapendekeza na baada ya tathmini kufanyika taratibu nyingine zitaendelea, hakuna *rocket science* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachokiomba mimi Waheshimiwa Wabunge, tuungane kwa pamoja tukubaliane na maoni ya Mheshimiwa Halima, tupokee maoni ya Mheshimiwa Waziri, tuamue kama nchi, tuweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimpongeze sana Mheshimiwa Halima kwa Hoja yake. Kama walivyosema wenzangu, hoja yake ni ya msingi sana na hakuna anayekataa kwamba kuna matatizo ya ardhi na hakuna anayepinga kwamba upo uvunjifu wa Sheria za Ardhi ambao mwingine unafanywa kwa makusudi au kwa maslahi fulani au mwingine unafanywa kwa kutokujua, kila mtu anajua. Kila Mbunge hapa angeweza kusema, lazima ana hadithi fulani kwenye Jimbo lake, inayohusiana na migogoro ya ardhi. Hata mimi kwangu ninao mgogoro wa ardhi. Lakini mimi wa kwangu ni tofauti kidogo, wananchi wanadai ardhi ambayo ilichukuliwa na Magereza, eneo kubwa lakini wanataka warudishiwe. Kwa hilo, namuunga mkono sana kwa kuchokoza jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo hili watu wengi wamelisema. Nakumbuka hata ndugu yangu Mheshimiwa Arfi na yeye alikuwa na hoja zake mbili siku nyingi, nakumbuka na Wabunge wengine huku wa CCM nao wamekuwa na hoja hizi. Kwa hiyo, ukiunganisha nguvu hapa, ukweli hoja hii ni ya Bunge zima na ndio maana hata Serikali, kupitia Waziri wa Ardhi, inaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ardhi, hakukataa hoja hii kwa sababu namna ya kuikataa hoja hii, tungeweza kuikataa tu kwa sababu Kanuni zinaturuhusu, lakini kwa hoja hii Serikali inaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naunga mkono kwa majadiliano haya, kama anavyosema Mheshimiwa Zitto, lazima tukubaliane. Wote tunahisi kwamba kuna utoaji usioridhisha wa ardhi katika vijiji na bahati nzuri Waziri mwenyewe kasema na wabunge wengi wamesema. Ingawa vijiji vinaruhusiwa kutoa ekari 50 kwa *minute* za wajumbe wote wa Mkutano wa Kijiji, lakini tumegundua kwamba baadhi ya vijiji ni kweli, huwa vina-*forge.* Kuna mmoja hapa amesema wajumbe wake walichukuliwa kwenye hoteli mpaka Dar-es-Salaam, wakaenda kusaini. Kwa hiyo, viko vitendo kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo hivi inawezekana hata Waziri anavijua, ndio maana amekubali. Lakini wanafanya chini ya kivuli kwa sababu kuna sheria inayowaruhusu. Kwa hiyo, anachokiomba Waziri, tena mimi ninampongeza sana Waziri kwa sababu hoja yenyewe

kaipata baada ya Mheshimiwa Halima kusoma leo. Katafakari leoleo, kakubaliana na hayo maoni leoleo, lakini pia ameomba kufanya marekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa ninamwomba Mheshimiwa Halima na wenzake wote wanaomuunga mkono, hoja hii inaungwa mkono na Wabunge wote, isipokuwa ninachomwomba Mheshimiwa Halima na wenzake, waunge mkono marekebisho kidogo ya yule mtendaji atakayesimamia utekelezaji wa hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi sana kulazimisha jambo ambalo Mtendaji hataweza kufanya, haipendezi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba tuunge mkono hoja hii kwamba tathmini ya kina ifanywe, ingawa ni kweli ina gharama, lakini tukiamua tunaweza. Tufanye tathmini ya kina na mimi sioni tatizo hata tathmini yenyewe kuletwa Taarifa ndani ya Bunge hili, sioni tatizo. Taarifa ya tathmini ije Bungeni, tunayo mijadala mingi inayoendelea ambayo kwa vyovyote itagusa tena sekta ya ardhi hata wakati wa bajeti. Bahati nzuri sasa hivi tunazungumza namna ya kuanza mapema kufanya bajeti, inawezekana mwezi wa nne tu, tukapambana tena na Wizara ya Ardhi, tukauliza mambo hayahaya. Hapa sio mwanzo na mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini hii itatupa upeo na ukubwa wa tatizo. Itatupa upeo na uwezo wa kuamua. Kutokana na tathmini hii, hata kama akifanya *sampling* kwa kuanzia Mikoa miwili, itatupa uwezo wa kuamua kwamba tufanye nini au tubadilishe sheria gani inayohusu masuala ya ardhi ya nchi yetu. Lakini mimi naona kuzuia kabisa, tunaweka jambo jipya kidogo. Mkumbuke Waheshimiwa Wabunge, kero tunazo nyingi sana. Leo tunazungumzia ardhi, kesho tutazungumzia rushwa, rushwa Mahakamani, rushwa Polisi, sasa Mahakama zote tufunge zisifanye kazi mpaka tufanye tathmini? Polisi wote wakalale majumbani kwao kwa sababu wanapokea sana rushwa mpaka tufanye tathmini, *precedent* mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mjue hapa mnaisimamisha Serikali isifanye kazi. Waziri huyu mwenyewe ndio msimamizi, ameshajua mnataka nini. Atafanya hayo mnayoyataka hata bila kumwambia. Kwa nini mfanye jambo ambalo halitawezekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza Mheshimiwa Halima, Mtoa Hoja, nia njema ya Waziri umeisikia. Yeye mwenyewe ingawa amekubali kufanya tathmini lakini ukiuliza hata mwenendo wa utoaji wa hizo hati unazozisema, ungekwenda kuchukua hata takwimu, sio hati nyingi mnazofikiri kwamba tathmini itaendelea basi Serikali itakimbia sana kugawa ardhi. Maana hapa tusichanganye mambo. Inawezekana kuna tabia ambayo hatuioni ya kutokuiamini Serikali imejificha hapa. Kwa sababu, tunatoa hoja hii na Serikali hii hatuiamini, itakimbia sana sasa, itagawa ardhi yote, mpaka tathmini itakapokwisha ardhi itakuwa imekwisha. Vinginevyo kama hakuna nia mbaya hiyo ya kuifikiria Serikali ina uroho wa kiasi hicho, kwa nini tuna mashaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao Serikali wanaofanya ni Mawaziri waliomo humu ndani. Wamesikia mwelekeo wa hoja ya Mheshimiwa Halima, watachukua tahadhari tu. Hakuna sababu ya, Mheshimiwa Zitto amesema kutoa povu, lakini mimi naona kama ninyi mlikuwa mnatumia povu zaidi, eeh? Mheshimiwa Sendeka, hajatoa povu; rafiki yangu Zitto, leo uligangamala sana, nilikuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nakuomba ndugu yangu Mheshimiwa Halima, nia njema ya Waziri, umpe muda ili afanye angalau. Mimi nasema tukifanikiwa hata kwa hilo moja tu la kufanya tathmini kwa Bunge hili tutakuwa tumepiga hatua. Yaani tukifanikiwa hata hilo la kufanya tathmini ili tuone hata hiyo Waziri anayosema 10% ya ardhi iliyopimwa iko mikononi mwa nani? Hawa watu walichukua ekari elfu 10, elfu 20, elfu 50, ambao

hawajaendeleza wako wapi? Na tuazimie kuwachukulia hatua, tutakuwa tumepiga hatua sana kuliko kusimamisha; kusimamisha maana yake unataka Serikali isimame, isifanye kazi halafu utaanza kugombana na watu. Kuna watu watajaribu kwenda Mahakamani, huwezi kujua hapa katikati wana-*process* nini, kwa nini tuingie kwenye mgogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wakienda Mahakamani, Mahakama itatuvunjia heshima, itasema imefanya Bunge limefanya kazi isiyo yake. Bunge hili halikuwa na mamlaka ya kufuta sheria kwa namna ya Azimio, kwa nini tunataka kujifedhehesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napendekeza pamoja na mjadala huu tungependa uwe mrefu sana, maana nimeona wanataka kusimama watu hapa 10, tunaweza tukaongea mpaka keshokutwa. Lakini mimi ninaomba tumpongeze sana kwa nia njema, hebu tumpe muda Mheshimiwa Waziri afanye angalau hili jambo moja, halafu tuazimie kutokana na matokeo yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nitumie nafasi hii vilevile kulipongeza Bunge zima kwa namna ambavyo limejadili mjadala huu ambao una maslahi mapana sana kwa nchi na kwa kiwango kikubwa kuweka tofauti za vyama vyetu pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza kama Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambapo kwa niaba ya wenzangu napenda niweke *position* ambayo nafikiri itatutoa katika mvutano huu uliopo tuweze kuona namna ya kwenda mbele pamoja kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Halima Mdee na Wabunge wengine wote kutoka kambi yetu ambao wamechangia mjadala huu, ni lazima kama viongozi tufike mwisho tufanye maamuzi. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Waziri kwa utayari wake na kukubali kwake kulibeba suala hili na kuona kuna sababu na hoja ya msingi ya kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishukuru sana Bunge kwa sababu tumetambua tatizo la msingi na wote, pande zote mbili tumekubaliana kuhusu tatizo la msingi ila tumekuwa tunapishana kidogo namna gani tutekeleze azma yetu ya kurekebisha hilo tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Wabunge wa upande wangu tukubali mapendekezo aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri kwamba zoezi la kusitisha ugawaji wa ardhi kwa sababu lina *further implication,* tukubali tuliache lakini tuitake Serikali basi itekeleze nia hii njema ambayo inadai kwamba iko tayari kuitekeleza kwa kipindi maalum na tusiache jambo hili likawa *open ended.* Kama sisi tuliona tatizo hili lina maslahi kwa Taifa basi vilevile tuone umuhimu wa uharaka wa kulikamilisha na kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba tathmini ifanyike kwa mapendekezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwamba tusisitishe ugawaji wa ardhi kama ilivyokuwa imependekezwa katika Azimio la msingi lakini ripoti yake ya tathmini iletwe Bungeni na iletwe Bungeni katika kipindi ambacho hakitazidi Bunge la mwezi Aprili ili tukijipa *time frame* inakuwa tumeona uzito wa jambo hilo. Kama tutakubaliana hapa, nafikiri tutakuwa tumeondoka hapa kwa salama zaidi kwamba Serikali imetueleza, tumeisikia na sisi tumeishauri

Serikali nayo imekubali kushauriwa kwa sababu tunao uzito wa tatizo basi tukafanye hiyo tahmini. Lakini kwenye Bunge la mwezi Aprili,2013 taarifa rasmi ya Serikali kuhusu tathmini hiyo iletwe ndani ya Bunge hili kisha Bunge liweze kuona mambo gani mengine ya msingi yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kuchangia hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Halima Mdee kwa kuleta hoja hii ambayo kwa kweli kwanza Bunge lako Tukufu sasa limefikia mahali pa kuweka maslahi ya Taifa mbele na mimi naomba *spirit* hii iendelee kwamba yale mambo ya kitaifa basi tusiwe na upande wowote wa kisiasa tunaoangalia, hilo nasema nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, napenda niseme mambo mawili. La kwanza, tulijiwekea utaratibu wa kisheria katika nchi na tumewaruhusu watu mbalimbali kuja kuwekeza katika nchi, tumepitisha sheria hapahapa ndani ya Bunge, sheria zetu sisi wenyewe kwa wakati wote tulitakiwa kurudi Bungeni na kuirekebisha. Sasa unapochukua hatua ya jambo lolote lile kulisimamisha haraka hatimaye ni watu kwenda Mahakamani na kudai fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbowe ni shahidi, kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, tumeshuhudia Serikali ikilipa fedha nyingi kwa maamuzi ambayo hatukuyafikiria vizuri na hatimaye tunaingia kwenye gharama kubwa ya kulipa fedha na hatimaye wananchi wanaendelea kulipa deni la Taifa. Kwa hiyo, nafikiri jambo la kuharikisha kuzuia ni jambo ambalo lisingeweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema nashukuru na namshukuru Mheshimiwa Mbowe kwamba kwa upande amekubali pendekezo la Mheshimiwa Waziri likubalike na mimi napenda vilevile nimshauri ndugu yangu Mheshimiwa Halima tukubali kwamba tathmini ifanyike kwa kipindi fulani lakini ningeomba jambo la ziada zaidi ni vyema Serikali ikatoa utaratibu utakaoeleweka wa aina ya tathmini itakayofanyika na taarifa zake si tu kungoja Bungeni pale ambapo tumepata taarifa kuna taathila fulani zilifanyika basi hatua haraka zichukuliwe. Kwa mfano, wako wawekezaji wameandikishwa kwenye *Tanzania Investment Center* wana maeneo wamekaa nayo kwa muda mrefu, hii haihitaji tathmini ya muda mrefu, taarifa ipo, ichukuliwe na maamuzi yachukuliwe haraka kwa upande wa Serikali ili ionekane Serikali sasa imefanya juhudi na hatua, pale ambapo tayari uvunjwaji wa sheria umetokea tusilegee katika hili. Wako *investors* wameji-*register* pale lakini vitendo wanavyovifanya ndani ya ule uwasilishaji wao wa *investments* ni vitu viwili tofauti na hatuchukui hatua kabisa, sasa hili nafikiri likifanyiwa kazi haya maneno yote mengine yatakuwa-*taken care.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimalizie kusema, wenzetu wa Zimbabwe waliwafukuza wawekezaji wakakimbilia Msumbiji, Msumbiji inawauzia chakula Zimbabwe na dunia ya hivi sasa kama kuna tatizo kubwa sana ni tatizo la chakula. Kwa hiyo, lazima tutahadhari maamuzi yetu yasije yakaifanya Tanzania hii yenye ardhi ya *square* kilomita milioni 29 hazijalimwa tukabaki na njaa. Kwa hivyo, naomba sana tusibaki na njaa kwa sababu tu ya maamuzi ambayo siyo sahihi hatimaye tukaenda kuhemea chakula kwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ifanye mambo matatu:-

(i) Pale ambapo sheria imevunjwa basi tusichelewe, tathmini ya kwanza ni kuangalia maeneo ambayo mwekezaji kachukua eneo kwa ajili ya kawekeza lakini hawekezi aondolewe kwa mujibu wa mkataba ulivyo. *(Makofi)*

(ii) Kwa maeneo ambayo tayari yako kwenye *process* hivi sasa, ni vyema Serikali ikaangalia, je, taratibu zote za kisheria zimefuatwa? Au wenzetu huko ndani wamelanguliwa na kadhalika, rushwa imetumika watu kupata ardhi? Hilo nalo lingefanyiwa kazi haraka.

(iii) Waiagize Mikoa *specifically* waangalie watu wangapi walionao ambao wanawekeza hivi sasa na orodha hiyo iwasilishwe Bungeni ili tupate taarifa kwamba wawekezaji tunaowazungumza maana inawezekana tunazungumza hewa kumbe wawekezaji wenyewe ni watano au sita, wawekezaji wengi wakawa ndani ya nchi ambao na wao wamehodhi ardhi. Hizo taarifa zikitoka kwa haraka zitatusaidia kufanya maamuzi sahihi ili hatimaye Tanzania isije ikabaki na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawaomba wenzangu tukubaliane na mapendekezo yaliyotolewa hapa ili tupitishe hoja yetu tuendelee na hoja nyingine, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri sasa kwa busara ya Kiti na kwa namna hali halisi ya majadiliano yanavyokwenda na ukizingatia kwamba tulikuwa tunaendelea na Kanuni hiyohiyo ya 57 na zile fasili zake zote. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Waziri ambaye ametoa hoja ya mabadiliko lakini hoja hiyo imechangiwa kwa kuboreshwa kwa mujibu wa Kanuni hiyohiyo ya 57(5)(6) mpaka ya (7). Hebu tusikie Mheshimiwa Waziri kwa mabadiliko yale ambayo yamependekezwa sasa ya kuweka muda maalumu anasemaje ili tumalize hoja hii tuweze kuingia hoja nyingine, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuwashukuru kabisa wachangiaji na kutambua kwamba Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani naye ametusaidia sana kama nilivyoomba, ameonyesha *by partnership* na hiyo ndiyo inayotakiwa katika suala hili la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema wakati nachangia kwamba hapa hakuna *ideology*, tunazungumza mustakabali wa Taifa letu. Katika hoja yangu sikutaka kutumia maneno mengi ningeweza kuandika *page* mbili, tatu nimetumia maneno kwamba uhai na uwepo wa Taifa, kama tungekwenda kama ilivyokuwa hoja yenyewe ya mwanzo ilivyokuwa inasema hata uhai na uwepo wa Taifa unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza, hatuna *definition* ya mwekezaji kwa sababu ukienda namna hiyo kuna wawekezaji wa vitunguu wana eka tano, ni wawekezaji katika vijiji. Kwa hiyo, kazi yao ingesimama kwa sababu mimi nilikuwa ninaiangalia kwa upana wake kama mtendaji wa sekta kusudi twende mbele. Hoja hii hakuna mjadala ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tumeshafika hapa tulipofika, mimi naona sasa tuko kwenye *constructive proposal*. Sasa hapa Azimio linakuwa *constructive*, linatekelezeka kwa sababu kusimamisha sekta ya ardhi katika nchi hii ni kitu ambacho hakiwezekani, hakitekelezeki kama hapa tunazungumza siyo kwa sababu tusikike, kama kweli unazungumza *constructive proposal* huwezi kusema usitishe kabisa kabisa. Hii pia ilikuwa haijaeleweka, *it is a tenable,* usingeweza kwenda mbele, umesitisha sekta ya ardhi. Ndiyo maana hapa namshukuru Mheshimiwa Mbowe na Waheshimiwa wote waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kwa upande wangu kama mtendaji wa sekta, kwanza nimesema kwangu mimi hakuna jipya, haya yote yaliyoandikwa humu ninayajua, ninayafanyia kazi labda tu sema sijazungumza sana nikasikika lakini mimi naamini kazi kwanza maneno baadaye. Sasa kwa kuwa kazi inaendelea na ilishaanza. Mimi nakubali kabisa kwamba kama sasa tunaboresha nadhani Mheshimiwa Mbowe alipendekeza tuwe tumemaliza tathmini kwenye Bunge la mwezi wa nne na kwa kujua kabisa kwamba Serikali suala hili siyo kwamba tumelilalia, Wizarani tunaendelea nalo, mimi bila kupoteza wakati, ninakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mbowe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kukubaliana kwamba hoja yangu iboreshwe na kwamba tunatoa hoja ndani ya miezi, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbowe, mwezi wa nne tathmini iwe tayari na kwa sababu hili ni agizo la Bunge, ninaamini na wenzangu Hazina wananisikia kwa sababu na mimi nitahitaji uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole-Sendeka hakudanganya, maana tathmini ya namna hii ni lazima iwe *credible,* huwezi kubabaisha, huwezi kuleta porojo hapa Bungeni ni lazima ufanye *survey*, ni lazima uwe na takwimu hata ukifanya *sampling* lazima uwe na *sampling frame,* kigezo chako cha kufanya *sample* ni nini? Ni lazima uwe na *list* ya mashamba yote ya uwekezaji, ndiyo *sampling frame* na ndiyo *from the sampling frame* unaweza ukaangalia kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubali kabisa kwamba mapendekezo hayo kama yameelezewa kama hivyo, natoa hoja basi kwamba tunaboresha Bunge la mwezi wa nne tathmini itakuja na kwamba wahusika maana ni tathmini ya Serikali, wahusika wengine wataniwezesha niweze kufanya kazi nzuri, nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana. Nimekuona Mheshimiwa Chenge, nitakupa nafasi. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana na hasa kwa kweli nawashukuru sana kwa mjadala huu wenye afya njema ndani ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 57(7) hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja nyingine ya mabadiliko sharti ihusiane na hoja kwanza ya mabadiliko na itolewe na ijadiliwe na kuamliwa. Kwa hiyo, ndiyo maana aliposema Mheshimiwa Mbowe mimi nilimpa tena nafasi Mheshimiwa Hamad Rashid ili kuendelea kuijadili na baada ya hapo sasa ninafikia hatua ya mwisho. Ninaomba sasa nichukue nafasi hii kwanza kuwahoji hoja hii ya mabadiliko iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri na kuongezewa sasa kipindi maalum cha utekelezaji na baada ya kuwahoji hoja hii ya mabadiliko ndipo tutarudi sasa kwenye ile hoja ya msingi. Sasa nitaanza kuwahoji wanaoafiki kwamba hoja hii ya mabadiliko iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri lakini ikachangiwa...

*(Hapa baadhi ya Wahehimiwa Wabunge walikuwa wakipiga kelele za chinichini)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jana tumepewa maelekezo, Mwenyekiti akishasimama yeye ndiye mwenye madaraka ya kuzungumza. Nimemwona Mheshimiwa Chenge, nitampata nafasi, naomba mniache niendelee kwanza.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kupiga kelele)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wanazomea)*

**MBUNGE FULANI:** Kabla!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, waliosimama naomba waketi, naomba Waheshimiwa Wabunge waliosimama waketi. *(Makofi)*

Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote waliosimama waketi. Waheshimiwa Wabunge, sasa ninawahoji, wanaofiki hoja ya mabadiliko iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ikajadiliwa na Bunge na ikahitimishwa na Mheshimiwa kwa kutoa makubaliano ya mjadala huu kupitia maamuzi ya Serikali. Kwa hiyo, mnanielewa hapo kwa sababu hoja ya mabadiliko imetolewa na Mheshimiwa Waziri, imejadiliwa na Bunge na Mheshimiwa Waziri aliposimama ametoa hoja yake, ameelezea hoja yake ile ambayo iko hapa na labda niisome ili tuelewane vizuri. Naomba niisome tuelewane vizuri tunachokizungumza ni kitu gani. Mheshimiwa Waziri hoja yake inasema hivi, anapobadili hoja ya Mheshimiwa Mdee, anasema kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na wa ndani lifanyiwe tathmini, tunakwenda pamoja Waheshimiwa Wabunge? Lifanyiwe tathmini ya kina ili kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mkononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji.

Ya pili, Waheshimiwa Wabunge twende pamoja, hicho ndicho nachotaka kuwahoji. Ya pili, kwamba tathmini itakayofanyika ibaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za Vijiji kinyume na matakwa ya Sheria ya Ardhi, Na.5 ya mwaka 1999 na kwamba nyongeza sasa ambayo Mheshimiwa Waziri hapa amesema taarifa ya tathmini hiyo italetwa katika Bunge la mwezi wa Aprili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maneno ya Mheshimiwa Waziri.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ya mabadiliko imepitishwa na sasa ninarudi, Waheshimiwa Wabunge ninaomba tusikilizane, hoja ile ya msingi ya Mheshimiwa Halima Mdee ikiambatana sasa na mabadiliko haya ambayo yameletwa na Serikali yamejadiliwa na Bunge na kuamliwa sasa yachukuliwe kama maazimio kamili ya Bunge hili.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga makofi na makelele mengi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order, order,* tunaelekea kwenye hoja ya pili na hoja ya pili sasa nitamwita Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ili aweze kuwasilisha hoja yake.

**Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto Kuhusu Kuitaka Serikali Kuchukua Hatua Dhidi ya Watanzania Walioficha Fedha Harama Nje ya Nchi**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuleta hoja binafsi chini ya Kanuni ya 54(1), (2) na (3) na pia kwa kutumia Kanuni ya 55 (11). Nitakayosoma ndiyo hoja yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 2 Novemba, 2012 niliwasilisha barua ya kusudio la kuwasilisha Bungeni hoja binafsi kuhusu suala la Watanzania waliokficha fedha na mali haramu nje ya nchi. Lengo la hoja binafsi hiyo ni kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasiliana na Taasisi ya Benki ya Dunia kupitia kitengo cha *Assets Recovery Unit*, kurejesha fedha haramu zilizofichwa na raia wa Tanzania katika mabenki huko nchini Switzerland. Ofisi yako ilinitaka nilete maelezo ya ziada kuhusu hoja hiyo ili ipatiwe nafasi ya kupangwa kwenye ratiba za Bunge na sasa nawasilisha hoja yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni, 2012, Benki Kuu ya Switzerland yaani *Switz National Bank* ilitoa taarifa kwa umma kuhusu raia wa mataifa mbalimbali duniani wenye dhamana kwenye mabenki nchini humo. Benki hiyo ilitangaza kwamba jumla ya dola za Kimarekani milioni 196 zilikuwa zimehifadhiwa kwenye akaunti za mabenki mbalimbali nchini humo na kwamba wenye fedha hizo ni raia wa Tanzania. Fedha hizo ni zaidi ya shilingi bilioni 312 ukizibadilisha kwa thamani ya fedha za Tanzania kwa bei ya jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo yangu ya mwisho niliyoyafanya jana usiku na wachunguzi binafsi yameongeza taarifa ya ziada muhimu. Kwanza kiwango cha fedha kinachomilikiwa na Watanzania nchini Switzerland peke yake ni takribani mara 20 ya kiwango kilichotangazwa na Benki ya Taifa ya Switzerland. Kwa mfano, Benki ya *UBS* peke yake ina maafisa 240 wanaohusika na Tanzania peke yake. Kila afisa mmoja husimamia mteja mwenye kiwango kisichopungua dola za Kimarekani milioni 10, hawa ni *Relationship Managers* wa *customers* wao hapa Tanzania. Fedha hizi ni sehemu tu ya fedha ambazo Watanzania wanazificha katika mabenki mbalimbali nje ya nchi na hasa visiwa vya Jersey, Mauritius na Cayman Islands maana nchi nyingine hazina utaratibu huo wa kuweka wazi kama ilivyo Switzerland ilivyofanya kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la *The Guardian* la tarehe 23 Juni, 2012 lilimnukuu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ndugu Edward Hosea, akisema kwamba siku ya Jumatatu tarehe 24 Juni, 2012 angeandika barua kwenda kwenye mamlaka za Switzerland kutaka kupewa orodha ya majina ya Watanzania wenye fedha katika akaunti zilizotajwa. Hata hivyo, mpaka ninavyoleta maelezo haya hapa Bungeni, umma wa Watanzania haujaelezwa kama barua hiyo iliandikwa na majibu yake yalikuwa ni nini. TAKUKURU ndiyo mamlaka hapa nchini ambayo inaweza kupata orodha ya majina ya watu wenye mabilioni haya kwa njia za halali na hasa kwa watu ambao wanaitwa *'Politically Exposed Persons'* kama Wabunge na waliowahi kuwa Wabunge, Mawaziri na waliowahi kuwa Mawaziri na viongozi wengine wa ngazi za juu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine duniani zimetumia njia mbalimbali kuhakikisha fedha haramu zinazotoroshwa zinarejea nchini kwao. Marekani na Ujerumani wao waliamua kununua *CDs* kutoka kwa waliokuwa wafanyakazi wa mabenki ya *Switzerland* wakagundua raia wao walioficha fedha nje na kuwatoza kodi kutokana na fedha hizo. Ujerumani wao wameingia mkataba wa kupashana taarifa za kikodi na nchi ya Switzerland ili kuwatoza kodi raia wao wenye fedha huko. Hata hivyo, mkataba huu wa kikodi haujapitishwa na Bunge la Ujerumani, Bunge la juu yaani Bundesrat kwani chama kikuu cha upinzani cha cha *SPD* kinapinga na tayari chama hicho kupitia Waziri wake wa Fedha wa Jimbo la *Nordrhein-Westfalen* wamenunua *CDs* zenye majina ya raia wa Ujerumani wenye akiba nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi karibuni gazeti moja nchini Ugiriki limechapisha orodha ya Wagirika walioficha fedha zao huko Switzerland. Orodha hii inatokana na orodha ambayo aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Ufaransa Christine Lagarde aliipa Serikali ya Ugiriki lakini Serikali hiyo haikufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiufupi, toka taarifa za Benki ya Taifa ya Switzerland kutangazwa, Serikali yetu haijachukua hatua yoyote ya maana kuhakikisha kuwa suala hili linafanyiwa uchunguzi wa kina na hatua stahili dhidi ya watoroshaji wa fedha hizo zinachukuliwa ikiwemo kurejeshwa kwa fedha hizo nchini kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Ikumbukwe kwamba kati ya Watanzania wenye fedha huko nje wapo ambao fedha zao wamezipata kihalali kutokana na shughuli za kibiashara na wapo ambao wamepata fedha hizi kwa njia ya rushwa. Uchunguzi wa kina ni muhimu sana kufanyika ili kuweza kutofautisha kati ya fedha haramu na fedha halali. Vilevile uchunguzi unatakiwa kutofautisha kati ya watu wenye fedha halali kama walifuata taratibu za kisheria za nchi zinazoruhusu raia wa Tanzania wanaoishi Tanzania kuwa na akiba ya fedha za kigeni nje ya Tanzania. Kitendo cha Serikali kukaa kimya bila kuchukua hatua kinaashiria ama kutotimiza wajibu au kwamba wanaopaswa kuchukua hatua ni washirika wa utoroshaji huu wa fedha za nchi na kuzificha katika mabenki ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza kwa kina vyanzo viwili vikubwa vya fedha kwa raia wa Tanzania wanaomiliki fedha na mali katika mabenki ya nje, nieleze kwamba, watu hufungua akaunti nje ya nchi au kumiliki mali nje ya nchi kwa sababu kuu mbili:-

(i) Ni kuficha fedha haramu zilizopatikana kwa njia zisizo halali; na

(ii) Ni kukwepa kodi kutokana na mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya kwanza hutumiwa zaidi na wanasiasa na watendaji wa Serikali kama nilivyoeleza hapo awali *Politically Exposed Personalities* na njia ya pili hutumiwa na wafanyabiashara wakubwa na hasa wafanyabiashara wanaouza bidhaa nje ya nchi. Harakati zozote za kuchukua hatua za kuchukua hatua dhidi ya makundi haya zina faida ya kuzuia ufisadi kwa kuonyesha kwamba hakuna pa kujificha iwapo ukifanya ubadhlifu na kuongeza mapato ya Serikali kwa kuhakikisha raia wote wakaazi yaani *residents* wanalipa kodi inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya *Global Financial Integrity* ya mwaka 2008, jumla ya dola za Kimarekani bilioni nane (8) zimetoroshwa kutoka Tanzania kati ya mwaka 1970 mpaka 2008. Kwa bei ya sasa ya dola za kimarekani fedha hizi ni sawasawa na shilingi trilioni 13. Mpaka mwezi Julai, 2012 deni la Taifa kuanzia mwaka 1961 mpaka Julai 2012 lilikuwa ni dola za Kimarekani bilioni 10. Hii maana yake ni kwamba fedha zote zilizotoroshwa kutoka Tanzani katika kipindi cha miaka 38 zingeweza kulipia 80% ya deni la taifa. Mwaka 2012 – 2013, Bunge limeidhinisha jumla ya shilingi trilioni 1.9 kulipia deni la Taifa. Suala hili ni changamoto kwa nchi mbalimbali za Kiafrika ambapo mabilioni ya fedha hutoroshwa kila mwaka na watawala wala rushwa na wafanyabiashara wasio waaminifu kwenda nje ya Afrika na kuliacha Bara la Afrika likiwa na ufukara wa kutupwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya fedha zilizotoroshwa zilitokana na ufisadi, nyingine zilitokana na ukwepaji wa kodi na nyingine zilitokana na madeni ambayo Serikali iliingia ambapo sehemu kubwa ya madeni ilibaki hukohuko ughaibuni lakini bado Watanzania wanayalipa madeni haya. Hata hivyo, fedha zilizotokana na ufisadi na zile za ukwepaji kodi ni nyingi zaidi katika fedha zilizotoroshwa kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kati ya mwaka 2003-2005, Tanzania iligubikwa na ufisadi mkubwa sana wa fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania ambapo jumla ya shilingi bilioni 135 zililipwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwenda Benki ya *NedBank* ya Afrika Kusini kama malipo ya mkopo ambayo Serikali iliudhamini kwa ajili ya mradi wa uchimbaji dhahabu, mradi

wa Meremeta. Fedha hizi zilikuwa ni mara 15 ya mkopo uliodhaminiwa na Serikali. Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa 70% ya fedha za mradi wa Meremeta ziliishia kwenye Benki nchini Switzerland kupitia nchi ya Mauritius. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya Meremeta ambayo baadaye ilibadilishwa jina kuitwa *TanGold* ilianzishwa kama mradi wa kutorosha mabilioni ya fedha za nchi kwenda kwa uhusika mkubwa sana wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha mezani kwako barua kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu ya tarehe 20 Agosti, 2001 yenye kumbukumbu nambari SHC/M.100/4/A kwenda *Deutsche Bank* Tawi la Uingereza kuitambulisha kampuni ya Meremeta na kampuni ya *Nedcor Trade Services Limited* ya Afrika Kusini ili ipewe mkopo wa dola milioni 10. Barua hiyo inatambulisha miradi miwili ya dhahabu yaani mradi wa Tembo ambao ulikuwa ni *undergroung mine* na mgodi wa Buhemba, kwamba ni miradi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Baada ya barua hiii, yaliyotokea ni mtandao mpana wa kuiba fedha za Tanzania kwenda Afrika Kusini baadaye Mauritius na kisha kuingia kwenye akaunti za watu binafsi nchini Switzerland na visiwa vingine ambavyo vinahusina na ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia barua hii kutoka Ikulu, mkopo wa dola za Kimarekani milioni 10 zilipatikana. Hata hivyo, Serikali ya Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania ililipa Benki ya *NedBank* jumla ya dola za Kimarekani milioni 138. Dola milioni 10 kati ya hizi zililipwa kupitia kupitia kampuni ya *Deep Green Finance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya uchunguzi binafsi kuhusu suala hili, nilijaribu kuwasiliana na benki ya *NedBank* ili kuweza kupata uhakika wa watu waliofaidika na uchotaji huu mkubwa na wa kihistoria wa fedha za umma. Ufuatiliaji huu umeendelea vya kutosha ila haujafikia mwisho. Hata hivyo, taarifa nilizokusanya hadi sasa zimeonyesha hatari kubwa namna ambavyo Watanzania wenzetu wenye mamlaka wanavyokwapua fedha za umma kwa faida yao. Nyaraka zote za wizi na utoroshaji huu wa fedha na mawasiliano yangu na watu wa *NedBank* nitayawasilisha mbele ya Kamati ya Bunge ninayopendekeza kuundwa ili kutazama suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala yanayohusu usalama wa nchi kutokana na kashfa hii ambayo pia ningependa kuyaonyesha katika Kamati ninayopendekeza kuundwa. Nyaraka hizo zinaonyesha silaha na aina ya silaha zilizonunuliwa na kutoka nchi gani na kwamba silaha hizo ziliishia wapi. Nimeona kuyasema masuala haya waziwazi kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, masuala haya ni muhimu yafahamike ili kuweza kuchukua hatua kwa watu wote watakaokutwa wamefanya makosa ya kuiibia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoibwa na kutoroshwa kupitia kampuni ya Meremeta na kampuni ya *Deep Green* ziliishia kwenye akaunti za watu binafsi kama nilivyoeleza hapo awali. Hata hivyo, mara baada ya kuundwa kwa kampuni ya *TanGold,* jumla ya dola za Kimarekani milioni 10 ziliwekwa kwenye akaunti ya kampuni hiyo katika Benki ya *NBC Corporate Branch,* nambari ya akaunti hiyo pia itatolewa katika Kamati ninayoomba kuundwa kwa ajili ya uchunguzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004, 2006 na 2007 Tanzania iligawa vitalu vya kutafuta mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali nchini. Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa zaidi ya dola za Kimarekani milioni 56 zililipwa kwenye akaunti za watu binafsi nchini Switzerland kutoka kwenye kampuni zilizoshinda zabuni ya kutafuta mafuta na gesi. Uchunguzi nilioufanya kwa msaada wa wachunguzi waliobobea kwenye masuala ya mifumo ya kifedha ya kimataifa

umeniwezesha kupata nyaraka muhimu zinazoonyesha watu na namna walivyopata fedha walizoweka katika akaunti zao nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 na 2005 mwanasiasa wa Afrika Kusini kutoka Chama cha *ANC,* Bwana Tokio Sekswale alitembelea nchini katika ziara ya kibiashara. Alileta marafiki zake wawili na kuanzisha kampuni iitwayo *Ophir Energy Tanzania limited.* Kampuni hii inamiliki vitalu vitatu katika Pwani ya Bahari ya Hindi, *Block I, Block III na Block IV.* Bwana Tokio Sekswale alitambulishwa hapa nchini na raia wa Kongo aitwaye Moto Mabanga. Hivi sasa Bwana Moto Mabanga ameishtaki Kampuni ya *Ophir Energy* kwa kutotimiza masharti waliyokubaliana kuhusiana na kufanikisha kupatikana kwa vitalu hivyo vya mafuta. Bwana Moto Mabanga ndiye alikuwa *deal maker* wa kampuni hii na ili kufanikisha hali hii alihonga sana wanasiasa na maafisa wa Serikali wanaohusika na ugawaji wa vitalu vya kutafuta mafuta na gesi. Wakati *Ophir* wanapewa vitalu hivi, sehemu ya hisa za kampuni hii ziligawiwa kwa baadhi ya Watanzani ikionekana kuwa ni hisa kwa ajili ya Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, uchunguzi wetu unaonyesha kuwa hisa hizo zilikuwa ni za watu binafsi. Hivi sasa hisa hizo zimeuzwa na fedha kufichwa katika mabenki mbalimbali nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kufanya uchunguzi wa kina kuhusu umiliki wa kampuni ya *Ophir Energy* wakati wanaingia nchini na mabadiliko ya umiliki katika kipindi cha miaka nane iliyopita. Vilevile uchunguzi unapaswa kufanywa kwa vitalu vyote vilivyogawiwa kati ya mwaka 2003 na 2008 na umiliki wa Watanzania katika makampuni yaliyopewa vitalu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu iagizwe na Bunge lako Tukufu kupata taarifa za kina kupitia njia za Kiserikali na njia za wachunguzi binafsi. Mimi kama Mbunge nilipofikia sasa nahitaji msaada wa Bunge kufanikisha jambo hili. Nilipofikia sasa ni kutoa taarifa na nyaraka zote nilizonazo na watu na taasisi, zitakazosaidia Kamati Teule ambayo Bunge litaundwa kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KWA KUWA kumekuwa na uthibitisho kutoka mamlaka za nchi ya Switzerland kwamba kuna raia wa Tanzania wanamiliki fedha za kigeni katika Benki nchini humo na kwamba kuna kanuni na taratibu za nchi zinazoendesha na kuongoza ufunguaji wa akaunti wa fedha za kigeni nje ya Tanzania kwa Watanzania wakaazi *(residents)* na kwamba kitendo kilichofanywa na wahusika kuweka mabilioni ya fedha kwenye nchi za nje kinaweza kuwa ni kinyume na Sheria ya *Foreign Exchange Act* ya mwaka 1992;

NA KWA KUWA sheria hiyo kifungu cha 10 cha Sheria ya Fedha za Kigeni kinazuia utoroshwaji wa fedha za Kitanzania isipokuwa kwa kibali cha Gavana wa Benki Kuu tu, hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kusafirisha fedha nje ya Tanzania na kinaeleza kuwa kwa msafiri anayekwenda nje ya Tanzania hataruhusiwa kuondoka na kiasi cha shilingi ambazo zinazidi dola za Kimarekani 50. Vilevile kwa mujibu wa sheria hiyo kifungu cha 6 na 7 na waraka ulitolewa na Gavana wa Benki Kuu kwamba Mtanzania yeyote mwenye kutaka kufungua akaunti kwenye mabenki ya nje ya Tanzania lazima apate kibali cha Gavana;

NA KWA KUWA masharti hayo ya sheria yanaweza kuwa yamekiukwa na wahusika kwa kuhifadhi fedha za kigeni katika mabenki ya nje;

NA KWA KUWA ukiukwaji huo ni dhahiri kuwa fedha zilizowekwa kwenye mabenki ya nje na kwa kiasi kikubwa ni fedha ambazo hazikupatikana kwa njia za halali na kwamba kuna uwezekano wa ukwepaji mkubwa wa kodi;

NA KWA KUWA nchi yetu imekuwa katika matatizo makubwa ya fedha za kigeni, jambo ambalo limepelekea nchi yetu kushusha thamani ya shilingi ili kukabiliana na gharama za manunuzi ya bidhaa nje ya nchi;

KWA HIYO BASI naliomba Bunge lako Tukufu liazimie:-

(i) Kwamba Bunge lako Tukufu liunde Kamati Teule kuchunguza raia wa Tanzania wenye kumiliki fedha za kigeni na mali nje ya Tanzania. Kamati Teule hiyo ifanye kazi zifuatazo:-

- Kuchunguza mfumo mzima wa utoroshaji wa fedha na kufichwa nje ya nchi;

- Kuchunguza na kupambanua mali na fedha haramu dhidi ya halali zinazomilikiwa na raia wa Tanzania katika taasisi za fedha nje Tanzania;

- Kuchunguza utaratibu mzima wa kugawa vitalu vya utafutaji mafuta na gesi kati ya mwaka 2003 – 2008;

- Kuchunguza mtiririko mzima wa utoroshaji wa fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania kupitia kampuni ya Meremeta na pia kampuni tanzu ya *Triannex pty* ya Afrika Kusini na *Deep Green Finance Limited* na kupendekeza hatua za kuchukua dhidi ya wahusika wote wa utoroshaji wa fedha kwenda nje;

- Kuchunguza umiliki wa Watanzania kwenye kampuni zote zenye mikataba ya utafutaji wa mafuta na gesi hapa nchini na namna umiliki huo umekuwa ukibadilika yaani *proceeds* zilizotokana na mabadiliko hayo ya umiliki na kama kodi stahili zimekuwa zikilipwa kutokana na mabadiliko ya umiliki huo; na

- Kuchunguza kwa kina mali za Watanzania wote waliowahi kushika nafasi za Uwaziri Mkuu kati ya mwaka 2003 mpaka 2010, waliowahi kushika nafasi za Uwaziri wa Nishati na Madini, Uwaziri wa Ulinzi, Ukuu wa Majeshi, Ukatibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ukatibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi, Uanesheria Mkuu wa Serikali, Ukamishna wa Nishati, Ukurugenzi Mkuu wa *TPDC*, Uenyekiti na Ujumbe wa Bodi wa *TPDC* katika ya mwaka 2003 mpaka 2010.

(ii) Kwamba, Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni ifikapo Mkutano wa 11 wa Bunge kwamba itakuwa ni marufuku kwa Kiongozi yeyote wa Umma au mume au mke wake au watoto wake kuwa na akaunti katika mabenki nje ya nchi isipokuwa kwa sababu maalumu na kwa kibali rasmi kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kwamba, Serikali iwasiliane na Benki ya Dunia ili kupitia Kitengo cha *Assets Recovery Unit* ili mabilioni ya Fedha na mali zisizoondosheka zinazomilikiwa na Watanzania katika mabenki ya nchini Switzerland, Dubai, Mauritius na visiwa na maeneo mengine yote ambapo hufichwa fedha na mali ili kukwepa kodi na kwamba mali hizo na mabilioni hayo yaliyopatikana kiharamu yarudishwe nchini mara moja. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

(iv) Kwamba, katika Muswada tajwa hapo juu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aimarishiwe mamlaka ya kutoa kibali kwa Mtanzania yeyote anayetaka kufungua akaunti ya Benki nje ya nchi na kwamba kila mwaka Gavana atatangaza kwenye Gazeti la Serikali na magazeti yanayosomwa na wananchi wengi orodha ya Watanzania walioomba na waliruhusiwa kuwa na akaunti ya benki nje ya Tanzania;

(v) Kwamba, Watanzania wote wenye akaunti za fedha nje waeleze wamezipataje na TAKUKURU wachukue hatua za kisheria dhidi ya watu wote wenye kumiliki fedha na mali kinyume na mapato yao halali;

**T A A R I F A**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto dakika moja. Mheshimiwa Assumpter!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kifungu cha 68 kwamba hayo anayosoma Mheshimiwa Mbunge hatunayo katika taarifa yake. Pia ukiangalia Kanuni ya 56 anatakiwa asomee mahali kwake, pale kwenye kiti chake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Assumpter, naomba urudie hoja ya kwanza.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza ni kwamba habari zilizomo katika hiki kitabu ziko tofauti na kitu anachotusomea sasa hivi. La pili anatakiwa asome akiwa kwenye kiti chake pale kulingana na Kanuni kama alivyofanya Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Assumpter sasa hiyo ni taarifa, ungeomba Mwongozo ili mimi nikupe ufafanuzi, sasa ukimpa taarifa huyo anatakiwa aijibu, ila hebu Waheshimiwa Wabunge ngojeni, Mheshimiwa umetumia Kanuni namba 68?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Kanuni ya 68.

**MWENYEKITI:** Eeh!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliguna)*

**MWENYEKITI:** Haya, hebu, hebu...!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Anachokisoma hapo hatuna hapa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliendelea kunong'ona)*

**MWENYEKITI:** Hebu taratibu, taratibu tu Waheshimiwa Wabunge! Ngoja kwanza nimwelewe vizuri mtoa hoja. Naomba tu msiwe na haraka, tumwelewe vizuri mtoa hoja. Umesema Kanuni namba ngapi?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Kanuni iliyonifanya nisimame ndiyo nimesema ya 68, ya kusema jambo ambalo naliona ni tofauti.

**MWENYEKITI:** Sitini na Nane ngapi, ni kuhusu utaratibu ama! *Any way* ngoja tuendelee. Mheshimiwa Assumpter naomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kabisa, kwa mujibu wa Kanuni, Mbunge anapotoa hoja kwanza anatakiwa kusimama mahali pake alipo. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, ni kweli kabisa na ninaomba radhi kwa sababu suala hilo nilimweleza Mheshimiwa Halima Mdee na kwa kweli sijamtendea haki Halima Mdee kwa sababu Mheshimiwa Zitto Kabwe alipokuwa anaanza nilikuwa nime-*concentrate* na Kanuni hapa, si unajua leo mambo ya Kanuni humu yamekuwa mazito sana. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Zitto ukamalizie pale mahali pako unapotakiwa. Mheshimiwa Zitto, naomba usikilize kauli ya Mwenyekiti, naomba urudi kwenye kiti chako utamalizia ukiwa pale. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Hilo lingine la pili lazima niwe na uhakika na anachokisema Mheshimiwa Assumpter.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa waliguna)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize. Naomba mwache amalizie wakati huo nalifanyia kazi suala hili na nitalitolea maelekezo. Mheshimiwa Zitto naomba umalize halafu nilitolee maelekezo.

*(Hapa minong'ono miongoni mwa baadhi ya Wabunge iliendelea)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

(vi) Kwamba, Serikali, katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja (11) na baada ya Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge kuhusu raia wa Tanzania wenye kumiliki fedha za kigeni kwenye mabenki na mali nje ya Tanzania ilete taarifa ya hatua ilizochukua ili kuziba mianya ya utoroshaji wa fedha nje ya Tanzania.

(vii) Kwamba, Serikali katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 itaanzisha kodi maalum '*financial transaction tax*' ya angalau asilimia 0.5 ya thamani ya '*transaction'* ili kuweza kuwa na rekodi za uhakika za fedha ndani na zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona, hoja imetolewa na imeungwa mkono lakini naomba nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Kabwe Zitto kwa jinsi alivyowasilisha hoja yake, isipokuwa kama alivyosema Mheshimiwa Mchungaji, anaitwa nani yule?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Assumpter Mshama, baadhi ya maneno ambayo Mheshimiwa Zitto ameyasema hayako kwenye hoja yake. Kwa hiyo, labda hili ni suala

la kujadiliana naye tujue hayo maneno yanaingia sehemu gani, siyo jambo la kukunjiana uso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ya Mheshimiwa Kabwe inahusu matumizi ya Sheria za Kijinai. Sheria hizo ni pamoja na Kanuni ya Adhabu, Sheria ya Mapato ya Kijinai, Sheria ya Ushirikiano katika Masuala ya Jinai, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sheria ya Ushahidi, Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Sheria ya Kudhibiti Uhalifu na Uhujumu Uchumi, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na Sheria ya *Foreign Exchange Control*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Serikali inalijua. Ilipopata taarifa ile iliyochapishwa kwenye magazeti kule Uswisi ilichukua hatua kupitia vyombo vyake vya uchunguzi. Sasa mambo mengine siwezi kuyasema sana na vyombo hivi vya uchunguzi viliniomba mimi kwa mujibu wa sheria ya Mashirikiano katika Masuala ya Jinai yaani *Mutual Assistance in Criminal Matters,* ninayo madaraka kwenye sheria hiyo ya kuiomba mamlaka ya Uswisi inayofanana na mamlaka yangu itupe taarifa kuhusu machapisho ya gazeti hilo. Barua hiyo ilipelekwa Uswisi kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Nchi za Nje kama ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata majibu haya kwamba tunahitaji kutaja mtu mmoja mmoja, kwa sababu gazeti lile halikuanisha, kutaja mtu mmoja mmoja na kueleza sheria ipi imevunjwa na uchunguzi gani unafanywa dhidi ya mtu huyo. Tukaambiwa mamlaka ile inayofanana na yangu haiwezi kuruhusu uvuaji yaani *fishing* ya taarifa hizo kwa sababu hilo ni jambo ambalo linahusu nchi nyingine hatuwezi kuwapeleka gerezani. Kwa hiyo, wakatwambia na nitasoma hapa, inanishinda kwa sababu taarifa zingine bado ni za kiuchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo ni ya sheria ya kwao, yanasema:-

*"The object of the following proceedings and the ground for the requesting authority must demonstrate a connection between foreign proceedings and measures that it requesting. The desired measures should be described in as much details as possible. Consequently a request that is simply fishing for evidence that might be available in Switzerland could be denied. Switzerland will not accommodate request which without providing further details seek to establish whether or not a person subject to proceedings abroad holds bank accounts in Switzerland. If a measure relates to funds suspected to be of criminal origin the requesting authority must state the number or at least the exact address of the bank where the account is presumed to have been opened. The requesting authority must demonstrate the link between this account, the funds there in and the offence committed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya mimi kupata taarifa hii na kwa utumishi wangu uliotukuka, nilichukua hatua mara moja kuvijulisha vyombo vinavyohusika na jambo hili ambavyo ni TAKUKURU ya kwetu pamoja na mamlaka nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge mmetunga sheria hapa kuiunda, *Financial Intelligent Unit*. Kwa hiyo, jambo hili kwa kweli Serikali haijalala na Mheshimiwa Zitto niliongea naye lakini bahati mbaya akawa na tatizo Jimboni, anipe hizo taarifa na kwa utukuka wangu nitazipatia mamlaka zinazohusika kusudi tuweze kukidhi haya matakwa yanayotakiwa hapa na sisi wenyewe pia watu wengine wanatuomba tutoe ushirikiano kwa watu wanaotuhumiwa nje na sisi tunawapa *information* hizihizi kwamba hatuwezi kuwapa mpaka mtupe a,b,c,d kwa sababu ndiyo utaratibu wenyewe wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatarajia katika wakati mwafaka kupendekeza mabadiliko katika hoja ya ndugu yangu Zitto Kabwe, lakini naomba kusema kwa hakika mambo yote ambayo yanasemwa sisi hatujakaa kwa kusinzia. Yako mambo mengi ambayo sheria inaturuhusu kuyafanya na yako mambo mengi ya upelelezi ambayo yanahitaji kuwa

mwangalifu, siwezi kuyasema hapa kwa sababu orodha hiyo ambayo Mheshimiwa Zitto Kabwe anayo katika ile nanii ya kwanza hatukuwa nayo kwa sababu yale magazeti hayakutaja majina ya watu. Kwa hiyo, *addresses* za hizo benki hazipo na watu wenyewe hatuwajui mpaka leo na tukiishawajua kazi itafanyika mara moja. Kwa hiyo, wakati mwafaka kwa lengo lile lile ambalo nimeliona mwanzoni pale, mimi mwanzoni nilitaka kusimama nilete suala la Katiba, lakini ukasema tuzungumze kwa sababu haya ni masuala makubwa sana ya uhai wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakushukuru sana, lakini kama nilivyosema turuhusu mjadala uendelee na wakati ukifika nitapendekeza marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kessy!

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia kuhusu hizi fedha zinazotoroshwa. Hii ilikuwa ni kazi ndogo kabisa, ni kwenda Umoja wa Mataifa kuzungumzia suala hili, nchi za Kiafrika zote ziungane pamoja maana yake siyo Tanzania tu, Nigeria kila mwaka zinaibiwa Dola bilioni 400, acha Tanzania tunaibiwa fedha kidogo. Ni kwenda Umoja wa Mataifa kuomba hawa wafadhili wetu Wazungu ambao tunakwenda kuwapigia magoti kila mwaka kutufadhili barabara, dawa, fedha za Ukimwi, wakati fedha zetu zinachukuliwa kwenda hukohuko kwao Ulaya kwenda kuwanufaisha Wazungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili siyo jambo la kupuuzia. Nchi yetu ni tajiri, hii ripoti imeonesha kwamba Tanzania ni tajiri inaweza kukopesha nchi za jirani, mpaka nchi kama za Ugiriki, Ureno, Usipanyiola (Hispania) na tukabaki bado tuna fedha. Leo Tanzania tunadaiwa Trilioni 20 wakati tuna fedha nyingi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo zilizotajwa hapa ni baadhi tu ya fedha, lakini zilizotoroshwa nje labda ni mara nne au tano zaidi. Hata zinazoibiwa humuhumu nchini ambazo zinajenga magorofa Dar es Salaam, Mwanza, Tabora na wapi, hizo ni kidogo nazo vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa kama kuna utata kwamba mpaka yajulikane majina, tuwabane hao Wazungu wafadhili. Imekuwa hawa kama wanatuchezea mpira, leo tukawapigie magoti, wanatudhalilisha sisi watupe fedha kwa riba wakati fedha zetu ziko Ulaya zinakaa kwa riba vilevile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kodi aliyopendekeza Mheshimiwa Zitto ya asilimia 0.5 ni ndogo sana, sheria iseme asilimia thelathini (30%) kama wananchi wa Tanzania wanavyolipa kodi hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipe asilimia 30 ya fedha hizo ambazo ziko nje na waulizwe kwanza. Mimi nilisema tangu mapema adhabu kali hizi tukizileta hapa wataogopa. Muibaji anaiba hizo fedha, ndugu zetu wanakufa kwa kipindupindu, maji machafu lakini mtu anaiba fedha ambazo ni bajeti ya hospitali nzima anapeleka Ulaya, watu wanakufa huko kwa magonjwa nyie mnasema kuua siyo haki za binadamu, ila kuiba fedha za hospitali ndiyo haki za binadamu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ya kifo na makaburi kuwekwa pingu, iletwe tuipitishe hapa Bungeni na huyo mtu atakayekataa ni fisadi. Kwa hiyo, lazima adhabu kali iwekwe na wataogopa kama vile Uchina. Nchi itaendelea, kuombaomba mpaka lini? Ni aibu, leo fedha yetu ndugu yangu inakuwa shilingi 1600 ndiyo sawa na dola moja. Sawa na Rwanda hawana

chochote, juzijuzi wametoka kupigana vita, sawa na Burundi hawana chochote ni kahawa tu, sisi tuna kila kitu katika nchi yetu hii, tuionee huruma, viongozi oneeni huruma nchi yetu hii, hali ni mbaya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mchango zaidi ya hapo. Tuunge mkono hoja, twende Umoja wa Mataifa kwa nia moja tukaombe Wazungu kule wote walioiba fedha, fedha zetu zirudi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba nimwite Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE: TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi naomba nichangie hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kurudi nyuma kidogo katika historia ya nchi yetu na nisema kwamba kwa mara nyingine tena *Meremeta Limited* Inatajwa ndani ya Bunge lako Tukufu kwa kuhusika na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2007 ilizungumzwa humu Bungeni na baadaye *Meremeta Limited, Tangold, Deep Green* na makampuni mengine hewa yaliyoanzishwa kwa ajili ya kuiba fedha za Serikali yamekuwa yanatajwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu makampuni haya, lakini vilevile waliokuwa wanayaongoza makampuni haya katika hicho kipindi ambacho *Meremeta Limited* ilikuwa inachotewa fedha, Mwenyekiti wa Bodi yake ya Wakurugenzi alikuwa mtu anaitwa Daudi Balali, Gavana wa Benki Kuu. Wajumbe wengine wa Bodi walikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Andrew Chenge, wengine walikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Grey Mgonja, Vincent Mrisho na wakubwa wengine wa Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari imekuwepo katika *public domain* kwa miaka mitano au zaidi hatua hazijachukuliwa. Hatua hazijachukuliwa sio kwa sababu hakuna sheria, hatua hazijachukuliwa kwa sababu nani atakayemchunguza mchunguzi, nani atakayemlinda mlinzi, wanaotakiwa walinde sheria, waliotakiwa kuwashughulikia wao wenyewe wanatakiwa washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimemsikia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akisema kwamba haya masuala ni ya kisheria na mimi sipingani naye, lakini suala la kimsingi ni dogo sana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali yake ndio kwanza wanajua haya leo! Ndio kwanza wanagundua kwamba haya masuala ya wizi na utoroshaji wa fedha za umma yanahusiana na hizi sheria nyingi alizozitaja! Kama jibu lake ni ndio maana yake ni kwamba amekuwa anafanya kazi gani ya Uanasheria Mkuu miaka yote hii? Kama jibu sio au kama jibu ni kwamba walikuwa wanajua mambo yote haya miaka yote hii, suala ni kwamba hoja yake hii ya sasa lengo lake ni nini kama sio kuua hoja hii ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ili walioiba na kuficha fedha nje ya nchi waendelee kula pesa za wizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, si fahari kuwa na Serikali ambayo watendaji wake wanahusishwa na wizi, sio fahari. Bunge hili lina wajibu angalau kwa mara ya kwanza ya kusema kwamba si fahari kwa Serikali yetu na watendaji wake kuhusishwa na ufisadi na kama si fahari, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili na hasahasa Wabunge walio wengi wenye uwezo wa kupitisha maamuzi haya kwa sababu ya wingi wao, watimize wajibu wao, waunge mkono Azimio hili ambalo Mheshimiwa Kabwe Zitto amelileta. Sisi upande huu tuko wachache, peke yetu hatutaweza, lakini kama hamtaunga mkono na walioiba wakaendelea kukaa na mali ya wizi, hiyo dhambi ya kutotimiza

wajibu itakuwa upande huu. Hiyo dhambi ya kuangalia upande mwingine wakati fedha za umma zinaibiwa itakuwa sio dhambi ya sisi wachache itakuwa dhambi ya wale waliokuwa na uwezo wa kuizuia hawakuizuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lina wajibu Kikatiba wa kuisimamia Serikali na kupitisha Azimio la kuchunguza uchafu huu ni sehemu ya Bunge hili kutimiza wajibu wake Kikatiba wa kuisimamia Serikali. Kwa uzoefu kwa hii miaka michache tangu haya matukio makubwa ya ufisadi yameanza kujitokeza ushahidi uko wazi. Serikali ikiachiwa iendelee kwa taratibu zake anazozisema Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuna litakalofanyika, tusidanganyane. Kwa namna ninayoiona, namna ya kuifanya Serikali iwajibike, ichukue hatua ambazo haijazichukua miaka yote hii, ni kwa Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili kuunga mkono hili Azimio kama lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mapendekezo ya mabadiliko ya hoja hii yaliyoletwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa Serikali pamoja na kwamba hajayasaini, lakini kama haya yatakubaliwa hili Azimio litakuwa limeuawa. Haya mapendekezo lengo lake ni kuua hoja ili wezi waendelee kukaa na *proceeds of crime*. Nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, tafadhalini tukatae kutumiwa kulinda wale ambao wanahujumu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nitamwita Mheshimiwa Ole-Sendeka na msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mpina.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Chama cha Mapinduzi tulikula kiapo siku ya kuchukua uanachama wa chama chetu, moja kati ya ahadi tulizozitoa ni kusema “Rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa”, “cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu”, “nitasema kweli daima, fitina kwangu ni mwiko”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii tukumbushane kwamba lengo la Serikali hii ambayo leo iko mikononi mwetu ni ustawi wa Watanzania. Ustawi wa Watanzania unakuja pale ambapo tuliopewa dhamana tutakuwa tunatimiza wajibu wetu wa kusimamia rasilimali za nchi yetu kwa faida pana ya maslahi ya Taifa letu kwa ujumla wake. Pale ambapo maslahi ya nchi yatawekwa pembeni na ubinafsi kupewa nafasi ya kutawala ndio kwamba Taifa la aina hiyo uhai wake unaelekea kwenye safari ya kifo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa hoja ya msingi aliyoitoa hapa ya kuhoji juu ya fedha zilizoko nje ya nchi. Najua kwamba wapo Watanzania wenye shughuli zao halali wanaomiliki akaunti zao katika nchi nyingi tu duniani kwa utaratibu na kwa mujibu wa sheria, fedha halali kabisa, hao hatuna tatizo nao. Mimi nasema hao hatuna tatizo na Mheshimiwa Zitto, mtoa hoja amesema hana tatizo. Ninachotaka kusema, haiwezekani ikawepo tuhuma kubwa ya aina hii tena ambayo inanyoosha vidole kwa watu wenye dhamana kubwa kwa nchi, maana hii ni mara ya pili hoja hii inazungumzwa hapa ndani ya Bunge na mimi nikasimama hapa kuomba mwongozo wa kutaka mtoa hoja wakati huo alikuwa Mheshimiwa Kabwe Zitto ataje majina ya watu wenye akaunti hizo za fedha ambazo hazikufuata utaratibu huko Ughaibuni au Serikali isaidie kusema ni kina nani ambao wana fedha huko nje. Kwa bahati mbaya sana, kuna hoja yangu ambayo niliitoa kwenye mkutano uliopita wa Bunge, Bunge lilifika mwisho wake na tukaahirisha Bunge bila ya kupata majibu. Imani yangu leo lazima umadhubuti wa Serikali uonekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata maelezo ya *Attorney General* hapa lakini haitoshi, kwa maoni yangu haitoshi lazima tufike mahali. Hoja ya mtoa hoja, ukurasa wa tatu inasema hivi, naomba kununukuu:-

*"Kitendo cha Serikali kukaa kimya bila kuchukua hatua kinaashiria ama kutotimiza wajibu au kwamba wanaopaswa kuchukua hatua ni washirika wa utoroshaji huo wa fedha za nchi na kuzificha katika mabenki ya nje".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukakaa hapa fedha zikaweza kutoroshwa na yakatokea maneno haya hata kama maneno yenyewe bado hakuna ushahidi, Serikali yenye vyombo vya ulinzi vya dola mpaka leo isiwe na jina la mtu yeyote ambaye anahusika na fedha hizo haramu nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, ziko fedha ambazo hatuwezi kunyamaza. Niliwahi kusema kwenye Bunge la Tisa kwamba nitalisema jambo hili katika kipindi cha uhai wangu na wenzetu Waislam wanasema ukiliona jambo ovu liondoshe, kama huwezi kuliondosha lishtakie na kama huyo unayemshtakia hataki kuondosha endelea kulinyooshea kidole mpaka atapotokea mtu wa kuliondosha. Nataka niwaambieni ndugu zangu tunaweza kujinasua katika uchafu huu pale ambapo tutajipambanua na kusema wanaohusika na uchafu huu ni hawa, wanaohusika na *Deep Green Finance* wako hai, wana vyeo, wako kwenye nchi hii na wanaendelea kulindwa. Waliohusika kwenye kashfa ya *RICHMOND* na *DOWANS* wamepandishwa vyeo wako kwenye Serikali hii, hatuonyeshi hasira dhidi yao. Waliohusika kwenye KAGODA, wana vyeo, wako humu ndani wengine na bado wanaendelea kubaki kwenye vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaelezeni msingi wa fedha haramu, kazi yake ya kwanza ni kupiga kabali demokrasia na mtashangaa na dhambi hii itawatafuna wote haijalishi CHADEMA, haijalishi CCM. Mkiwa na fedha haramu, fedha haramu haiwezi kufanya jambo jema, itafanya jambo ovu. Mtakwenda kwenye chaguzi za vyama vyenu mtawekewa viongozi kwa fedha haramu na manung'uniko yapo na Waswahili wanasema, "Lisemwalo lipo na kama halipo laja". Hamwezi kuendelea kukaa kimya, mnaziba masikio wakati fedha haramu zinaonekana zinazunguka na watu wanaendelea kupata madaraka kwa fedha haramu, Taifa la aina hiyo linaelekea kwenye kifo chake. Nataka niwaambieni ndugu zangu kama kuna hoja ambayo haipaswi kufanyiwa marekebisho, nami nataka kusema acheni utani, kama kuna hoja ambayo haihitaji kufanyiwa marekebisho na kama mnarekebisha ni kwa nia ya kuboresha na sio kwa nia ya kuiweka pembeni**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwaambia wakubwa zangu wakati fulani kwamba kama wewe ni kiongozi wa juu wa chama hiki, lakini wewe watu wanakunyooshea kidole, wakati fulani nikasema ni afadhali tuunde Tume, tukuchunguze, wewe ukithibitika ukaangalia ng'ombe zako na rafiki yako huyo anayetuhumiwa naye akithibitika amefanya biashara zake, nataka kusema na narudia kusema mbele ya Bunge hili tuunge mkono hoja hii na kama ni kuunda Kamati Teule mimi naunga mkono na kama ni kuomba tukutane na Balozi zote zilizoko Tanzania tuwaalike tuzungumze nao mambo haya yawe bayana wanaoiba fedha hizi wazirejeshe, tuwachukulie hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, hivi kuna dhambi gani kwa nchi hii maana mimi nataka niwaambieni ndugu zangu, katika Mkutano uliopita kuna hoja moja tulikuwa tunaizungumzia hapa ya utaratibu wa Sheria ya Manunuzi ambapo mtu mwenye akili zake, mwenye dhamana, *Accounting Officer* anachukua fedha za Serikali shilingi bilioni 13 hafuati Sheria ya Manunuzi anakwenda kufanya manunuzi kama ananunua shati au pete ya

kumpelekea mkewe na watu wanapiga makofi wanasema eti huo ndio uzalendo, uzalendo ni wa aina gani usiozingatia sheria! Ukomo wa uzalendo na dhamira inaanzia pale unapoanza kuvunja sheria na taratibu ambazo nchi ya watu wazima wamejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Zitto na nategemea nitaunga mkono mabadiliko yoyote yenye kuhakikisha jambo hili linafikia hatma yake iliyo njema. Ni mara ngapi tumesikia watu waliokuwa wanahusika kwenye kashfa za *EPA*, pamoja na wengine wamepelekwa, wengine bado hawajapelekwa, hao mnawaacha kwa nini? Lakini sio hivyo tu, baadhi ya hao mliowapeleka asubuhi yake, makampuni yake mnayapa tenda za Serikali, unampaje adui yako tena silaha ya kukupiga? Mimi nataka niwaambieni ninyi mlioko kwenye *front bench,* itendeeni nchi hii haki na mimi namwambia Mheshimiwa Zitto kama ana majina ayataje. Mimi nasema ayataje, amtaje huyo, kama ni watoto wa wakubwa semeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofedhehesha katika siku za karibuni katika Bara la Afrika na katika nchi zetu, ni kuona kwamba ama wakubwa wenyewe katika Serikali wana akaunti nononono huko Ughaibuni au watoto wao wana akaunti, ghafla mtu ambaye alikuwa hana hata kibanda cha kuuza maandazi, hana kibanda cha kuuza chochote, anakuwa milionea. Katika nchi inayojiheshimu na nchi inayojali ustawi wa watu wake, ni lazima wawaone wale watu kama ukoma, iwaogope na iwashughulikie kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwaambieni ndugu zangu na hili wote tuungane msilete siasa. Kama walioko mbele kuna yeyote anayehusika, kama ni Mawaziri Wakuu wa zamani, kama ni walioko leo, kama ni waliowahi kuwepo, wasemeni tusaidiane wote. Tuwafichue, watajwe, washughulikiwe, wakaangalie mashamba yao na tuwapeleke gerezani wale ambao wanastahili kupelekwa gerezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, ninaunga mkono hoja na naliomba Bunge hili liwe moja katika hili na tusitende dhambi hata kidogo, dhambi hiyo itawatafuna mwaka 2015. Fedha hizo haramu zitakuja kwenye Majimbo yenu, itawaondoa na mimi nawaambieni haijalishi itikadi. Kama ni upande wa Upinzani semeni, wako wengine wanatajwa wana nyumba zao huko Dubai, wengine wanatajwa wana akaunti zao huko Ughaibuni, kwenye mitandao inaonekana, nataka niwaambieni haitajalisha wewe ni kiongozi wa Kambi ya Upinzani, wewe ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri, wewe ni Rais wa nchi hii, wewe ni mtoto wa mkubwa yupi, tukithibitisha kwamba unazo fedha haramu, Bunge hili litaondoa kinga yoyote ile na tutakuburuza Mahakamani ili haki iweze kutendeka. Nataka niwaombe Wabunge wa Bunge hili itendeeni nchi hii haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto na jambo hili naiomba Serikali iwe wazi, tusaidieni kama hamwezi kuwataja hao watu vyombo vya ulinzi tulivyonavyo waondoeni wote, hamwezi kukaa na vyombo ambavyo vinatumwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, kengele ya pili tayari, ujumbe wako umesikika vizuri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Aaah! Imezimika? Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ya kwangu ni hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimwite Mheshimiwa Mpina, lakini ninajaribu kufanya hesabu ya muda kuruhusu. Naomba Waheshimiwa Wabunge, hizi semina za kanuni naona bado hazitusaidii sana. Ninasema hivi, nafikiri muwe tu na nidhamu kidogo ya kusikiliza. Nimesema hivi, nilisema msemaji wangu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mpina. Ninaangalia muda wangu Mheshimiwa Mpina atatufikisha mpaka saa 1.30, atatumia kama dakika 15.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize, Mheshimiwa Mpina atatumia dakika zake za kikanuni kuzungumza. Kwa hali hiyo, hatutakuwa na muda wa kutosha kumpa Mheshimiwa *AG* kuileta hoja yake ya mabadiliko ili ijadiliwe. Kwa hali hiyo, naomba mnisikilize, kwa hali hiyo, nitaongeza tena mchangiaji mwingine mmoja kusudi hoja hii tuweze kuendelea nayo kesho ama kwa mwongozo wa Mheshimiwa Spika, ama kwa kadri ya Mheshimiwa Spika atakavyotuongoza kusudi tuweze kuimaliza kwa utaratibu muafaka zaidi. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Mpina na katika orodha yangu hapa nitamwita Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Lakini vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa hoja yake hii binafsi ambayo ameiwasilisha hapa. Lakini vilevile niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine waliozungumza hapa bahati nzuri au mbaya kwamba Mheshimiwa Zitto amekuwa na maneno mengi mazuri ambayo ameyaongezea kwenye hoja yake hii binafsi, lakini kwenye vitabu hivi hayapo. Sasa maneno hayo kwa sababu Mwenyekiti uliyakubali Mheshimiwa Kabwe Zitto akayasoma wakati hayapo kwenye vitabu basi ni vizuri zaidi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, nimekupa nafasi ya kuchangia hoja na sio kufanya mabadiliko.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ndio nachangia Mheshimiwa Mwenyekiti. Ninachokisema mwisho wa siku Mheshimiwa Kabwe Zitto lazima tuboreshe hoja yake aliyoiwasilisha lakini kuna maneno aliyoyazungumza ambayo hatukuweza kuyakamata wakati anayasoma kwa sababu kwenye vitabu hayapo. Kwa hiyo, hoja yangu ni kwamba kwa sababu uliyaruhusu maneno hayo ya Mheshimiwa Kabwe Zitto basi ni vizuri pia yaletwe kwa maandishi ili tujue wakati tunaboresha hoja yake tunaboresha nini kwa sababu hayapo humu kwenye vitabu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, itakumbukwa katika Bunge la Nane nilisimama hapa Bungeni nikawasilisha taarifa nne za watafiti. Taarifa ya *Global Financial Intergrity Report* ya mwaka 2008 ambayo na Mheshimiwa Kabwe Zitto amei-*cite* katika ripoti yake ambayo inaonyesha kwamba Tanzania ilipoteza katika kipindi hicho cha miaka 38 shilingi milioni 3,356.4 ambapo ni sawa na shilingi trilioni 11.6. Nikawasilisha kitabu kingine, utafiti mwingine wa Ndikumana na Boyce wa mwaka 2008 vilevile wa kutoka mwaka 1970 mpaka 2004 ambao Tanzania ilipoteza USD milioni 5,185 ambayo ni sawa na shilingi trilioni 8.2. Lakini ripoti ya Karl na Katwith Smith ya mwaka 2008 ambayo vile vile inaonyesha Tanzania ilipoteza shilingi trilioni 10.4 kwa utoroshaji wa fedha nje ya nchi. Lakini na ripoti ya nne niliyoiwasilisha ilikuwa ni ile ya *One Billion Dollar Question* ambayo inaonyesha kwamba Tanzania kila mwaka imekuwa ikipoteza bilioni 478. Pamoja na ripoti ile ya Benki za Uswisi ambayo inaonyesha ni zaidi ya bilioni 300 zinamilikiwa na Watanzania huko katika mabenki, nikaiomba Serikali na nikasema kwamba kwa muda mrefu taarifa hizi zimekuwa zikisemwa lakini Serikali imekuwa ikisema haina taarifa hizi, nikaona niziwasilishe ili kwa maana ya kuondoa utata kwamba Serikali haina taarifa hizi ili iwenazo sasa. Lakini vilevile kuiwezesha Serikali kuchukua hatua ya mafedha haya ambayo yanaripotiwa na taasisi mbalimbali pamoja na benki mbalimbali hapa nchini ili kwamba Serikali iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa ninasema rasmi kwamba hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe imekuja muda mwafaka wa kuitaka sasa Serikali leo iweze kuchukua hatua za makusudi za watu wote ambao wameficha fedha nje ya nchi kuweza kuzirejesha. Fedha ambazo zinatajwa Uswisi ni baadhi ya fedha tu ambazo zimefichwa na watu wanaohujumu taifa hili, ni mfano wa fedha zilizofichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama alivyoandika Mheshimiwa Zitto Kabwe hapa ametaja kwamba mabilioni ya fedha, sio mabilioni ya fedha ni matrilioni ya fedha zilizoibwa na kwenda kufichwa nje ya nchi ambazo zingeweza kurejeshwa zingewezesha taifa hili kupiga hatua kubwa sana katika maendeleo na mimi nasema kwamba Wabunge wote kwa kauli moja tutafanya marekebisho kwa muda mwafaka kama nilivyosema kwamba hata marekebisho tuliyokuwa tunafanya yamevurugika kulingana na maelezo yaliyoongezwa, tutafanya marekebisho mengine ya kurekebisha vizuri hoja hii ili isije, kwa baadaye yanaweza yakaharibu tena utaratibu mzima wa nchi hata wa uwekezaji. Kwa hiyo, mimi binafsi nitaleta mapendekezo ya kuona kwamba hoja hii inaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi napata taabu sana. Hili suala linanipa matatizo sana, kwamba ni Mawaziri wa Serikali hii waliweza kusimama na kutamka kwamba watu walioficha fedha nje ya nchi wanawafahamu kwa majina lakini wale Mawaziri hawakuweza kutaja yale majina mpaka leo licha ya Serikali kusema kwamba inawajua watu hawa. Lakini Mheshimiwa Zitto Kabwe pia nilimsikia wakati tunazungumza na anatoa hoja hii, mimi bahati nzuri sikuwa na majina lakini mwenzangu akasema anayo majina kwamba anawafahamu watu walioiba na kuficha fedha hizo nje ya nchi. Sasa leo hoja ya Mheshimiwa rafiki yangu sana Zitto Kabwe inaisha na yeye hajasema hao watu walioiba hizo fedha na kuficha nje ya nchi ni akina nani? Kwa hiyo, napata mgogoro mkubwa kwamba ni kwa nini hawa watu wasiweze kutajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi niseme ninyi ni viongozi ambao mmekula kiapo, mmeapa, Mheshimiwa Membe nakutaja kwa jina ulisema kabisa kwamba hawa watu unawajua na sikujua sababu zilizokukwamisha usiwataje, muwataje mlishakula kiapo mlisaidie taifa. Mheshimiwa Zitto Kabwe wasemeni hawa watu hata kama ni viongozi wakubwa wenye nafasi za aina gani hapa duniani au hapa Tanzania watajeni. Ukifa leo dunia itakukumbuka kama unasema ukweli. Kuna sababu gani ya kuzificha taarifa ambazo mna uhakika nazo halafu mnaendelea kuzunguka? Mheshimiwa Zitto Kabwe unazunguka na hoja binafsi hapa, tungependa hoja binafsi uliyoileta tuanzie na majina unayoyafahamu, uchunguzi tuanzie hapo. Kwa nini unazunguka unasema *Deep Green* wakati unajua majina ili tuanze na hayo majina, tuwachunguze hao. Mimi Mpina nasema siogopi chochote hapa duniani, siogopi chochote hapa duniani, ningekuwa mimi ninayo majina ningeyasoma leo dunia ikasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mnazunguka, wataje watu hawa mnaowafahamu ili tuanzie hapo, tusizunguke, tusianze na Tume, tuanze na hawa. Kwa sababu majina kama tunayafahamu, tutahangaika na Tume hizi mwishoni zitatuingiza gharama kubwa, tuanze nao hawa ili tuweze kurejesha hizo fedha kwanza walizozificha halafu sasa hata kama tunaunda Tume tuunde Tume wakati baadhi ya fedha tumeshazirejesha na hizo ndizo zitakazosaidia kufanya uchunguzi.

**T A A R I F A**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Mpina, naomba uketi kuna taarifa. Mheshimiwa Nassari taarifa kwa mujibu wa Kanuni gani?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8). Naomba kwa sababu ya muda nisiisome au kama ukitaka niisome nitaisoma.

**MWENYEKITI:** Nafikiri usipoteze muda, hebu nenda tu kwenye taarifa yako.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mpina kwamba ukiisoma vizuri hiyo hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe inasema kwamba inashawishi Bunge liunde Kamati na Mheshimiwa Zitto Kabwe anasema wazi kabisa kwenye hoja yake kwamba zipo taarifa nyingi alizonazo ambazo asingeweza kuzitoa hapa lakini atakuwa tayari kuzitoa kwenye Kamati itakayoundwa. Pengine taarifa hizo ni pamoja na majina yaliyopo na ameeleza wazi kwenye hoja na mengine amesema kwa sababu ya usalama wa nchi.

**WABUNGE FULANI**: Ayataje!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Acheni kuzomea, mnamzomea...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari, wewe ongea na Kiti.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wanaozomea najua ndiyo haohao waliotajwa huku na mnataka kuwa wakubwa wa nchi. Sasa niseme tu kwamba Mheshimiwa Zitto kwenye hoja yake amesema wazi kwamba kuna taarifa nyingi nyeti alizonazo ambazo akizitoa sasa hivi pengine sio vizuri kwa usalama wa nchi lakini endapo Kamati itaundwa, atakuwa tayari kuzitoa kwa Kamati. Kwa hiyo, kimsingi Bunge liridhie Kamati iundwe, Mheshimiwa Zitto apeleke nyaraka kwenye Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Umemaliza?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kusema, *why do we need to go for John the Baptist while Jesus is there.* Mheshimiwa Zitto anataka kwenda kwa *Jesus straight* iundwe Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari sasa sijui taarifa unayotaka kumpa Mheshimiwa Mpina ni ipi kwa sababu ungejielekeza moja kwa kwenye taarifa. Sasa badala ya kuwa na taarifa ambayo inakwenda moja kwa moja na wewe unahama kwenye taarifa yako nzuri uliyotaka kuisema. Kwa hiyo, naomba nimruhusu Mheshimiwa Mpina aendelee.

Mheshimiwa Mpina, kuna Mheshimiwa mwingine kasimama. Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa ya ziada kwamba...

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni gani Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(8) hiyohiyo. Nilikuwa napenda kumpa taarifa mdogo wangu Mheshimiwa Nassari kwamba, kinachosemwa hapa kwa Mheshimiwa Zitto ndani ya Bunge hili, anachosema Mheshimiwa Mpina ni kwamba ndani ya Bunge hili kuna utaratibu, maana utakaowapa taarifa wajumbe wa Kamati Teule ni Wabunge wanzako wachache lakini

wenzako tunapenda wote hapa, badala ya kuunda Kamati Teule chukua hayo makaratasi weka mezani pale, badala ya kusubiri watu wachache ukawape kazi ya kusoma makaratasi yenye majina mazito, weka mezani pale, ndiyo utaratibu wetu. Kama kuna mtu anazo taarifa zozote anaweka mezani pale. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Zitto weka mezani pale zisomwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hizi taarifa nashindwa kuzipima zaidi naona wote taarifa zao ni kama vile wanachangia hoja hii. Mheshimiwa Mpina naomba uendelee!

**MHE. LUHAGA J. MPINA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa aliyonipa mdogo wangu mimi nadhani hakunielewa ninachokizungumza. Lakini taarifa aliyotoa Mheshimiwa Lukuvi ni kama tu ameanza kuiba mchango wangu hapa ambao nachangia, lakini namshukuru. Ninachosema mimi nikisimama hapa niko *firm,* kama nina *document* yoyote hapa mezani ambayo inathibitisha maneno haya ninayoyazungumza sihitaji tena kwamba nisubiri mpaka Kamati ya watu wachache nikaonyeshe *documents* hizo. Leo ningekuwa mimi zile *documents* anazozungumza Mheshimiwa Zitto Kabwe ningezikabidhi rasmi, Wabunge wote wakaziona na hatua zikaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge lako ni la viongozi ambao wamekula kiapo kwa kushika Quran na wengine Biblia. Mimi nadhani kwamba hata wanapofikia kwenye maamuzi ambayo Mheshimiwa Zitto Kabwe anayataja, hizo *documents* tugawiwe ili twende tukaidhinishe vizuri haya maazimio yake ambayo ameyaweka na tuwe na uhakika kabisa na tunaposema tunaunda Tume tuwe na uhakika wa kutosha na *document* zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hawa watu walioiba fedha za Watanzania, taifa maskini linaendelea kuwa maskini sana kwamba tuwasake popote walipo, tusake popote fedha walipoficha ili tuhakikishe kwamba fedha zetu zimerejeshwa hapa nchini na Watanzania wamenufaika na fedha za watu walizozitorosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taratibu nyingi za kurejesha fedha na kama ambavyo amezungumza yeye mwenyewe lakini Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuliyenaye anao uwezo wa kuomba *document* yoyote katika mamlaka yoyote katika nchi zilizopo duniani na kupewa. Kwa hiyo, pia jukumu la Serikali kuendelea kuhakikisha kwamba zile fedha za Watanzania zilizoonyeshwa kwenye tafiti na tulizoonyeshwa na mabenki zote zinathibitishwa zilipo na zifuatiliwe na ziletwe Watanzania waweze kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba kwa sababu maneno mengine yamesemwa na wenzangu sihitaji kurudia kwamba Mheshimiwa Zitto Kabwe afanye mambo yafuatayo:-

(i) Asome majina yote ya watu waliioficha fedha nje;

(ii) *Documents* zote alizonazo amkabidhi Mheshimiwa Spika ili tuweze kuziona;

(iii) Hayo maelezo ya Mheshimiwa Zitto Kabwe tulikuwa tunafuatilia mstari kwa mstari, kuna maelezo mengi ameyaongeza, kwa hiyo, tunashindwa hata namna ya kuboresha hotuba yake. Hayo maelezo pia ambapo ni ya nyongeza, yaongezwe ili wakati tunashauri tujue tunashauri kitu gani na Serikali ichukue mkondo wake wa kuhakikisha kwamba fedha za Watanzania zilizoibiwa zinarejeshwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Lugola!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mwakyembe amepiga marufuku abiria wasichimbe dawa wanapokuwa wanasafiri. Leo Bunge hili ninaomba tumruhusu Zitto Kabwe achimbe dawa ya muarobaini kwa ajili ya kuangamiza mazalia na maficho yote ya mafisadi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Majimbo yenu hayana maji kwa sababu ya fedha zinazofichwa na mafisadi hawa. Majimbo yenu, zahanati hazina dawa, watu wanakufa kwa sababu ya fedha hizi zinazofichwa na mafisadi, Majimbo yenu watoto wanakaa chini, Walimu hawatoshi kwa sababu ya fedha hizi zinazofichwa na mafisadi. Kila siku tunalia tuwe na barabara za lami, tuwe na umeme vijijini hatupati kwa sababu ya fedha zinazofichwa na mafisadi hawa kwenye nchi za nje. Nawaomba Wabunge wenzangu tuache ushabiki wa kusema majina yako wapi, tuache ushabiki wa kusema ushahidi uko wapi, tuache ushabiki wa kusema kwamba Mheshimiwa Zitto Kabwe lazima aweke zile nyaraka mezani leo. Tukiyasema maneno hayo Waheshimiwa Wabunge tutaligawa Bunge hili na nina hakika hatutawaondoa mafisadi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala alilozungumzia Mheshimiwa Zitto Kabwe anaomba Kamati Teule kwa ajili ya uchunguzi. Mimi ni *professional* katika uchunguzi, naomba niwape maadili katika hili. Ukikuta bastola imeangukia kwenye tukio la ujambazi bila kumjua mwenyewe, hautaacha kufanya uchunguzi. Itabidi uchunguze bastola ile na ndipo utaweza kumbaini nani anamiliki bastola ile. Leo Mheshimiwa Zitto kaleta ufunguo, mahali pa kuanzia, nchi hii itapata unafuu na itapumua. Naomba tuchukue mambo yote ambayo Zitto leo ameyafungua ili Kamati Teule ianzie pale kwa sababu akaunti hizi zinafahamika ziko nchi gani ndipo wenye majina watakapofahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naamini kwamba Bunge hili yupo mwenzetu Mheshimiwa Membe aliwahi kusema na mimi nikamsikia kwamba anawafahamu mafisadi hawa, nilijua kwamba tutagawana uzoefu katika Bunge hili. Wapo wanaofahamu majina, wapo wanaofahamu akaunti na wapo wanaofahamu hata sura za mafisadi. Nakuomba Mheshimiwa Membe kama una nia njema na taifa hili...

**MWENYEKITI:** Unakiomba kiti Mheshimiwa!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa sababu mwenzetu aliwahi kusema anafahamu majina haya, kwa sababu ya kutenda mambo mema na kuwaonea huruma Watanzania awe tayari kuwataja watu hawa na sisi Bunge hili litamsimamia tuhakikishe mafisadi hawa tunawashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka na muziki wa mafisadi, mafisadi. Hatuwezi kuondoa ufisadi kwa kuimba nyimbo, hatuwezi kuondoa ufisadi kwa kutamka, tutauondoa ufisadi kwa kutoa tamko ambalo litaruhusu Kamati iundwe ili tuweze kuchunguza ni akina nani hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwona mtu anasimama anasema kwamba kuna vikwazo hivi vya kisheria maana yake wanafahamu mafisadi hawa ni akina nani. Nje ya kutotuambia kuna sheria zinazotuzuia ziko sheria nyingi hapa katika nchi yetu zinapindwapindwa kwa ajili ya kunyoosha mambo. Kwa nini tunataka kunyoosha mambo ya ufisadi tunataka tena kupindisha mambo ya sheria hapa katika Bunge hili. Hao watu wa Uswisi hawatuzuii sisi kuanza kujipanga kwa maana ya kutaka kuchunguza tujue ni akina nani wanaohusika na utoroshaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hatujui vizuri madhara ya fedha haramu. Tuna tatizo kubwa la ukwepaji wa kodi. Watu wana-*declare* mapato yao ni kidogo kila wakati wanalipa kodi kidogo kwamba wanapata hasara lakini hawaachi kufanya biashara wanayoifanya. Lakini baada ya siku tatu unaona wanaotesha majumba, unaona wanaleta magari mazuri ni kwa sababu ya fedha wanazozificha nje kwa kukwepa kodi wanakuja kuzisafisha na kusema kwamba wamepata mikopo au misaada. Tutaondoaje rushwa katika nchi hii? Tutaondoaje rushwa katika chaguzi? Tutaondoaji rushwa katika miradi mikubwa mikubwa ya gesi ambayo sasa tunataka kuhakikisha kwamba nchi hii inapata mapato? Kama leo Bunge hili halitaazimia kwa kauli moja kuhakikisha kwamba hoja ya Mheshimiwa Zitto isipingwe kwa namna yoyote ili mafisadi hawa waweze kushughulikiwa kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Ole-Sendeka katika Bunge la Tisa walianza kushughulika na mafisadi hawa, lakini kwa sababu Bunge liligawanyika, kwa sababu tunashabikia kuomba ushahidi katika hatua za mwanzo, hatuwezi kuondoa ufisadi katika nchi hii; na Watanzania watatuhukumu endapo wanatuchagua kwa kura nyingi kuja kuhakikisha kwamba tunasimamia rasilimali zao, tunasimamia fedha zao halafu tunafika hapa tunaanza kuleta itikadi za vyama, tunaanza kuleta itikadi huyu ninamjua, tunaanza kuleta itikadi za kutetea Serikali, Serikali ambayo ina watu ambao ndiyo wanaiba fedha. Naomba tutenganishe pia kati ya Serikali na watu wanaoiba fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kange, kuna maneno mengine hayastahili kwenye lugha za kibunge. Endelea!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hawa mafisadi ambao walijidhihirisha kwenye *DOWANS, RICHMOND* baadaye wakajidhihirisha kwenye *EPA* baada ya kuona kwamba Bunge hili limekuwa likipata hoja nzuri za kuwashughulikia lakini linagawanyika matokeo yake sasa ndiyo tumekwenda kupata fedha za Uswisi. Leo tutaacha fedha za Uswisi, wameshatuzoea kesho tutapata fedha zingine za Amerika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nashukuru kwamba Wabunge wenzangu njia zote za kuleta fedha haramu katika nchi hii, ni njia ambazo zinafahamika kwa sababu haiwezekani watu wanatoa mamilioni ya pesa kwenye chaguzi halafu mnasema hatuna fedha haramu katika nchi. Haiwezekani watu wanakuwa na fedha nyingi za kutoa kila mahali kwa njia ya michango halafu mnasema kwamba hatujui hizi ni fedha haramu. Fedha haramu zinafahamika, mafisadi tunafahamu kwamba ndiyo wanaovuruga nchi, lazima tuhakikishe kwamba hoja ya Mheshimiwa Zitto ni hoja nzito, ni hoja ambayo haitakiwi kwa kweli Waheshimiwa Wabunge kuipinga kwa namna yoyote ile na yeyote atakayepinga hoja hii mimi nawaambieni nimekwisha kuwa na kifaa kinachoweza kubaini fedha mahali zilipofichwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine wameanza kuchimba mashimo kwenye nyumba wanaficha fedha. Nawaambieni hizo fedha hamtazikuta, nitaanza kupita kila mahali kwa sababu kuna kitu kinatambua pesa. Kwa hiyo, msifikiri kwamba ninyi ni wajanja sana katika mambo ya kuficha fedha, mimi siwadanganyi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester Bulaya hapa asubuhi alituambia kwamba wapo watu wanakuja kinyemela wanajifacha kuoa Tanzania baadaye wanachukua ardhi wanawekeza baadaye wanawafukuza. Lakini mimi nimeshuhudia kuna vijana sasa hivi wa miaka 18 mpaka 20 unakuta ameoa Mzungu wa miaka 70 au 80. Sasa unajiuliza ni penzi tu au kuna kitu kingine cha ziada? Hawa tuwaangalie sana, hawa ndiyo *carrier* wa fedha haramu,

wanazileta hapa nchini. Unakuta vijana wana magari ya kifahari, wana nyumba za kifahari, wanazitoa wapi pamoja na kwamba sisi kule nyumbani tunasema ng'ombe hazeeki maini, lakini hao vijana ni penzi tu kwa huyu bibi wa miaka 80? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhakikishe kwamba sambamba na Azimio hili la Mheshimiwa Zitto Kabwe na mimi nitaleta mapendekezo ya kuboresha kwamba sasa wakati umefika Watanzania kila mahali walipo tuorodheshe majumba na miradi ambayo imekuja kuota katika hali ambayo si ya kawaida ili watu hao pia wachunguzwe sambamba na Kamati hii. Kamati hii iwe na wigo mpana. Tunaweza tukaondoa ufisadi kama tutapeleka mtikisiko mkubwa. Tukienda na katikisiko kadogo, tutachukua vifisadi vidogovidogo halafu yale makubwa tutayaacha. Halafu unashangaa kwa nini tukigusa Meremeta, tukigusa *Deep Green* utaona watu wanaibuka kama nyoka na ndimi mbili; ushahidi uko wapi, ushahidi uko wapi, wataje majina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba uchunguzi si lazima ujue jina la mtu kwa sasa, jina la mtu litabainika baadaye katika uchunguzi. Kwa hiyo, tusilazimishe kwamba bila kuwa na majina hatuwezi kuchunguza, sio maana ya uchunguzo hata kidogo. Mheshimiwa Membe mimi ni rafiki yangu mkubwa, leo ndiyo ninataka nione unadhihirisha kwamba unaweza na unayaweza, leo ndiyo tunataka udhihirishe kwamba hata ukiwa kiongozi mkubwa katika nchi hii wewe ni jasiri. Hatutaki viongozi waoga, tunataka viongozi ambao ni jasiri, ambao hawawezi wakatumbukiza taifa hili kwenye makorongo, leo ndiyo tunataka ututajie majina ya hawa ambao ni mafisadi. *(Makofi/Vicheko/Vigelegele)*

***(Hapa Mheshimiwa Bernard Membe alitoa ishara ya kukubaliana na mzungumzaji)***

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA**: Vinginevyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Kwa kweli siku hii ya leo imekuwa moto. Kiti kimekuwa moto na mambo yote moto. Nina matangazo mafupi. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ananiomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wabunge 113 bado hawajaenda kuchukua alama za vidole kwa ajili ya vitambulisho vya taifa. Waheshimiwa Wabunge, hili ni jambo muhimu sana, ninawaomba wale ambao hawajaenda waelekee kwenye kile chumba ambacho kipo mkabala na ukumbi wa Pius Msekwa wakakamilishe zoezi hilo.

Mheshimiwa Juma Sereweji, anasema anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa amepoteza *ATM card* yake ya NMB pale Benki tarehe saba siku ya jana. Kwa hiyo, anaomba mtu aliyeiona ama kuiokota amsaidie kuirejesha.

Mheshimiwa Hassan Ngwilizi ameleta ombi lake hapa nadhani tutaliwasilisha Ofisi ya Spika ili Kamati yake iweze kukutana hiyo kesho. Mheshimiwa Spika atatoa kibali kama inawezekana. Mheshimiwa Ngwilizi anaomba kibali Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge iweze kukutana kesho saa tano. Kwa hiyo, madaraka ya kuruhusu Kamati hiyo ikutane yapo kwenye mikono ya Mheshimiwa Spika atawapa majibu na ataruhusu kama inafaa.

Kuna taarifa ya kikao pia. Uongozi wa Bunge *Sports Club* mnaarifiwa kuwa kutakuwa na kikao cha dharura cha Kamati tendaji ya Bunge *Sports Club* leo jioni. Nadhani hicho kikao

kimeshafanyika maana ilikuwa ni saa kumi. Kama ni baada sawa kwa sababu Mheshimiwa Iddi Azzan aliandika saa kumi jioni na saa kumi imeshapita, kwa hiyo ni baada ya kikao hiki.

Halafu ninatangazo lingine kutoa Ofisi ya Spika linasema kwamba naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ya kilimo cha pamba kuwa wakutane baada ya kuahirisha kikao cha Bunge kwenye ukumbi wa Pius Msekwa ili kuzungumzia matatizo yaliyopo kwenye zao hilo. Baada ya kuahirisha kikao hiki.

Halafu ninalotangazo linguine, *TANAPA* kwa kushirikiana na Kampuni ya *MINCCO Company,* wanaendesha zoezi la uhamasishaji wa kupigia kura vivutio vya Tanzania kuingia katika maajabu saba ya asili ya Afrika. Waheshimiwa Wabunge wote mnahamasishwa kushiriki zoezi hilo katika mlango wa kuingilia jengo la utawala hapa Bungeni. Kwa Watanzania wote nchini wanaotusikiliza, zoezi hili linaendelea katika vituo mbalimbali katika maeneo ya nchi yetu. Kwa hiyo, Watanzania wote tunahamasishwa tujitokeze kwa wingi kupigia kura vivutio hivi.

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji bado ni ndefu na bado ninawachangiaji kama 12, sasa kama nilivyosema itabidi tuwasilishe taarifa ya kazi hii ya leo kwa Mheshimiwa Spika tukizingatia kwamba kesho nadhani ni siku yetu ya mwisho ya Bunge kwa mujibu wa ratiba ya Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, masuala yote ya nini kifanyike, nadhani yataamuliwa kwa kuona busara ya Mheshimiwa Spika, itakuwa inaangaliaje suala hili.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa shughuli za leo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

*(Saa 1.45 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 9 Novemba, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*

## VIAMBATISHO

*(Hapa ni Hoja jinsi zilivyowasilishwa Bungeni)*

### MAELEZO YA HOJA BINAFSI JUU YA KUSITISHA UGAWAJI WA ARDHI HADI TATHMINI KINA ITAKAPOFANYIKA KUJUA KIASI CHA ARDHI KILICHO MIKONONI MWA WAGENI

***[Chini ya Kanuni ya 54(1) na (2)]***

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mujibu wa Kanuni namba 54(1) , (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 naomba kutoa hoja binafsi ya kuitaka serikali kusitisha zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji ( wa ndani na wa nje) mpaka hapo tathmini ya kina itakapofanyika kuweza kubaini ni kiwango gani cha ardhi kiko mikononi mwa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika miaka ya hivi karibuni, kufuatia mtikisiko wa uchumi duniani uliokwenda sambamba na upungufu wa chakula , tumeshuhudia wimbi kubwa la wawekezaji kutoka nje ,wakinunua au kumilikishwa maeneo makubwa ya ardhi nchini, kwa maelezo kwamba wana nia ya kuwekeza kwa manufaa ya wananchi wenyeji na Taifa kwa ujumla , hali ambayo itaweza saidia upatikanaji wa ajira , kukuza uchumi na kupunguza umasikini .

Kwa kadiri gharama za Chakula na uhitaji wa Chakula duniani unavyoongezeka ndivyo na kasi ya mahitaji ya ardhi yanavyoongezeka , wawekezaji wanaona ardhi kama biashara nzuri na yenye tija katika miaka ya baadae. Na kwa nchi tajiri zinazoagiza vyakula toka nje ( China,Japan,Korea ya Kusini ,Saudi Arabia nk.) wanaona umiliki wa mashamba makubwa kama njia ya kujihakikishia usalama wa chakula katika nchi zao. Na wakati huo huo Makampuni binafsi makubwa ya kimataifa wanaiona hii kama fursa ya kujitanua kibiashara na kutengeneza faida kubwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Inakadiriwa kwamba kati ya mwaka 2001 hadi 2010 kulikuwa na maombi ya ardhi zaidi ya hekta milioni 203 katika nchi zinazoendelea. Hii ni sawa na maombi ya hekta 55,616 kila siku katika kipindi cha miaka 10[1]. Halikadhalika nchini Tanzania katika miaka ya karibuni takriban hekta milioni nne zimeripotiwa ‘kuombwa’ na wawekezaji wa nje kwa kilimo cha mazao ya mafuta **(AGROFUEL)** na Chakula.

**Mheshimiwa Spika,**
Kasi ya maombi ya ardhi ,na hatimaye kumilikishwa ardhi wageni, imegeuka shuruba kwa wananchi , wengi wao wakiwa ni wakulima wadogo wadogo ambao wamejikuta wakiondolewa kwa katika maeneo yao ya asili ili kuwapisha wageni. Wengi wao wakiachwa hohe hahe, na katika lindi la umasikini mkubwa. Hii inatokana na ukweli kwamba **kumekuwa na tafsiri ambayo sio sahihi, kwamba ardhi wanayopewa wawekezaji haina wenyewe/haina mtu /haitumiki . Wakati ukweli ni kwamba maeneo mengi kama sio yote yalikuwa yanatumiwa n a wakulima wadogo .**

**Mheshimiwa Spika,**
Hali halisi inaonyesha kwamba , ni sehemu ndogo sana ya ardhi inayochukuliwa na wageni inatumika kwa manufaa ya kutatua/kupunguza matatizo ya njaa katika nchi husika . **Hali kadhalika** maeneo mengi ardhi yanayochukuliwa na wawekezaji hao huwa hayaendelezwi kama inavyopasa , na yale ambayo yanaendelezwa , yanaendelezwa kwa kiwango kidogo sana huku wananchi wengi wakiachwa pasi na ardhi ya kutosha kwa kilimo. Na katika hatua nyingine, wawekezaji baada ya kupata /kumilikishwa ardhi kwa bei ya kutupa, hawaitumii,wanasubiri ipande thamani , kisha kuiuza kwa faida kwa wawekezaji wengine.

[1] ILC ( 2011) 'Land Rights and the Rush for Land', http://www.landcoalition.org/cpl/CPL- Synthesis-report.

**Mheshimiwa Spika,**
Ninaliomba Bunge lako tukufu , likubaliane na hoja ya kuitaka Serikali kusitisha zoezi la ugawaji wa ardhi ili kuweza kutoa fursa ,kama nchi kuweza kujitahmini kwa kina, wapi tulikosea ili tuweze kujipanga upya kwa manufaa ya nchi na wananchi. Hii inatokana na ukweli kwamba hata wizara ya ardhi leo wakitakiwa kutoa taarifa sahihi ya ardhi kiasi gani iko chini ya miliki ya wageni,hawana takwimu sahihi,zaidi ya zile chache zilizopatikana kupitia Tanzania Investment Centre (TIC) na ambazo pia zimethibitika kuwa na mgogoro mkubwa kutokana na taratibu kutofuatwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Mifano mingi inaonyesha kwamba kumekuwa na ubabaishaji mkubwa sana na kuumizwa sana kwa wananchi , na mbaya zaidi katika mazingira mengine serikali imekuwa kuwadi wa wawekezaji dhidi ya wananchi wake. Kuna haja kubwa kwa waheshimiwa wabunge kutambua kuwa matatizo ya ardhi yanayoikumba Rufiji, Kilombero, Bagamoyo, Kisarawe na lugufu yanaikumba pia Muheza, Pangani, Katavi ,Meatu, Kinondoni, Njombe na Ngorogoro. Hivyo basi kuna haja kubwa ya kujenga mshikamano kwa kuunganisha nguvu ili kulinda maslahi na rasilimali za umma. Nitatoa mifano michache, kuonyesha uzito wa tatizo hili:

**Bonde la Mto Rufiji (Rufiji River Basin)**
Hili ni eneo lenye ukubwa wa Km za mraba 176,000. Linajumuisha Rufiji Delta, Luwero,Kilombero na Mto Ruaha..93% ya wakazi wa maeneo wanaozunguka eneo hili wapatao 500,000 wanajishughulisha na kilimo, kama wakulima wadogo wadogo. Kutokana na umuhimu na unyeti wa eneo husika kumekuwa na wimbi kubwa la makampuni ya kigeni, wakipeleka maombi moja kwa moja kwenye vijiji au kwa kupitia baadhi ya vyombo vya serikali (RUBADA-Rufiji Basin Development Authority ) ambavyo vimeacha majukumu yake na kugeuka kuwadi wa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,**
Makampuni yafuatayo; (SEKAB Tanzania Ltd (Sweden), African Green OIL Ltd , SAP Agriculture Ltd (Turkey ), RUBADA na Korean Rural Community Corporation , Kilombero Plantation Ltd ( British) , Kilombero Valley Teak Co. Ltd ( British) , Kilombero Sugar Co. Ltd (South Africa), Kilimo cha Yesu ( Uswiss), na Eurovistas (India) ni kati ya makampuni yaliyomilikishwa ardhi iliyokuwa inatumiwa na wanakijiji kwa shughuli za kilimo. Wengi wao wakitolewa kwa nguvu ili kuwapisha wawekezaji kwa kurubuniwa kwa kauli tamu.Wakiahidiwa kuletewa maendeleo. Ahadi ambazo nyingi zimegeuka za uongo huku tayari vijiji vikiwa vimepoteza uhalali wa kutumia ardhi yao.

**Mheshimiwa Spika,**
Taarifa zinaonyesha kwamba katika ukanda huu , ukiacha makampuni ya Kilimo cha Yesu (Uswis) na Kilombero Sugar Co, kilombero Plantation Co na Kilombero Valley Teak(British), wawekezaji wengine waliokabidhiwa maelfu ya ardhi ya watanzania wameyaendeleza kidogo

sana au kuyatelekeza kabisa mashamba ! inawezekana wakisubiri ardhi ipande thamani wawakabidhi wenzao kwa gharama kubwa .[2]

**Kisarawe**:

Sun Biofuels Ltd ni kampuni ya kiingereza inayojishughuliza na kilimo Jatropha . Wanahisa wake wakubwa ni kampuni ya Sun Biofuels Plc ya Uingereza yenye hisa **88%**, Julian ozanne ( mwingereza) mwenye hisa **10%** na watanzania wawili, Daudi Makobore na Herbert Marwa wenye hisa 2% **(yaani 1% )**.

Inasemekana mwekezaji huyu alipanga kuwekeza kiasi shilingi bilioni 25.3 za kitanzania, lengo likiwa kujenga mtambo wa kufulia mafuta na kilimo cha Jatrofa ( pamoja na mihongo kwa ajili ya kuwalisha vibarua). Ilikadiriwa kutokana na uwekezaji huo zingepatikana ajira za kudumu 1,500, na ajira za ziada kwa vibarua hasa wakati wa uvunaji.

[2] Land Grabbing in a post investment period and popular reaction in the Rufiji River Basin. A Research Report by Haki Ardhi,2011. Study carried out by Dr . Abunuwasi Mwami of the Department of Sociology , University of Dar es salaam and Dr Ng'wanza Kamata of the Department of Political Science , University of Dar es salaam

Mwaka 2009 Kampuni ilifanikiwa kupata eneo lenye ukubwa wa hekta 8,211 kutoka vijiji 11 vya ( Mtamba, Muhanga, Marumbo,Palaka, Kidugalo, Kurui (40% ya eneo la kijiji lilichukuliwa ),Mtakayo, Vilabwa , Mitengwe, Mzenga 'A' and Chakaye. Hata hivyo mwezi Oktoba 2011, mradi husika ulisamama kutokana na ukosefu wa fedha, na mustakabali wa ardhi ya kijiji haujulikani.

Mwanakijiji mmoja wa **kijiji cha Palaka**, Kisarawe alinukuliwa akisema kwamba walikubali kuwaachia ardhi wawekezaji kwa mdomo, pasi kuandikiana popote kwa sababu waliaziamini ahadi zao za kutoa huduma za jamii i.e maji, barabara,shule nk, lakini hakujua kiasi gani cha eneo lake kinapaswa kuchukuliwa kwa sababu hawakuwa na nyaraka zozote za kuonyesha mipaka ya shamba lake. **Hakuwa anafahamu haki zake za kisheria**, hivyo hakujua madhara ya kile alichokikubali mpaka alipopoteza ardhi yake yote bila kulipwa fidia.[3]

Mwananchi mwingine wa kijiji **cha Kurui,** alinukuliwa akisema kuna tofauti kubwa kati ya **makubaliano ya kutoa ardhi na kushiriki katika mkutano wa kijiji**. Anadai kwamba kushiriki kwao katika kikao cha kijiji ,kulichukuliwa kama kukubali kutoa maeneo yao . Hakuingia makubaliano na mtu yeyote kutoa eneo lake.[4]Eneo lilichukuliwa na mwekezaji , majina ya mahudhurio yalitumika kama kielelezo kuonyesha kama waliafiki,wakati hawakufanya hivyo.

[3] Participant in Community focus Group discussion , Palaka Village , Kisarawe District , December 3 , 2010 cited in Frederic Mousseau et al . "Understanding Land Investment Deals in Africa – Country Report Tanzania"

[4] ibid

**Rukwa**:

**Mheshimiwa Spika**

Eneo hili ,linahusisha Hekta 80,317 (Katumba) na 219,800 (Mishamo) kwa ajili ya Kampuni ya kimarekani ya Agrisol. Majadiliano yanaratibiwa na viongozi wakubwa sana Serikalini. Mradi huu

umejikita kwenye uendelezaji wa mashamba makubwa , na matumizi ya mbegu zenye viini tete (GMO). Ili kufanikiwa kwa mradhi huu wakulima wadogo wadogo wapatao 162,000 walitakiwa kuhama kumpisha mwekezaji huyo wa kigeni.

Licha ya kelele nyingi kupigwa juu ya makosa ya kiufundi ambayo serikali inayafanya kwa kutaka kulikabidhi eneo kubwa na lenye rutuba kwa wageni, na licha aliyekuwa mshirika muhimu wa Agrisol IOWA State University College of Agriculture, aliyekuwa mhimili muhimu wa mwekezaji huyu hasa katika kuwasaidia wakulima wadogo kujitoa baada ya kugundua kwamba mwekezaji huyu hana dhamira ya kuisaidia nchi na wakulima wadogo zaidi ya kujinufaisha kibiashara. Na kwamba alikitumia Chuo husika ili apate uhalali wa kukubalika kirahisi kama mwekezaji mahiri. Serikali inaonekana bado imeziba masikio!

**Kigoma**

Wawekezaji walionunua ardhi mkoa wa Kigoma ni Agrisol na FELISA.

FELISA amenunua ekari 3000 katika wilaya ya uvinza kijiji cha basanza kata ya uvinza. Wawekezaji hawa wamewakuta wakulima na wafugaji katika maeneo haya. Wafugaji na wakulima wakagoma kuondoka kwakuwa walikuwa wakiendesha maisha Yao kutegemea ardhi hiyo Huu ni ushahidi dhahili kuwa hakuna ziada ya ardhi ukilinganisha na mahitaji. Mwekezaji kwa kushirikiana na vyombo vya dola alianza zoezi la kuwatoa wananchi mwezi Mei mwaka huu akitumia vikosi vya mgambo kupiga wananchi, kuchoma nyumba, kuharibu mazao na halikadhalika kuwafungulia wananchi mashtaka!

**USHAHIDI ZAIDI KUHUSU MGOGORO HUU TAYARI KUNA KESI MAHAKAMA YA MWANZO MWANDIGA KIGOMA KATI YA WAKAZI WANAOGOMA KUHAMA NA MWEKEZAJI.**

**AGRISOL**

Mwekezaji huyu amepewa hekta elfu 10,000 eneo la Lugufu. Eneo hili ndio ili kuwa kambi ya wakimbizi. Na eneo hili ndio limetengwa kuwa Makao makuu ya wilaya . Kwa mujibu wa Mbunge wa Kigoma Kusini (ambaye eneo lenye mgogoro liko ndani ya jimbo analoliwakilisha), Mhe David Kafulila alipozungumza  na watendaji wa halmashauri walikiri kuwepo shinikizo kutoka ngazi za juu.

Na hii inatokana na mantiki ya kawaida tu kuwa uamuzi wa kumpa mwekezaji huyu Eneo hili ni Sawa na kuamua Makao makuu ya wilaya ya uvinza yazungukwe na shamba na mwekezaji. Hivyo mji ambao ni Makao makuu hautatanuka kwasababu utakuwa eneo dogo sana lililozungukwa na shamba. Nasema eneo dogo kwasababu mpaka sasa haijafahamika Makao hayo makuu yatawekwa wapi wakati eneo lote kashapewa mwekezaji. Labda serikali **imwombe** Agrissol eneo la kujenga wilaya.

**Mheshimiwa Spika,**

Zaidi ya mkanganyiko huo pia kuna tatizo la mahitaji ya ardhi, wakazi wa eneo la jirani,wanaotoka Uvinza na Mwamila wanahitaji kulima katika eneo hili lakini wanazuiwa. Taarifa ya mahitaji ya eneo hili kwa wakulima wakawaida ipo ofisi ya mkuu wa mkoa Kigoma.Mkuu wa Mkuu wa Mkoa anakiri kuwa ni tatizo, na kupendekeza labda watu walime kwa muda wakati mwekezaji hajafika. Wakazi mwamila walifanya jaribio la kutaka kulima mwaka huu wakafukuzwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Mchakato mzima wa agrossol kupewa eneo halikuridhiwa na wana kijiji,halmashauri na wataalamu walishinikizwa. Na isisitizwe kuwa uamuzi huu unakinzana na juhudi za serikali yenyewe kusukuma wananchi katika kilimo kwani wilaya ya uvinza Hivi sasa mbunge amekopa trekta nne ili kusukuma kilimo kwa yeye kulima na wananchi kulimiwa kwa bei ya chini kuliko bei ya serikali.Halmashauri awali ili kuwa na kituo chenye trekta mbili hapo lugufu Kama kituo cha huduma ya matrekta ya kilimo kwanza, pia halmashauri imenunua trekta tano kwa ajili ya kusukuma kilimo wilaya hii. Juhudi zote hizi ambazo ni matunda ya mkopo ya SUMA JKT, INAKWAMISHWA NA UAMUZI WA SERIKALI KUUZA ARDHI.

**Mheshimiwa Spika,**
Ni muhimu ikaeleweka kwamba,hakuna anayepinga umuhimu wa uwekezaji, lakini ni muhimu vile vile ikaeleweka kwamba hatutaweza kuendelea kama tukikabidhi kila kitu kwa wageni. Sote tunajua ni kwa namna gani dhahabu, almasi na Tanzanite zimetumika kujenga uchumi wa mabeberu! Hatuwezi kufanya makosa tena kwenye rasilimali hii muhimu ya ardhi inayopanda thamani kwa kasi sana! Uchumi hauwezi kuachwa uendeshwe na watu wa nje!

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na uwekezaji kutoka nje wa makampuni makubwa uchumi wa Tanzania unarekodiwa kukua kwa asilimia 7. Hiki ni kiasi kikubwa kinachoifanya nchi hii kuwa miongoni mwa nchi 20 kileleni kwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi dunia lakInI wakatihuohuo inasikitisha kuona nchi hii ni miongoni mwa nchi 20 duniani. Hii inatokana na ukweli kuwa kilimo kinachoajiri 70% ya watanzania kimeachwa, njia ya kuondoka kwenye mlinganyo(equation) hiyo ni ARDHI. wakulima wadogo wagawiwe ardhi, wawezeshwe zana na ufundi kwa kilimo.

**Mheshimiwa Spika,**
Mambo kadhaa yamejitokeza:

1) Uvunjwaji wa haki za binadamu
2) Kutokuzingatiwa kwa sheria inayotaka wananchi waarifiwe mapema washirikishwe na kupewa taarifa sahihi, ili wafanye uamuzi ulio sahihi kwa maendeleo yao (the principle of free, prior and informed concent- FPIC)-kuhusiana na mradi husika.

3) Mikataba iliyotawaliwa na usiri mkubwa, na wakati mwingine sheria za nchi kupuuzwa .

4) Serikali kulipwa fedha kidogo sana. Wastani wa gharama ya kukodi ardhi ni shilingi 200 kwa hekta kwa mwaka. Na muda wa kukodisha ardhi kisheria ni miaka 99.Gharama hii haijalishi eneo shamba lilipo au mazao yanayozalishwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Inawezekana kabisa Tanzania tukawa hatujafikia hali mbaya kama ilivyo kwa nchi nyingine..... more than 30% of the land in liberia has been handed out in large scale concessions in the past five years , Cambodia , inakadiriwa linalokadiriwa kuwa 56-63% of **all arable** land in the country has been handed out to private companies . There is an opportunity for the government , Tanzanians and all concerned actors to ensure transparency and open debate for the best way forward..

Ni muhimu kufanya maamuzi sasa . Maamuzi tutakayoyafanya sasa yatakuwa na athari chanya ama hasi kwa kizazi kijacho . Inakadiriwa ifikapo mwaka 2050 watanzania tutakuwa milioni 150, kama leo ardhi yetu tunagawa kwa wageni kwa muda wa miaka 99, tunaweka akiba gani kwa kizazi kijacho? Nini usalama wa Chakula na Uchumi kwa Tanzania ya kesho?

## HOJA BINAFSI KUHUSU KUSITISHA UGAWAJI WA ARDHI KWA WAWEKEZAJI HADI TATHMINI YA KIASI CHA ARDHI ILIYOGAWANYWA UTAKAPOFANYIKA

***[Chini ya Kanuni ya 54(3)]***

**Mheshimiwa Spika,**
**Kwa kuwa** rasilimali ardhi ndio urithi pekee wa asili wa mtanzania katika kujitafutia riziki na kuendesha maisha yake;

Na kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka wakati ukubwa wa ardhi hauongezeki jambo ambalo linaonesha dhahiri kwamba kuna hatari ya kiasi cha ardhi kilichopo kisitosheleze mahitaji halisi ya wananchi;

Na kwa kuwa kumekuwa na ugawaji ardhi kwa wawekezaji hasa wa nje usiojali mahitaji ya ardhi kwa wananchi siku za mbeleni;

Na kwa kuwa imebainika kwamba uwekezaji katika ardhi unaofanywa na makampuni ya nje haujawasaidia wananchi kwa maana ya fursa za ajira na upatikanaji wa chakula kwa kiwango kilichoahidiwa na Serikali na makampuni hayo;

Na kwa kuwa ugwawaji huu wa ardhi kwa wawekezaji unakwenda sambamba na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na wananchi waliokuwa katika maeneo hayo kupigwa, kuvunjiwa nyumba zao na kufukuzwa bila kulipwa fidia;

Na kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zoezi la ugawaji ardhi kwa wawekezaji linakiuka sheria za nchi ambazo zinataka wananchi waarifiwe mapema juu ya ugawaji huo wa ardhi na kushirikishwa kikamilifu ili waweze kufanya maamuzi sahihi kwa maendeleo yao jambo ambalo halifanyiki;

Na kwa kuwa mikataba ya ugawaji wa ardhi inafanyika kwa usiri mkubwa jambo ambalo linaashria mazingira ya rushwa na kutia shaka kama maslahi ya nchi yanazingatiwa;
Na kwa kuwa Serikali inapata kodi kidogo sana kutokana na uwekezaji katika ardhi ( yaani shilingi 200 kwa hekta kwa mwaka) na ikizingatiwa muda wa kukodisha ardhi kisheria ni miaka 99;

Na kwa kuwa asilimia 80 ya watanzania wanategemea ajira katika sekta ya kilimo ambacho msingi wake ni ardhi;

Na kwa kuwa Ibara ya 63(2)(c) na (d) ya Katiba ya Jamjhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inasema kwamba: “Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza; kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu na wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo; kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria”;

HIVYO BASI, naliomba Bunge liazimie:

1. KWAMBA, zoezi la ugawaji ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji.
2. KWAMBA, tathmini ya kina ifanyike kuweza kubaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia serikali za vijiji kinyume na matakwa ya sheria ya ardhi Na. 5 ya mwaka 1999.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

…………………………………..

**Halima James Mdee(Mb)**
**Jimbo la Uchaguzi-Kawe**
**05.11.2012**

## HOJA BINAFSI YA KABWE ZUBERI ZITTO(MB) KUHUSU KUITAKA SERIKALI KUCHUKUA HATUA DHIDI YA WATANZANIA WALIOFICHA FEDHA HARAMU NJE YA NCHI

***[Chini ya Kanuni ya 54(1) na (2)]***

**UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,**
Mnamo tarehe 2 Novemba 2012 niliwasilisha barua ya kusudio la kuwasilisha Bungeni Hoja binafsi kuhusu suala hilo hapo juu. Lengo la Hoja binafsi hiyo ni kuitaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwasiliana na Taasisi ya Benki ya Dunia kupitia kitengo cha 'Assets Recovery' kurejesha fedha haramu zilizofichwa na Raia wa Tanzania katika Mabenki huko nchini Switzerland. Ofisi yako ilinitaka nilete maelezo ya ziada kuhusu hoja hiyo ili ipatiwe nafasi ya kupangwa kwenye ratiba za Bunge. Baada ya kuleta maelezo hayo Ofisi yako imenipa nafasi kuwasilisha hoja hii mbele ya Bunge lako tukufu. Kwa heshima na taadhima ninawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu hoja hii muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Taifa letu linaziba mianya ya ufisadi na hususani utoroshwaji wa fedha za kigeni za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwezi Juni mwaka 2012, Benki Kuu ya Switzerland (National Bank of Switzerland) ilitoa taarifa kwa umma kuhusu raia wa mataifa mbalimbali duniani wenye dhamana kwenye mabenki nchini humo. Benki hiyo ilitangaza kwamba Jumla ya dola za Kimarekani milioni 196 (milioni mia moja tisini na sita) zilikuwa zimehifadhiwa kwenye akaunti za mabenki mbalimbali nchini humo na kwamba wenye fedha hizo ni Raia wa Tanzania. Fedha hizo ni zaidi ya shilingi bilioni 314 (mia tatu kumi nanne bilioni) ukizibadilisha kwa thamani ya fedha za Tanzania.

Fedha hizi ni sehemu tu ya fedha ambazo watanzania wanazificha katika mabenki mbalimbali ya nje ya nchi na hasa visiwa kama Jersey, Mauritius na Cayman Islands maana nchi nyingine hazina utaratibu huu wa kuweka wazi kama ilivyo kwa nchi ya Swistzerland kwa mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika,**
Gazeti la The Gurdian On Sunday la tarehe 23 Juni 2012 lilimnukuu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ndugu Edward Hosea akisema kwamba siku ya jumatatu tarehe 24 Juni mwaka 2012 angeandika Barua kwenda Mamlaka za Switzerland kutaka kupewa orodha ya majina ya raia wa Tanzania wenye fedha katika akaunti zilizotajwa. Hata hivyo mpaka ninaleta maelezo haya umma wa Watanzania haujalezwa kama barua hiyo iliandikwa na majibu yake yalikuwa ni nini. TAKUKURU ndio mamlaka pekee hapa nchini ambayo inaweza kupata orodha ya majina ya watu wenye mabilioni haya kwa njia za halali na hasa kwa watu ambao ni 'Politically Exposed Persons'kama Wabunge na waliowahi kuwa wabunge, Mawaziri na waliowahi kuwa Mawaziri na viongozi wengine wa ngazi za juu katika Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kiufupi, toka taarifa za Benki ya Taifa ya Switzerland kutangazwa, Serikali haijachukua hatua yeyote ya maana kuhakikisha kuwa suala hili linafanyiwa uchunguzi wa kina na hatua stahili dhidi ya watoroshaji wa fedha hizo zinachukuliwa ikiwemo kurejeshwa kwa fedha hizo nchini kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Ikumbukwe kwamba katika watanzania wenye fedha huko nje wapo ambao fedha zao wamezipata kihalali kutokana na shughuli za kibiashara na wapo ambao wamepata fedha hizi kwa njia za rushwa. Uchunguzi wa kina ni muhimu sana ili kuweza kutofautisha kati ya Fedha haramu na fedha halali. Vilevile uchunguzi unatakiwa kutofautisha katika watu wenye fedha halali kama walifuata taratibu za kisheria za nchi zinazoruhusu raia wa Tanzania wanaoishi Tanzania kuwa na akiba ya fedha za kigeni nje ya Tanzania. Kitendo cha Serikali kukaa kimya bila kuchukua hatua kinaashiria ama kutotimiza wajibu au kwamba wanaopaswa kuchukua hatua ni washirika wa utoroshaji huu wa fedha za nchi na kuzificha katika mabenki ya nje.

**Uchunguzi wa chanzo cha Fedha.**
**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mujibu wa Taarifa ya Global Financial Integrity (GFI) ya mwaka 2008, jumla ya dola za kimarekani bilioni 8 (dola bilioni nane) zimetoroshwa kutoka Tanzania kati ya mwaka 1970 mpaka 2008. Kwa bei ya sasa ya dola za kimarekani fedha hizi ni sawa na shilingi trilioni 13 (trilioni kumi na tatu). Mpaka Mwezi Julai mwaka 2012 Deni la Taifa kuanzia mwaka 1961 lilikuwa ni dola za kimarekani bilioni kumi. Hii maana yake ni kwamba fedha zote zilizotoroshwa kutoka Tanzania katika kipindi cha miaka 38 kingeweza kulipia asilimia themanini ya Deni la Taifa. Mwaka 2012/2013 Bunge limeidhinisha jumla ya shilingi trilioni 1.9 kulipia Deni la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,**
Sehemu ya Fedha hizi zilizotoroshwa zilitokana na ufisadi, nyingine zilitokana na ukwepaji wa kodi na nyingine zilitokana na madeni ambayo Serikali iliingia ambapo sehemu kubwa ya Madeni ilibaki huko huko ughaibuni lakini bado Watanzania wanalipa madeni hayo. Hata hivyo Fedha zilizotokana kutokana Ufisadi na zile za ukwepaji kodi ni nyingi zaidi katika fedha zilizotoroshwa kutoka Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mfano kati ya mwaka 2003 - 2005 Tanzania iligubikwa na ufisadi mkubwa sana wa Fedha kutoka Benki ya Tanzania ambapo jumla ya shilingi bilioni 155 zililipwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwenda Benki ya NedBank ya Afrika Kusini kama malipo ya mkopo ambao Serikali iliudhamini kwa ajili ya mradi wa uchimbaji dhahabu wa meremeta. Fedha hizi zilikuwa ni mara ya kumi na tano ya mkopo uliodhaminiwa na Serikali. Uchunguzi wetu unaonesha kuwa asilimia

70 ya fedha za mradi wa meremeta ziliishia kwenye Benki nchini Switzerland kupitia nchi ya Mauritius.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Meremeta ambayo baadaye ilibadilishwa jina na kuitwa TanGold ilianzishwa kama mradi wa kutorosha mabilioni ya fedha za nchi kwenda kwa uhusika mkubwa sana wa Serikali. Nawasilisha mezani kwako barua kutoka Ofisi ya Rais Ikulu ya tarehe 20 Agosti 2001, yenye kumbukumbu nambari SHC/M.100/4/A kwenda Benki ya Deutsche Bank tawi la Uingereza kuitambulisha Kampuni ya Meremeta na Kampuni ya Nedcor Trade Services Limited ya Afrika ya Kusini ili ipewe mkopo. Barua hiyo inatambulisha miradi miwili ya dhahabu (mgodi wa Tembo na Mgodi wa Buhemba) kwamba ni miradi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Baada ya barua hii yaliyotokea ni mtandao mpana wa kuiba fedha za Tanzania kwenda Afrika Kusini, baadaye Mauritius na kasha kuishia kwenye akaunti za watu binafsi nchini Switzerland  na visiwa vingine vya ukwepaji kodi (tax havens). Kufuatilia barua hii kutoka Ikulu, mkopo wa dola za kimarekani milioni kumi zilipatikana. Hata hivyo Serikali ya Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania ililipa Benki ya NedBank jumla ya dola za Kimarekani 138 milioni, dola milioni kumi kati ya hizi zililipwa kupitia kampuni ya Deep Green Finance.

**Mheshimiwa Spika,** nilifanya uchunguzi binafsi kuhusu suala hili. Nilijaribu kuwasiliana na Benki ya NedBank ili kuweza kupata uhakika wa watu waliofaidika na uchotaji huu mkubwa na wa kihistoria wa fedha za umma. Ufuatiliaji huu haukuwa na matokeo mazuri sana. Hata hivyo taarifa nilizokusanya zimeonyesha hatari kubwa namna ambavyo watanzania wenzetu wenye mamlaka wanavyokwapua fedha za umma kwa faida yao. Nyaraka zote za wizi na utoroshaji huu wa fedha na mawasiliano yangu na watu wa Benki ya NedBank nitayawasilisha mbele ya Kamati ya  Bunge ninayopendekeza kuundwa ili kutazama suala hili.

**Mheshimiwa Spika,** Kuna masuala yanayohusu usalama wa nchi kutokana na kashfa hii ambayo pia ningependa kuyaonyesha katika Kamati ninayopendekeza kuundwa. Nyaraka hizo zinaonyesha silaha na aina za silaha zilizonunuliwa na kutoka nchi gani na kwamba silaha hizo ziliishia wapi. Nimeona kwamba kuyasema masuala haya waziwazi kunaweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Hata hivyo masuala haya ni lazima yafahamike ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa dhidi ya watendaji wa Serikali watakaokutwa na makosa.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zilizoibwa na kutoroshwa kupitia kampuni ya Meremeta na kampuni ya Deep green ziliishia kwenye akaunti za watu binafsi nje ya nchi. Hata hivyo mara baada ya kuundwa kwa kampuni ya TanGold, jumla ya dola za kimarekani milioni kumi ziliwekwa kwenye akaunti ya Kampuni hiyo katika Benki ya NBC, Corporate Branch. Nambari ya akaunti hiyo pia itatolewa katika kamati ninayoomba kuunda kwa ajili ya uchunguzi wa kina.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwaka 2004, 2006 na 2007 Tanzania iligawa vitalu vya kutafuta mafuta na Gesi katika maeneo mbalimbali nchini. Uchunguzi wetu unaonyesha kuwa zaidi ya dola za kimarekani milioni 56 zililipwa kwenye akaunti za watu binafsi nchini Switzerland kutoka kwenye kampuni zilizoshinda zabuni ya kutafuta mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika,**
Uchunguzi mbali mbali nilioufanya kwa msaada wa wachunguzi waliobobea kwenye masuala ya mifumo ya kifedha ya Kimataifa umeniwezesha kupata nyaraka zote muhimu zinazoonyesha watu na namna walivyopata fedha walizoweka katika akaunti zao nje ya Tanzania.

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha,

**HOJA BINAFSI YA KABWE ZUBERI ZITTO (MB) KUHUSU KUITAKA SERIKALI KUCHUKUA HATUA DHIDI YA WATANZANIA WALIOFICHA FEDHA HARAMU NJE YA NCHI**

***[Inatolewa chini ya Kanuni ya 54(3)]***

**Mheshimiwa Spika,**
KWA KUWA kitendo kilichofanywa na wahusika kuweka mabilioni ya fedha kwenye nchi za nje ni kinyume na sheria ya "**FOREIGN EXCHANGE ACT, 1992"**

**NA KWA KUWA** sheria hiyo kifungu cha (10) kinachosema kuwa *". (1) Subject to sub section (2), except with the permission of the Governor no person shall export from or cause to be exported from the United Republic:-*

*(a) any notes or coins which are or have been at any time legal tender in the United Republic, or*

*(b) any gold.*

*(2) There shall be exempted from the provisions of sub section (1) of this section, the exportation from and Importation into the United Republic –*

*(i) in case of any resident person traveling abroad provided that the amount of Tanzania currency does not exceed the equivalent of fifty United States dollars, or" ….* Kwa kibali cha Gavana wa Benki Kuu tu, hakuna mtu yeyote atakaye ruhusiwa kusafirisha fedha nje ya Tanzania. Na kinaeleza kuwa kwa msafiri anayekwenda nje ya nchi hatoruhusiwa kuondoa na kiasi cha shilingi ambazo zinazidi dola za kimarekani hamsini. Vile vile kwa mujibu wa Sheria hiyo kifungu cha 6 na 7 na waraka uliotolewa na Gavana wa Benki Kuu kwamba Mtanzania yeyote mwenye kutaka kufungua akaunti kwenye mabenki nje ya Tanzania lazima apate kibali cha Gavana.

**NA KWA KUWA** masharti hayo ya sheria yanaweza kuwa yamekiukwa na wahusika,

**NA KWA KUWA** ukiukwaji huo ni dhahiri kuwa fedha zilizowekwa kwenye mabenki ya nje kwa kiasi kikubwa ni fedha ambazo hazikupatika kwa njia za halali na kwamba kuna uwezekano wa ukwepaji mkubwa wa kodi,

**NA KWA KUWA**, nchi yetu imekuwa katika matatizo makubwa ya fedha za kigeni, jambo ambalo limepelekea nchi kushusha thamani ya shilingi ili kukabiliana na gharama za manunuzi ya bidhaa nje ya nchi,

**NA KWA HIYO BASI**, ninaliomba Bunge hili liazimie:

1. Kwamba Serikali iwasiliane na Benki ya Dunia ili kupitia Kitengo cha Assets Recovery Unit ili mabilioni ya Fedha yanayomilikiwa na Watanzania katika mabenki ya nchini Switzerland na

visiwa na maeneo mengine yote ambapo hufichwa fedha ili kukwepa kodi yarudishwe nchini mara moja.

2. Kwamba Serikali ilete muswada wa Sheria Bungeni ifikapo Mkutano wa 11 wa Bunge kwamba itakuwa ni marufuku kwa Kiongozi yeyote wa Umma au mume au mke wake au watoto wake kuwa na akaunti katika mabenki nje ya nchi.

3. Kwamba katika muswada tajwa hapo juu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aimarishiwe mamlaka ya kutoa kibali kwa Mtanzania yeyote anayetaka kufungua akaunti ya Benki nje ya nchi na kwamba kila mwaka Gavana atatangaza kwenye Gazeti la Serikali na magazeti yanayosomwa na wananchi wengi orodha ya Watanzania walioomba na walioruhusiwa kuwa na akaunti ya Benki nje ya Tanzania.

4. Kwamba Watanzania wote wenye akaunti za fedha nje waeleze wamezipataje na TAKUKURU wachukue hatua za kisheria dhidi ya watu wote wenye kumiliki fedha na mali kinyume na mapato yao halali.

5. Kwamba Serikali, katika mkutano wa Bunge wa 11 ilete taarifa ya hatua ilizochukua ili kuziba mianya ya utoroshaji wa fedha nje ya Tanzania.

6. Kwamba Serikali katika Bajeti ya mwaka 2013/13 itaanzisha kodi maalumu 'financial transaction tax' ya angalau asilimia 0.5 ya thamani ya 'transaction' ili kuweza kuwa na rekodi za uhakika za fedha ndani na zinazotoka nje ya nchi.

7. Kwamba Bunge lako tukufu liunde Kamati Teule kuchunguza mfumo mzima wa utoroshaji wa fedha na kufichwa nje ya nchi, kuchunguza na kupembenua fedha haramu dhidi ya halali, kuchunguza utaratibu mzima wa kugawa vitalu vya utafutaji mafuta na gesi kati ya mwaka 2004 mpaka 2008, kuchunguza mtiririko mzima wa utoroshaji wa fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania kupitia Kampuni ya Meremeta (pia Triannex pty ya Afrika Kusini na Deep Green Finance ltd) na kupendekeza hatua za kuchukua dhidi ya wahusika wote wa utoroshaji wa fedha kwenda nje.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja,

**……………………**
**KABWE ZUBERI ZITTO(MB)**
**JIMBO LA UCHAGUZI-KIGOMA KASKAZINI**
**08.11.2012**